# Nipashe

Alhamisi Oktoba 31, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580063

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Watozwa faini ya mil. 6.8/- kukiri kuiba tausi wa Ikulu

UKURASA 2




UKURASA 13

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**WAFUGAJI WATANGAZIWA NEEMA UOGESHAJI MIFUGO**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amezindua kampeni ya kitaifa ya uogeshaji mifugo nchini na kutangaza neema kubwa kwa wafugaji ambapo ng'ombe ...

**UKURASA WA 10**

**KIWANDA CHA MIFUKO MBADALA CHATOZWA FAINI**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limekipiga faini ya Sh. milioni 35 kiwanda cha kuzalisha mifuko mbadala...

**UKURASA WA 22**

**SABABU KUAJIRI WATAALAMU WA KUTOKA NJE ZAELEZWA**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), imetaja sababu ya waajiri kuajiri wataalamu kutoka nje ya nchi kuwa ni kutokana...




# Afungwa minyororo chumbani miezi 2

**AKUTWA** akiwa utupu, kila kitu afanyia hapo hapo, kisa na mkasa...

UKURASA 2

## HOJA TISA BARUA YA CHADEMA KWA JAFO

UKURASA 3



Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Ifakara, wilayani Kilombero, alipofanya ziara ya kushtukiza juzi. **PICHA: IDDA MUSHI**

# RC abaini mazito shule kongwe ya wasichana

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


**MICHEZO** MANULA ATISHA REKODI AKIPIGA YA 100 SIMBA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## Walipa mil. 6.8/- kwa kuiba tausi Ikulu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imewahukumu watu watatu kulipa fidia ya Sh. 6,890,000 na kuwaachia huru watu watatu, baada ya kukiri kukutwa na nyara za serikali ikiwamo ndege watatu aina ya tausi.

Kadhalika mahakama hiyo imetaifishwa ndege hao kuwa mali ya serikali. Pia imewaachia huru kwa masharti ya kutokutenda kosa ndani ya miezi sita.

Hukumu hiyo ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salumu Ally, baada ya washtakiwa kumwandikia Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) barua ya kukiri makosa yao.

"Mahakama hii inawaamuru washtakiwa kulipa fidia ya Sh. 6,890,000, ndege hao wanataifishwa kuwa mali ya serikali na inawaachia huru kwa masharti kwamba wasitende kosa la jinai ndani ya miezi sita," alisema Hakimu Ally wakati akisoma hukumu hiyo.

Awali, washtakiwa walidaiwa kujihusisha na genge la uhalifu, kukutwa na nyara za serikali ikiwamo ndege aina ya tausi watatu wa Ikulu ya Tanzania.

Washtakiwa hao ni David Graha, Mohammed Hatibu na Mohammed Mahamoud, wote wakazi wa jijini Dar es Salaam.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Vick Mwaikambo.

Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa shtaka la kwanza, kati ya Juni Mosi, 2015 na Oktoba 14, mwaka huu waliratibu mipango ya uhalifu kwa kujihusisha na biashara ya ndege hao wenye thamani ya Dola za Marekani 1,500 (sawa na Sh. 3,444,150).

Nchimbi alidai katika shtaka la pili, washtakiwa walikutwa na ndege watatu aina ya tausi wenye thamani hiyo ya fedha.

Wankyo alidai katika shtaka la tatu, Oktoba 14, mwaka huu eneo la Mikocheni, mshtakiwa wa tatu Mahamoud alikutwa na tausi hao.

# Afungwa minyororo chumbani miezi 2

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHADRACK Johanes (26), mkazi wa Old Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga, amefungiwa chumbani kwa miezi miwili akiwa amefungwa minyororo mikono na miguu.

Imeelezwa kuwa ndugu wa kijana huyo ambaye Nipashe imemkuta kwenye chumba hicho akiwa uchi, walilazimika kuchukua hatua hiyo baada ya kuwa amepata tatizo la akili.

Shangazi wa kijana huyo, Devota Emmanuel, aliiambia Nipashe juzi kuwa baada ya kuanza kupatwa na tatizo hilo la akili, mpwa wake alianza kupiga watu, kuvunja vioo vya magari na nyumba za watu.

Kutokana na kutumia fedha nyingi kuwalipa watu waliokuwa wanaharibiwa nyumba na magari yao na kijana huyo, Devotha alisema waliamua kumfungia ndani ili asiendelee kuwatia hasara.

Alidai kuwa walimpeleka Hospitali ya Rufani ya Bugando jijini Mwanza kupatiwa matibabu, lakini madaktari hawakubaini ugonjwa unaomsumbua, hivyo kuwapa rufani kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili.

"Kutokana na hali ngumu ya kimaisha na ukosefu wa fedha, tukaamua kurudi naye hapa nyumbani na kumfungia ndani ili asifanye fujo tena mitaani," Devotha alisema na kueleza zaidi:

"Kijana huyu ni mtoto wa kaka yangu, baba yake yuko Bukoba na ameshakata tamaa, msaada mkubwa nimebaki ni mimi na kaka yake, na sisi hatuna uwezo wa kifedha kumpeleka huko Muhimbili, ndiyo tukaamua kumfungia ndani takribani miezi miwili sasa.

"Tumemfunga minyororo hii ili asitoroke na tukimvalisha nguo ana zichana, ndiyo maana tukaamua kumwacha aishi hivyo akiwa uchi.

"Tumeweka ndoo ya kujisaidia lakini huwa anajisaidia chini na chakula chake huwa ana kula humo humo (chumbani), na mpaka sasa hatujui tufanye nini."

Kaka wa kijana huyo, Golden Johanes, alisema imekuwa vigumu kwao kumsaidia mdogo wake kutokana na madaktari kushindwa kubaini tatizo linalomsumbua.

Alisema wanaamini huenda mdogo wake huo "amechezewa kishirikina" na kwamba familia yao haina uwezo wa kifedha kumpeleka kwenye matibabu ya kibingwa Muhimbili ndiyo maana ikaamua kumfunga minyonyoro chumbani.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Shinyanga, Panuela Samwel, alilaani kitendo hicho, akieleza kuwa ni ukatili.

Aliitaka familia hiyo kumsafisha kijana huyo na kuhakikisha inamvalisha nguo, kumlaza kwenye godoro badala ya sakafuni, kumpatia chakula kwa wakati na kumhifadhi sehemu safi.

Ofisa huyo wa serikali pia aliitaka familia hiyo kuhakikisha ndani ya wiki mbili kuanzia juzi, iwe imeshajipanga kifedha kumpeleka kijana huyo kwenye hospitali zinazotoa matibabu ya ugonjwa wa akili.

Alisema kitendo cha kumficha chumbani na kumfunga minyororo kinaweza kusababisha magonjwa mengine yakiwamo ya mlipuko.

Mei 19, 2014, mtoto mwenye ulemavu wa akili (15) aligundulika wilayani Korogwe amefungiwa ndani ya chumba kwa miaka tisa kutokana na hali yake ya ulemavu.

Ilibainika aliyefanya kitendo hicho ni mama yake wa kambo ambaye alimfungia ndani ya chumba na alikuwa akijisaidia humo haja kubwa na ndogo na kuwekewa chakula katika bakuli maalum.

Pia, Julai 16, 2014, wadau wanaotetea haki za watoto walimtembelea, Apewe Mathayo (12), mtoto mwenye ulemavu wa viungo aliyefungiwa ndani kwa miaka 11.

Mtoto huyo aliokolewa na mkazi wa Kijiji cha Kamagambo, Kata ya Kiruruma, wilayani Karagwe, baada ya kutelekezwa na wazazi wake



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Dk. John Pombe Magufuli, akiongoza Kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, katika Ofisi ndogo za chama hicho, Mtaa wa Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# RC abaini mazito shule kongwe ya wasichana

**Na Idda Mushi,** KILOMBERO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, amefanya ziara ya kushtukiza katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ifakara wilayani Kilombero na kubaini baadhi ya wanafunzi wakitoroka shuleni kwenda mitaani nyakati za usiku.

Kiongozi huyo pia amebaini wanafunzi wakipewa nusu ya kiwango cha chakula kinachopendekezwa na Wizara ya Elimu huku baadhi ya walimu wakidaiwa kujihusisha kimapenzi na wanafunzi.

Imeelezwa kuwa matatizo hayo ndiyo yamechangia shule hiyo kuwa na ufaulu mbovu katika matokeo ya mtihani wa taifa wa kidato cha sita mwaka huu, ikishika nafasi ya mwisho kimkoa licha ya kuwa na majengo mazuri, walimu wa kutosha na serikali kuipatia Sh. bilioni 1.3 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu yake.

Mkuu wa Mkoa, akiambatana na baadhi ya wajumbe wa Kamati yake ya Ulinzi na Usalama, alifanya ziara hiyo ya kushtukiza juzi na kuzungumza na walimu, watumishi wengine wa shule na wanafunzi na kubaini utovu wa nidhamu ni tatizo kubwa katika shule hiyo.

Alisema serikali imetoa fedha nyingi kuigharamia shule hiyo kufanya ukarabati wa miundombinu na kulipa mishahara ya walimu, lakini nidhamu ni mbovu na watuhumiwa wakubwa ni walimu.

Alisema kutokana na wanafunzi kutotendwa haki, wamekuwa na mikakati ya siri ya kufanya uharibifu shuleni kama njia ya kufikisha malalamiko yao.

Alisema ameelezwa kuwa usiku wa kuamkia juzi, wanafunzi wawili walikamatwa usiku wa manane wakirejea shuleni baada ya kuwa wametoroka kwenda kusikojulikana.

Alisema wanaotuhumiwa kuwatorosha nyakati za usiku wanafunzi wa shule hiyo kongwe iliyoko katikati ya Mji wa Ifakara, ni walimu, ndugu za walimu na wananchi wa maeneo ya jirani.

"Huyu mwalimu aliyetorosha mwanafunzi usiku ni afadhali aondoke kabla hatujamkamata kwa sababu ataozea magereza," alitahadharisha.

"Shule hii mambo mengi hayaendi vizuri kabisa, na ndiyo maana imekuwa ya mwisho

INAENDELEA UK. 8

HABARI KITAIFA

# Mpina atangazia neema wafugaji

**Na Mwandishi Wetu,** MLELE

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amezindua kampeni ya kitaifa ya uogeshaji mifugo nchini na kutangaza neema kubwa kwa wafugaji ambapo ng'ombe mmoja ataogeshwa kwa Sh. 50 badala ya Sh. 500, huku mbuzi na kondoo wakiogeshwa kwa Sh. 10 kila mmoja.

Uamuzi huu wa serikali utawawezesha kuokoa Sh. bilioni 19 ambazo wafugaji wangezitumia kuogesha mifugo yao, lakini sasa zitatumika Sh. bilioni 2.16 tu, huku serikali ikiwapatia wafugaji ruzuku ya asilimia 90 ambapo kama wafugaji wangeendelea na gharama hiyo ya miaka ya nyuma wangetumia Sh. bilioni 21.6.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa kampeni ya uogeshaji mifugo awamu ya pili katika josho la Kikonko wilayani Mlele na baadaye mkutano wa hadhara uliofanyika Kijiji cha Majimoto, Waziri Mpina alisema kupitia mpango huo serikali itasambaza dawa ya ruzuku lita 12,546 kwenye majosho yanayofanya kazi 1,733 nchini.

Mpina aliwaambia wananchi kuwa serikali imedhamiria kuleta mageuzi kwa vitendo hasa katika sekta ya mifugo.

Alisema Ilani ya Uchaguzi ya CCM Ibara ya 25 inaiagiza serikali kuhakikisha mifugo yote inaogeshwa ili kuzuia magonjwa yote yanayoenezwa na kupe ambapo asilimia 72 ya vifo vya mifugo vinasababishwa na kupe.

Alisema uogeshaji utawezesha mifugo kujikinga na maradhi na vifo ambapo serikali itaogesha michonyo milioni 38 kwa ng'ombe, michonyo milioni 18 ya mbuzi, michovyo milioni 7 ya kondoo pamoja na michovyo 2,500 ya punda hivyo, utaliwezesha taifa kupata mifugo bora ambayo haina magonjwa.

Waziri Mpina alibainisha kuwa katika kipindi kifupi cha mwaka mmoja serikali imekarabati majosho 400, na kwamba majosho yaliyobaki ambayo hayajakarabatiwa ni 639 na kusisitiza kuwa yote yatakarabatiwa ili kuongeza kasi ya uogeshaji mifugo.

Waziri Mpina alisisitiza kuwa zaidi ya asilimia 60 ya magonjwa ya binadamu yanasababishwa na mazao ya mifugo ikiwamo nyama na maziwa, hivyo uamuzi wa serikali kuogesha mifugo pia umelenga kupambana na magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Aidha, aliagiza kila kijiji nchini kiwe na josho kwenye vijiji vyote zaidi ya 12,000 ili kila kuogesha mifugo na kusisitiza kuwa serikali itakuja na mkakati wa kuhakikisha kila kijiji kinapata josho kama sehemu ya kuboresha afya za mifugo.

Pia ameziagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha majosho yote yamekarabatiwa ndani ya mwezi mmoja, na wizara itahakikisha inasambaza dawa kwenye majosho yote mabovu.

Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera alimhakikishia Waziri Mpina kuwa mkoa huo inatasimamia maagizo yote, na kwamba hakuna mfugaji atakayeonewa au kudhulumiwa, gharama elekezi iliyotangazwa italeta neema kubwa kwa wafugaji.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Hezron Nonga, alisema uogeshaji utafanyika nchi nzima, na kuwataka wafugaji kujitokeza kuogesha mifugo yao.



Washtakiwa watatu waliokuwa wakikabiliwa na kesi ya kukutwa na nyara za serikali ikiwamo ndege watatu aina ya tausi, wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. Mahakama hiyo, imewahukumu kulipa fidia ya Sh. milioni 6.8 na kuwaachia huru baada ya kukiri kosa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hoja 9 barua ya Chadema kwa Jafo

**Na Enock Charles**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kimeandika barua kwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, kikieleza mambo tisa kisiyopendezwa nayo katika mchakato unaoendelea wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Hatua iliyofikiwa kwa sasa katika mchakato wa uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu, ni wagombea wa vyama mbalimbali kuchukua fomu kwenye ofisi za serikali za mitaa.

Distributed via ippmedia

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya chama hicho, Tumaini Makene, alisema wameandika barua kwa waziri huyo wakilalamikia kile alichokiita ukiukwaji wa taratibu za uchaguzi na kumtaka achukue hatua.

Makene alisema kuwa katika barua yao hiyo, wametoa mifano mahususi ya maeneo yanayolalamikiwa na kwamba nakala zimetumwa pia kwa ofisi mbalimbali za serikali zinazohusika na masuala ya siasa na demokrasia.

"Katika barua hiyo ambayo nakala yake imepelekwa Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, Chadema kimemtaka Waziri wa Tamisemi kuchukua hatua.

"(Waziri huyo) kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ni mamlaka ya rufani," alisema Makene katika taarifa hiyo.

MBIO ZA MWENGE

Alizitaja hoja tisa zilizoainisha na Chadema katika barua yake hiyo kwa Waziri Jafo kuwa ni pamoja na wasimamizi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kutoa nakala ambazo chama hicho kimedai kuwa hazina nembo na mihuri ya halmashauri husika kuthibitisha kuwa ni nakala halisi.

Ofisa huyo wa Chadema alisema hoja yao ya pili ni ofisi za serikali za mitaa katika baadhi ya maeneo kutokufunguliwa mapema au kutokufunguliwa kabisa, katika ni sehemu ya mipango ovu ya wagombea wao kutopewa fomu.

Chama hicho pia kinadai baadhi ya wagombea wake

INAENDELEA UK.8

# Barua kigogo Takukuru bado kwa DPP

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi inayomkabili kigogo wa zamani wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Kulthum Mansoor, umedai mahakamani bado haujapokea majibu ya barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya kukiri kutenda tuhuma hizo.

Mansoor ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na tathmini wa Takukuru, anakabiliwa na mashtaka ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha. Wakili wa Utetezi, Elia Mwingira, alidai jana kuwa DPP amemweleza kwamba amesikia kwamba kigogo huyo amemwandikia barua, lakini bado haijamfikia, hivyo kuomba mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kelvin Mhina, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, kusaidia kupata majibu ya barua hiyo.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alidai kuwa hawana hoja zaidi wanasubiri majibu ya utetezi kuhusu taarifa yao ya kuandika barua kwa DPP.

Hakimu Mhina alisema kesi hiyo itatajwa Novemba 12, mwaka huu na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi ya msingi, Mansoor anakabiliwa na mashtaka manane ya kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na kutakatisha Sh. bilioni 1.477.

Inadaiwa katika tarehe tofauti kati ya Januari, 2013 na Mei, 2018 mshtakiwa alighushi barua ya toleo (offer) ya Agosti 13, 2003 kwa madhumuni ya kuonyesha kuwa imetolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo huku akijua si kweli.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kati ya Januari, 2012 na Mei, 2017 maeneo ya Upanga, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa kwa kudanganya alijipatia Sh. milioni 5.2 kutoka kwa Alex Mavika ambaye ni mfanyakazi wa Takukuru kama malipo ya kiwanja kilichoko kijiji cha Ukuni, Bagamoyo.

Pia inadaiwa kati ya tarehe hizo, Mansoor alijipatia Sh. milioni tatu kutoka kwa Wakati Katondo kama malipo ya kiwanja kilichoko katika Kijiji cha Ukuni.

Mshtakiwa huyo pia anadaiwa kujipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Ofisa wa Takukuru, Gogo Migutah, kama malipo ya kiwanja kilichopo eneo hilo hilo.

Katika mashtaka ya tano, inadaiwa Mansoor alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa Ekwabi Majungu ambaye pia ni ofisa wa Takukuru kama malipo ya kiwanja hicho.

Mansoor anadaiwa kati ya Januari, 2012 na Mei, 2017 maeneo ya Upanga jijini Dar es Salaam, akiwa Mkurugenzi wa Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini, alijipatia Sh. milioni saba kutoka kwa John Sangwa kama malipo ya kiwanja cha eneo hilo.

Inadaiwa kuwa mshtakiwa akiwa mwajiriwa wa Takukuru, alijipatia Sh. milioni tano kutoka kwa Rose Shingela kwa ajili ya malipo hayo.

Katika mashtaka ya utakatishaji fedha, inadaiwa kati ya Januari, 2013 na Mei, 2018 huko maeneo ya Upanga, mshtakiwa alijipatia Sh. 1,477,243,000 wakati akijua kuwa fedha hizo ni haramu na ni zao la kosa tangulizi la kughushi.

# KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED (KCBL)

## Issued pursuant to regulations 7 and 8 of the Banking and Financial Instituions (Disclosures) Regulation, 2014

### CONDENSED STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT THE QUARTER ENDED 30/09/2019
(Amounts in shillings)

| | | Current Quarter Date: 30.09.2019 | Previous Quarter Date: 30.06.2019 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **ASSETS** | | |
| 1 | Cash | 3,918,609 | 11,237,197 |
| 2 | Balances with Bank of Tanzania | 259,661,853 | 260,478,137 |
| 3 | Investments in Government securities | - | - |
| 4 | Balances with other banks and financial institutions | 993,350,593 | 2,202,867,656 |
| 5 | Cheques and items for clearing | - | - |
| 6 | Inter branch float iterms | - | - |
| 7 | Bills negotiated | - | - |
| 8 | Customers' liabilities for acceptances | - | - |
| 9 | Interbank Loans Receivables | - | - |
| 10 | Investments in other securities | - | - |
| 11 | Loans, advances and overdrafts (net of allowances for probabl | 225,607,837 | 267,595,039 |
| 12 | Other assets | 182,927,084 | 86,053,791 |
| 13 | Equity Investments | - | - |
| 14 | Underwriting accounts | - | - |
| 15 | Property, Plant and Equipment | 1,181,570,009 | 1,197,442,241 |
| **16** | **TOTAL ASSETS** | **2,847,035,985** | **4,025,674,061** |
| **B.** | **LIABILITIES** | | |
| 17 | Deposits from other banks and financial institutions | - | - |
| 18 | Customer deposits | 5,672,187,157 | 5,641,584,699 |
| 19 | Cash letters of credit | - | - |
| 20 | Special deposits | - | - |
| 21 | Payment orders/transfers payable | - | - |
| 22 | Bankers' cheques and drafts issued | 3,873,216 | 2,796,056 |
| 23 | Accrued taxes and expenses payable | 78,794,704 | 59,475,621 |
| 24 | Acceptances outstanding | - | - |
| 25 | Interbranch float items | - | - |
| 26 | Unearned income and other deferred charges | - | - |
| 27 | Other liabilities | 464,601,892 | 258,639,791 |
| 28 | Borrowings | - | - |
| 29 | **TOTAL LIABILITIES** | **6,219,456,969** | **5,962,496,167** |
| 30 | **NET ASSETS/(LIABILITIES)(16 minus 29)** | **(3,372,420,984)** | **(1,936,822,106)** |
| **C.** | **SHAREHOLDERS' FUNDS** | | |
| 31 | Paid up share capital | 6,379,464,064 | 7,579,464,064 |
| 32 | Capital reserves | 453,542,327 | 453,542,327 |
| 33 | Retained earnings | (9,562,085,906) | (9,572,175,251) |
| 34 | Profit (Loss) account | (665,209,190) | (432,851,218) |
| 35 | Other capital accounts | 21,867,721 | 35,197,972 |
| 36 | Minority Interest | - | - |
| 37 | **TOTAL SHAREHOLDERS' FUNDS** | **(3,372,420,984)** | **(1,936,822,106)** |
| 38 | Contingent liabilities | - | - |
| 39 | Non performing loans & advances | 1,526,968,400 | 1,627,308,995 |
| 40 | Allowances for probable losses | 1,265,443,509 | 1,280,817,009 |
| 41 | Other non performing assets | 79,009,928 | 78,896,948 |
| **D.** | **SELECTED FINANCIAL CONDITION INDICATORS** | | |
| (i) | Shareholders Funds to total assets | -118.45% | -48.11% |
| (ii) | Non performing loans to total gross loans | 97.26% | 96.25% |
| (iii) | Gross loans and advances to total deposits | 27.68% | 28.84% |
| (iv) | Loans and advances to total assets | 7.92% | 6.65% |
| (v) | Earning assets to Total Assets | 5.49% | 5.04% |
| (vi) | Deposits Growth | 0.54% | 7.01% |
| (vii) | Assets growth | -29.28% | -44.31% |

### CONDENSED STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE QUARTER ENDED 30/09/2019. (Amounts in shillings)

| | | Current Quarter Date: 30.09.2019 | Comparative Quarter (Previous Year) Date:30.09.2018 | Current Year Cumulative Date: 30.09.2019 | Comparative Year (Previous Year) Cumulative Date:30.09.2018 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Interest Income | 13,595,301 | 63,240,338 | 44,925,839 | 255,405,786 |
| 2 | Interest Expense | 26,548,016 | 26,513,899 | 74,859,369 | 217,855,995 |
| 3 | Net Interest Income ( 1 minus 2) | **(12,952,715)** | **36,726,439** | **(29,933,530)** | **37,549,791** |
| 4 | Bad Debts Written -Off | - | - | - | - |
| 5 | Impairment Losses on :Loans and Advances | (15,373,500) | 271,440,111 | (7,524,550) | 320,529,298 |
| **6** | **Non Interest Income:** | **46,195,038** | **14,431,117** | **96,967,533** | **62,957,047** |
| | 6.1 Foreign Currency Dealings and Translation Gains/ (Loss) | - | - | - | - |
| | 6.2 Fees and Commissions | 11,527,220 | 11,440,060 | 33,187,319 | 48,742,398 |
| | 6.3 Dividend Income | - | - | - | - |
| | 6.4 Other Operating Income | 34,667,818 | 2,991,057 | 63,780,214 | 14,214,649 |
| **7** | **Non Interest Expenses:** | **280,973,797** | **357,551,354** | **739,767,743** | **1,060,409,460** |
| | 7.1 Salaries and Benefits | 105,111,596 | 142,415,706 | 374,288,715 | 453,414,511 |
| | 7.2 Fees and Commission | 44,228,163 | 6,548,000 | 48,359,763 | 45,614,801 |
| | 7.3 Other Operating Expenses | 131,634,038 | 208,587,648 | 317,119,265 | 561,380,148 |
| **8** | **Operating Income/ (Loss)** | **(232,357,973)** | **(577,833,909)** | **(665,209,190)** | **(1,280,431,920)** |
| **9** | **Income Tax Provision** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **10** | **Net Income / (Loss) After Income Tax** | **(232,357,973)** | **(577,833,909)** | **(665,209,190)** | **(1,280,431,920)** |
| **11** | **Other Comprehensive Income (itemize)** | | | | |
| **12** | **Total Comprehensive Income/(loss) for the year** | **(232,357,973)** | **(577,833,909)** | **(665,209,190)** | **(1,280,431,920)** |
| 13 | Number of Employees | 22 | 32 | 22 | 32 |
| 14 | Basic Earnings Per Share | -182.11 | -418.86 | -521.37 | -928.16 |
| **15** | **Number of Branches** | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **SELECTED PERFORMANCE INDICATORS** | | | | |
| (i) | Return on Average Total Assets | -24.48% | -24.12% | -210.28% | -160.31% |
| (ii) | Return on Average Shareholders' Fund | -10.93% | -25.13% | -93.85% | -509.69% |
| (iii) | Non Interest Expense to Gross Income | 469.93% | 460.34% | 521.35% | 333.08% |
| (iv) | Net Interest Income to Average Earning Assets | -102.99% | -36.97% | -294.852% | -81.92% |

Average figures shall be computed by summing up the end balances for respective months in the period divided by number of months in the period.

### CONDENSED STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY AS AT 30/09/2019

| Current Year | Share Capital | Share Premium | Retained Earnings | Regulatory Reserve | General Provinsion Reserve | Others | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Balance as at the beginning of the year** | 7,363,802,064 | 0 | -6,497,512,011 | 9,096,425 | 806,449 | 453,542,328 | 1,329,735,255 |
| Profit for the year | | | (665,209,190) | | | | -665,209,190 |
| Other Comprehensive Income | | | | | | | - |
| Transactions with owners | (984,338,000) | | | | | | (984,338,000) |
| Dividends Paid | | | | | | | - |
| Regulatory Reserve | | | | 12,421,181 | | | 12,421,181 |
| General Provision Reserve | | | | | (456,335) | | (456,335) |
| Others | | | (3,064,573,895) | | | | (3,064,573,895) |
| **Balance as at the end of the current period** | **6,379,464,064** | **-** | **(10,227,295,096)** | **21,517,606** | **350,114** | **453,542,328** | **(3,372,420,984)** |
| **Previous Year** | | | | | | | |
| **Balance as at the beginning of the year** | **1,512,496,093** | **-** | **(3,888,172,293)** | **93,021,759** | **27,594,788** | **487,455,289** | **(1,767,604,364)** |
| Profit for the year | - | - | (2,623,756,656) | - | - | - | (2,623,756,656) |
| Other Comprehensive Income | - | - | - | - | - | - | - |
| Transactions with owners | 5,851,305,971 | - | - | - | - | - | 5,851,305,971 |
| Dividends Paid | - | - | - | - | - | - | - |
| Regulatory Reserve | - | - | - | (83,925,334) | - | - | (83,925,334) |
| General Provision Reserve | - | - | - | - | (26,788,339) | - | (26,788,339) |
| Others | - | - | 14,416,937 | - | - | (33,912,961) | (19,496,024) |
| **Balance as at the end of the previous period** | **7,363,802,064** | **-** | **(6,497,512,011)** | **9,096,425** | **806,449** | **453,542,328** | **1,329,735,255** |

Distributed via ippmedia

### CONDENSED STATEMENT OF CASH FLOW STATEMENT FOR THE QUARTER ENDED 30/09/2019 (Amounts in shillings)

| | | Current Quarter Date:30.09.2019 | Previous Quarter Date:30.06.2019 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Cash flow from operating activities:** | | |
| | Net income/ (Loss) | (232,357,973) | (174,532,362) |
| | **Adjustments for:** | - | - |
| | - Impairment/Amortization | - | - |
| | - Depreciation | 15,872,232 | 15,872,232 |
| | - Net change in Loans and Advances | 41,987,202 | 19,968,628 |
| | - (Gain)/loss on Sale of Assets | - | - |
| | - Net change in Deposits | 30,602,458 | 369,413,579 |
| | - Net change in Short Term Negotiable Securities | - | - |
| | - Net change in Other Liabilities | 205,962,101 | 49,601,085 |
| | - Net change in Other Assets | (96,873,293) | 1,971,269,670 |
| | - Tax Paid | - | - |
| | - Others ( specify) | 17,155,338 | (3,450,497,326) |
| | - Minority interest | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by operating activities*** | **(17,651,935)** | **(1,198,904,494)** |
| **II:** | **Cash flow from investing activities:** | | |
| | Dividend Received | - | - |
| | Purcharse of Fixed Assets | - | - |
| | Proceeds from Sale of Fixed Assets | - | - |
| | Purchase of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Proceeds from Sale of Non-Dealing Securities | - | - |
| | Others (specify) | - | - |
| | ***Net cash provided (used) by investing activities*** | - | - |
| **III:** | **Cash flow from financing activities:** | | |
| | Repayment of Long-term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Long Term Debt | - | - |
| | Proceeds from Issuance of Share Capital | (1,200,000,000) | 2,200,000 |
| | Payment of Cash Dividends | - | - |
| | Net Change in Other Borrowings | - | - |
| | Others | | - |
| | ***Net Cash Provided (used) by Financing Acities*** | **(1,200,000,000)** | **2,200,000** |
| **IV:** | **Cash and Cash Equivalents:** | | |
| | **Net Increase/ (Decrease) in Cash and Cash Equivalents** | **(1,217,651,935)** | **(1,196,704,494)** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the Beginning of the Quarter/Year** | **2,474,447,993** | **3,671,152,487** |
| | **Cash and Cash Equivalents at the end of the Quarter/Year** | **1,256,796,058** | **2,474,447,993** |

| Name and Title | Signature | Date |
|---|---|---|
| Janeth. J. Minja<br>**Ag. GENERAL MANAGER** | ........................ | 31ST October 2019 |
| Anna. H. Teete<br>**SENIOR ACCOUNTANT** | ........................ | 31ST October 2019 |
| Denis. A. Ruhangisa<br>**INTERNAL AUDITOR** | ........................ | 31ST October 2019 |

We, the under-named, non-executive members of the board of directors, attest to the correctness of the above statements. We declare that the statements have been examined by us, and to the best of our knowledge and belief have been prepared in conformance with the instructions and are true and correct.

| Name | Signature | Date |
|---|---|---|
| **1. Dr G Machimu, CHAIRMAN, BOARD OF DIRECTORS** | ........................ | 31ST October 2019 |
| **2. Ms A.A. Mshana ,VICE CHAIR PERSON BOARD OF DIRECTORS** | ........................ | 31ST October 2019 |

## MINIMUM DISLOSURES OF CHARGES AND FEES

| NUMBER | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1.0 | Current Accounts | |
| | (a) Required minimum opening balance | 100,000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type): | |
| | Individuals | 8,000 |
| | Co-operatives | 6,500 |
| | Companies | 8,000 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | 1,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | 1,000 |
| | (e) ATM min statement | 500 |
| | (f) Interim statement per page | 1,500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 1,000 |
| | (h) Cheque book | 20,000 |
| | (i) Dishonoured cheque | 40,000 |
| | (j) Special clearance | N/A |
| | (k) Counter cheque | 700 |
| | (l) Stop payment | 30,000 |
| | (m) Standing order | N/A |
| | (n) Balance enquiry | N/A |
| | (o) New ATM card issuance | 10,000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | 10,000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | N/A |
| | (r) Unarranged overdraft | N/A |
| | (s) Interbank transfer | 13,000 |
| | (t) Bill payments through ATM | 1,000 |
| | (u) Deposit fee i.e for school fees | 1,000 |
| | (v) Withdrawal without cheque leaf | 5,000 |
| | (w) Withdrawal charges above 6 million | 0.15% |
| 2.0 | Savings Accounts (Disclosure for product specific types) | |
| | (a) Required minimum opening balance | 30,000 |
| | (b) Monthly service fee | 1,000 |
| | (c) Interim statement | 1,500 |
| | (d) Account closure | 10,000 |
| | (e) School fees deposite charges | 1,000 |
| | (f) ATM withdrawal fee | 1,000 |
| | (g) Withdrawal charges over the counter | 600 |
| | (h) Replacement of ID Card | 5,000 |
| | (i) Withdrawal above 3 million without notice | 0.25% |
| | (j) Stop payment charges | 30,000 |
| | (k) Salary processing fee | 3,000 |
| | (l) Pension processing fee | 2,000 |
| | (m) Searching past records fee | 10,000 |
| | (n) Dormant Account Activation | 10,000 |
| | (o) Certificate of Balance | 3,000 |
| 3.0 | Electronic Banking | |
| | (a) Internet banking monthly fee | N/A |
| | (b) Internet transfer | N/A |
| | (c) SMS banking | N/A |
| | (d) Other TT/SWIFT | 13,000 |
| | (e) Transfer from bank account to mobile | 1,000 |
| 4.0 | Foreign Exchange Transaction | N/A |
| | (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | N/A |
| | (b) Purchase of foreign cheque | N/A |
| | (c) Sale/purchases of cash passport | N/A |
| | (d) Telegraphic transfer | N/A |
| | (e) Telex/SWIFT | N/A |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | N/A |
| 5.0 | Personal Loans | |
| | (a) Processing /Arrangement/Appraisal fee | 1.5-4% |
| | (i) Personal loans | 24% |
| | (ii) Overdrafts | 18-24% |
| | (iii) Mortgage finance | N/A |
| | (iv) Asset finance | N/A |
| | (b) Unpaid loan instalment i.e. above the existing rate | 5% |
| | (c) Early repayment | N/A |
| | (d) Valuation fees | N/A |
| | (e) Discharge of Security Document to other banks | 120,000 |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Janeth. J. Minja | Ag. General Manager | | 31ST October 2019 |
| 2 | Anna .H. Teete | Senior Accountant | | 31ST October 2019 |
| 3 | Denis. A. Ruhangisa | Internal Auditor | | 31ST October 2019 |

215491102

TANGAZO


Kitochi Smart 4G
Simu ya 4G kwa Wote!
4G
Shs. 49,000/-
Furahia Facebook BURE! kwa miezi 3
T-Smart
Pre-Order SASA Kitochi 4G Smart upate Facebook ya BURE bila kikomo.
Piga: 100 au Tembelea Duka la Tigo
4G+
tigo
Weka Oda kuanzia Oktoba 30, 2019 hadi Novemba 15, 2019 simu ni chache.
Kwa Masharti na Vigezo tembelea: www.tigo.co.tz
215491402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tufanye utafiti zaidi kukielewa kiharusi

**TAARIFA** kuwa idadi ya watu wanaofariki dunia kutokana na kiharusi nchini ni kubwa ni habari ambazo licha ya kusikitisha zinaogopesha pia.

Zinaogopesha kwa kuwa zinawagusa Watanzania wote baada ya wataalamu kueleza kuwa matatizo ya kiharusi yanawaathiri watu wa rika zote na si wazee kama ilivyokuwa imezoeleka hapo awali Licha ya kuhofisha na kusikitika ni vyema pia kuanza uwajibikaji zaidi katika kuwahamasisha wananchi kuanzia watoto shuleni, vyuoni na umma kwenye jamii zetu ili waamke na kuchukua hatia dhidi ya maradhi haya.

Tatizo tulilonalo Watanzania ni kuamini kuwa kiharusi ni tatizo la kurogwa , licha ya kwamba wasomi wanatueleza kuwa ni ukosefu wa hewa safi na chakula ubongoni kwa sekunde chache.

Chakula na hewa hiyo hufikishwa na damu licha ya kwamba kitaalamu damu haiugusi ubongo, moja kwa moja, lakini kuna utaratibu wa kufikisha virutubisho hivyo.

Kwa maana nyingine ni kwamba mfumo unaopeleka chakula na hewa na virutubisho unapochelewa kuhudumia ubongo tatizo hutokea. Wataalamu wa masuala ya mishipa ya fahamu wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, wanaeleza wakati wa Siku ya Kiharusi Duniani (Oktoba 29), kuwa ni ugonjwa wa pili kwa kuua watu duniani.

Aidha, wanautaja kuwa ni chanzo cha ulemavu kwa Watanzania wengi ambao mara nyingi wanafika Muhimbili wakiwa wamechelewa. Inawezekana wanachelewa kwa vile wengi hukimbilia kwa waganga wakiamini kuwa wamerogwa.

Taarifa hizi za madaktari bingwa zinaturudisha kule kule kwenye utamaduni wa Watanzania wa kuchelewa kuripoti hospitalini tatizo lolote kuanzia degedege na hata kina mama kujifungua.

Ni kawaida kwa watu wengi kupuuza kwenda hospitalini kutokana na kuamini zaidi ushirikina na kukimbilia kwenye tunguri na kupigwa chale.

Wapo watu wanaoamini kuwa ugonjwa wa kiharusi ni wa kulogwa na huitwa 'kipapai' na kwa msingi huo hukimbilia kwa waganga ambako nako hawaponi, wakizidiwa ndipo hukimbilia hospitalini. Hali inatisha kwa vile wataalamu wanaeleza kuwa wastani wa wagonjwa watatu hadi watano hupokelewa kila siku hospitalini hapo ambao licha ya kufika wengi wanachelewa na kama wangewahi wangepona kwani ukifika hospitalini saa sita baada ya kuugua ugonjwa unatibika.

Taarifa za kitisho cha ugonjwa huo ni vyema zianze kufanyiwa kazi kwa kutumia utafiti na uchunguzi zaidi ili watu wafahamu chanzo cha maradhi hayo kwa ufasaha.

Tungependa kupata maelezo na taarifa zaidi kwanini ugonjwa huo umezidi zama hizi na ni vipi vichocheo vyake? Je kuna uhusiano na matatizo mengine kama ya moyo, shinikizo la damu, uvimbe kwenye ubongo na magonjwa yakiwamo kisukari. Na zipi ni njia za kujikinga?

Watu wanaweza kujichunguza kwa namna gani kufahamu kuwa wana tatizo hilo? Kwa watu wa kawaida wanaoishi vijijini wanaweza kuchukua tahadhari zipi kujiepusha na tatizo hilo?

Tunapenda kupata taarifa zaidi kwa vile kuna maelezo ya jumla yanayotolewa na wataalamu kuwa matatizo ya moyo na kiharusi ni matokeo ya mitindo ya maisha watu wanayoishi.

Maelezo yao ni kwamba watu wengi hawafanyi mazoezi, hutumia kwa wingi vyakula vyenye mafuta na sukari nyingi mno, ni wanene kupindukia na pia hawachunguzi afya zao.

Wakati mwingine tunaona kuwa maelezo hayo si ya kuridhisha kwa vile kuna watu wembamba, wanaofanyakazi sana wanaoishi vijijini ambao hawana miili mikubwa waliopoteza maisha kutona na kiharusi.

Ndiyo maana tunasisitiza kuwa ukifanyika utafiti zaidi na kuzifahamu njia za kukabiliana na tatizo hilo utakuwa mwanzo wa kupata ufumbuzi na kuepusha madhara ya kiharusi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mzizi wa mimba kwa wanafunzi uko huku

Na Sabato Kasika

Distributed via ippmedia

**LICHA** ya serikali kuweka adhabu kali kwa wanaowasababishia ujauzito kwa wanafunzi na watoto chini ya umri wa miaka 18, bado tatizo la mimba za utotoni limeendelea kuwapo na kukatisha ndoto zao.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa - Tamisemi), Mwita Waitara, anataja chanzo ni mila na desturi, kwa vile zipo ambazo mabinti wanapofikia umri fulani, wanapewa chumba chao.

Kwa mujibu wa Waitara kupitia kauli yake jijini Dodoma kwenye maadhimisho ya Siku ya Idadi ya Watu Duniani, tatizo hilo ni kubwa kwa shule zote; msingi na sekondari.

Waitara anasema, asilimia 29 ya tatizo hilo linachangiwa kwa kiasi kikubwa na mila na desturi na kuleta walakini hata katika utekelezaji wa mashtaka na uendweshaji wa kesi zinazohusu ngono na mimba kwa wanafunzi.

"Uendeshaji kesi hizi mpaka kumtia mtu hatiani bado ni changamoto, kwa kuwa wanaofanya vitendo hivyo, wengine ni watu wa karibu na familia na wengine wanarubuni ndugu na kumalizana kimya kimya," anasema Waitara.

Anafafanua kwamba, uelewa wa watoto bado ni mdogo, huku mimba nyingi zinazoripotiwa zikiishia hewani bila ya kujua mwisho wa kesi.

Naibu Waziri anasema, serikali kila mara imekuwa ikifanya vikao na wazazi kuondokana na tatizo hilo, lakini bado mwitikio ni mdogo katika kudhibiti vitendo hivyo.

Mbali na hayo, anasema bado kuna changamoto ya vifo vitokanavyo na uzazi na kwamba kati ya vizazi hai 100,000 vya watu waliopo, 556 wanaripotiwa kufariki dunia kwa sababu mbalimbali, ikiwamo mimba za utotoni.

Mjadala huo naamini una haja ya kuchukuliwa hatua za makusudi, ili kumaliza tatizo. Hiyo ni pamoja na kuwaelimisha wazazi, ambao ni wazito kuelewa umuhimu wa elimu.

Inasikitisha kuona serikali inawashirikisha wazazi katika kumaliza tatizo hilo, halafu baadhi yao wanakuwa wazito kutoa ushirikiano. Inawezekana na hao ndiyo wanaoendekeza mila na desturi zisizo sahihi.

Ni vyema juhudi mbalimbali zinazochukuliwa na serikali kwa lengo la kuhakikisha mtoto wa kike anakamilisha elimu yake bila ya kikwazo ziheshimiwe na watu wote.

Hebu fikiria, eti kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu, wanafunzi 142 wameshakatisha masomo kwa sababu ya mimba, mkoani Lindi.

Taarifa iliyowasilishwa katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na Ofisa Elimu (Taaluma), Hatibu Tuki, inaonyesha idadi hiyo walipata ujauzito kuanzia mwezi Januari hadi tarehe 30 iliyopita.

Hivi hali kama hii ikiwa kwenye mikoa yote nchini kutakuwa na wanafunzi wangapi wenye mimba? Ni vyema wazazi na walezi wabadilike na kushiriki kikamilifu katika vita ya kuzuia mimba hizo.

Tabia hii chafu ya kuwapa mimba wanafunzi haijawaacha nyuma baadhi ya walimu wa shule za msingi na sekondari, kwani nao wamekuwa wakitajwa katika vitendo hivyo, ambavyo ni kinyume na maadili.

Katika kukabiliana na tatizo hilo la mimba, mwaka 2016 serikali ilifanyia marekebisho Sheria ya Elimu ya mwaka 1978, ikisimama katika marufuku ya mapenzi na mwanafunzi.


Sheria ya Makosa ya Kujamiiana inaenda mbali, kwa kutangaza adhabu nzito inayoangukia miaka 30 hadi kifungo maisha.

Kwa bahati mbaya, pamoja na kuwapo sheria hizo, bado tatizo la mimba limeendelea kusikika na kuthibitishwa katika maeneo mbalimbali nchini, hali ambayo ni hatari kwa maendeleo ya elimu ya mtoto wa kike.

Mjadala huu unaamini kwamba, ushirikiano wa wazazi na walezi na serikali katika kutatua tatizo hili na muhimu kusaidia kuwabana wanafunzi na 'mafataki' wanaosababisha kuendelea kuwapo mimba hizo.

Wasichana wana haki ya kupata elimu, hivyo wanatakiwa kulindwa, ili kukomesha mtindo huo wa baadhi ya watu wasio na 'mshipa wa aibu' kwa kuendekeza ngono. Kukomesha uwapo kwa mimba kwa wanafunzi inawezekana, iwapo kila mmoja atatimiza wajibu wake ikiwamo malezi bora na pia kutoa ushirikiano na vyombo vya dola ili kuwanasa 'mafataki' hawa.

TANGAZO



absa
Huduma za
kimataifa
kukuunganisha na dunia
Kufanya kazi katika nchi 12 barani Afrika na ulimwenguni kunatufanya kuwa benki ya Kiafrika inayoongoza.
Tembelea absa.africa
Absa Group, serving Tanzania as Barclays.
BARCLAYS
Absa Group Limited yenye usajili No 1986/003934/06. Absa Group Limited inatumia chapa ya Barclays chini ya leseni ya Barclays Bank Plc.

# Bandari yajenga gati 4 Mtwara kuhudumia shehena gesi

**Na Mary Geofrey, MTWARA**

SERIKALI inaendelea kupanua Bandari ya Mtwara kwa kujenga gati nne za kisasa kwa ajili ya kuhudumia shehena ya gesi, mafuta na mazao ya kilimo katika Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara unaojumuisha mikoa ya Kusini na nchi jirani za Malawi, Zambia na Msumbiji.

Mradi huo ukikamilika utaiwezesha Bandari ya Mtwara kuhudumia shehena zaidi ya tani milioni moja kwa mwaka.

Meneja wa Bandari ya Mtwara, Mhandisi Juma Kijavara, aliyasema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani humo jana kuhusu utekelezaji wa mradi huo.

Alisema awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi huo ni ujenzi wa gati urefu wa mita 300 lenye uwezo wa kuhudumia shehena mchanganyiko unaogharimu Sh. bilioni 137.

Alisema Mamlaka ya Bandari (TPA), iliingia mkataba na mkandarasi ambaye ni muunganiko wa Kampuni za China Railway Construction Engineering Group na China Railway Major Bridge Engineering Group ulioanza Machi 4, 2017 na kutarajia kukamilika Machi 2020.

"Hadi sasa kazi ya usanifu imekamilika na ujenzi unaendelea na kufikia asilimia 55," alisema Kijavara.

Naye Kaimu Mhandisi wa Bandari hiyo, Norbart Kalembwe, alisema pia wanaendelea na mradi wa ujenzi wa mita ya kupima mafuta unaotekelezwa chini ya Ofisi ya Rais.

Alisema mradi huo unafanywa na Mkandarasi Endress+Hauser kutoka Uswiss akishirikiana na Kampuni ya Kizalendo ya BQ Constractor kwa ujenzi wa mita za kupima mafuta Mtwara, Dar es Salaam na Tanga kwa thamani ya Euro milioni 17.

Pia kwa Mtwara mradi utahusisha ujenzi wa mitambo miwili pamoja chumba cha usimamizi kwa ajili ya kupima mafuta ya dizeli na petroli. Alisema mradi huo ulianza Machi, mwaka huu na utatekelezwa kwa miezi 15 unaotarajiwa kukamilika Mei, mwakani.

"Mradi ukikamilika utakuwa umeiwezesha bandari kutekeleza maelekezo ya serikali na itakuwa na uwezo wa kupima mafuta halisi yanayopita katika bandari hii," alisema Kalembwe.

Kadhalika, alisema wanatekeleza mradi wa ujenzi wa sehemu ya kuhifadhia makasha matupu pamoja na sehemu ya kupanga mzigo kwa msimu wa korosho na ukarabati wa ghala namba tatu.

# RC abaini mazito shule kongwe ya wasichana

INATOKA UK. 2

kitaaluma katika ngazi ya mkoa katika mitihani ya kidato cha sita mwaka huu.

"Haiwezekani shule ilipiwe kila kitu na serikali, ipatiwe fedha nyingi za ukarabati halafu bado ifanye vibaya. Ofisa Elimu Sekondari, hii ni aibu kubwa sana.

"Wanafunzi wamekuwa wakitoroka mara kwa mara na ushahidi ni tukio la usiku wa kuamkia leo (juzi), wanafunzi wawili wamenaswa saa nane na saa tisa usiku wakirejea, na watuhumiwa wakubwa ni walimu," Ole Sanare alisema.

Mkuu wa Mkoa alisema serikali haitafumbia macho kuona walimu wanaotegemewa kama walezi na wazazi wa wanafunzi, kugeuka kuwa wachumba wa watoto hao.

"Ni lazima bodi ya shule kama ipo, ingawa nasikia toka 2017 haipo, ichukue hatua kumaliza matatizo yanayoikabili shule hii.

"Wafukuze kabisa wanafunzi na walimu wanaofanya upuuzi huu, OCD, RPC mkamate hawa walimu watakaobainika kuwatorosha wanafunzi na kwenda kujihusisha nao kimapenzi.

"Haya ni mambo ya ovyo, hatuwezi kuyaachia, wasihamishwe, nasema malizana nao hapahapa, wafukuzwe na walimu wakamatwe wafikishwe kwenye vyombo vya dola wakaozee magereza," aliagiza.

Pia alisema amebaini wanafunzi wa shule hiyo wamekuwa wakipewa chakula chini ya kiwango kinachopendekezwa na Wizara ya Elimu, hivyo hawashibi huku walimu wakila chakula kinachopelekwa shuleni kwa ajili ya wanafunzi kinyume cha taratibu.

Alisema kitendo hicho kimekuwa kikichukiza wanafunzi na mara kwa mara wamekuwa wakitishia kufanya uharibifu wa shule.

"Unakuta wanafunzi 555 waliopo wanapaswa kula gramu 250 (kila mmoja) sawa na kilo 138 za mchele, lakini wanapewa pungufu, wanapaswa kula sembe gramu 250 sawa na kilo 138, lakini wanapata kilo 75 kwa siku, mafuta lita 18, lakini wanapewa lita nane, 10 hazijulikani zinapokwenda, nyama, sukari, chumvi, majani ya chai na vyakula vingine wanapewa kwa uchache, hivyo vingine vinakwenda wapi?

"Mkuu wa Shule (Setina Ngailo), nasema wanafunzi wakifanya uharibifu kutokana na hizi changamoto zilizopo, utawajibika kwa asilimia 100," Ole Sanare alionya.

Mkuu wa Mkoa pia alieleza kushangazwa na kitendo cha shule hiyo kwa muda mrefu kukosa bodi ya shule, akieleza kuwa kinasababisha walimu au wanafunzi wakiwa na matatizo kukosa mahali pa kupeleka malalamiko yao.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Ifakara kumchukulia hatua Ofisa Elimu Sekondari aliyemdanganya katika mkutano huo kuwa shule ina bodi ilhali mchakato wa kupendekeza majina ya wajumbe wa bodi hiyo ndiyo kwanza umeanza.

Pia, alionya kitendo cha Boharia wa shule hiyo, Dora Chambila, kudaiwa kutafuta tenda mwenyewe, kutoa oda ya ununuzi wa vyakula peke yake, kupokea vyakula na kuhifadhi mwenyewe stoo na kugawa vya kupikwa.

Boharia huyo alijitetea kwa kueleza kuwa amekuwa akifanya kazi kwa kushirikisha timu inayoundwa na watu mbalimbali akiwamo Makamu Mkuu wa Shule, Mhasibu na Mpishi Mkuu.

Mkuu wa Mkoa aliunda kamati maalum inayoshirikisha Ofisa wa Takukuru wa Wilaya, wajumbe wawili kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mdogo wa Ifakara na wawili kutoka ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa na kuipa siku tatu kufanya uchunguzi wa kina wa madai na tuhuma zinazolalamikiwa ili kumpa ripoti kamili. Alisema kamati hiyo pia itatakiwa kufuatilia matumizi ya Sh. bilioni 1.3 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya ukarabati wa shule hiyo.

Mkuu wa Shule hiyo, Sentana Ngailo, alikiri kuwapo kwa vitendo vya utovu wa nidhamu, lakini akasisitiza kuwa bado ni mgeni kwa kuwa ana mwezi mmoja tangu aripoti kuiongoza.

"Tayari tumekamata simu nne kutoka kwa wanafunzi na katika upekuzi tulikuta mawasiliano yakiendelea baina ya wanafunzi na majirani wa nje, lakini tumeshaweka mikakati kabambe kupata ushirikiano na kulikomesha, hata la chakula kidogo nalo nililikuta lakini nimeshalirekebisha," alisema.

Distributed via ippmedia






## Hoja 9 barua ya Chadema kwa Jafo

INATOKA UK. 3

wamepewa fomu pungufu ambazo nyingi zimeonekana kutoambatishwa fomu za maadili.

Makene alidai chama chao kinaona huo ni mkakati wa makusudi ili baadaye kutumika kama kigezo cha kuwaengua wagombea wao watakapokatiwa rufani kwa kutojaza fomu hizo.

Alitaja hoja ya nne katika barua yao hiyo kuwa ni wagombea wao kunyimwa fomu za kugombea kutokana na kile alichodai hawakutoa mchango wa mbio za Mwenge wa Uhuru.

Alisema wanamtaka waziri huyo achukue hatua kutokana na wagombea wao kunyimwa fomu katika baadhi ya maeneo kwa hoja kuwa wamejiandikisha mara mbili na hata walipotoa ripoti ya kughushiwa kwa majina yao, Jeshi la Polisi limedaiwa kutokuchukua hatua.

Makene alisema hoja yao ya sita ni wagombea wao kutokupatiwa fomu kwa kile walichodai kuwa wasimamizi waliwaambia kuna wagombea wa chama hicho ambao tayari wamepatiwa fomu ilhali wanaodaiwa kupewa fomu hawatambuliwi na chama.

Alidai baadhi ya wagombea wa chama hicho wamekamatwa na polisi, mgambo na viongozi wa serikali za mitaa na fomu zao kushikiliwa kinyume cha kanuni za uchaguzi huo.

Alidai tatizo hilo limetokea katika Kitongoji cha Nyanghali, Kijiji cha Mwamagembe, Kata ya Mwataga wilayani Kishapu.

"Lipo tatizo la wasimamizi au wasimamizi wa uchaguzi katika maeneo yao kuwaambia wagombea wa Chadema kuwa katika maeneo yao wapo wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) pekee kinyume cha kanuni," alidai katika taarifa yake hiyo.

Hoja ya tisa ya chama hicho ni wasimamizi wasaidizi kukataa kutoa nakala ya fomu ya kuomba kugombea baada ya mgombea kurejesha fomu ya kuomba kuteuliwa.

Uchukuaji fomu za kugombea katika uchaguzi huo ulianza rasmi juzi na utakamilika Novemba 4, mwaka huu.

HABARI KITAIFA

# Maambukizi ya VVU bado ni tatizo SADC

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amesema maambukizi ya Virusi (VVU) na Ukimwi kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) bado ni changamoto, lakini kwa Tanzania yamepungua kutoka asilimia saba mwaka 2003 hadi asilimia 4.7 mwaka huu.

Amesema mawaziri wa SADC wanaoshughulikia afya na Ukimwi wanatarajia kukutana jijini Dar es Salaam kwa siku nne wakijadiliana namna ya kupambana na kupunguza maambukizi ya VVU, kifua kikuu, malaria, lishe, ebola pamoja na kuimarisha mifumo ya afya na usambazaji dawa katika nchi zao.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akifungua mkutano wa waandishi wa habari kuhusu mkutano wa Mawaziri wa SADC wanaoshughulikia afya na Ukimwi unaotarajiwa kuanza Jumatatu hadi Ijumaa. Alisema Makatibu Wakuu wa SADC watakutana na kujadili mpango mkakati wa kikanda wa kupambana na magonjwa hayo, hatua za kuchukua katika utekelezaji wa pamoja, na mgeni rasmi atakuwa Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Waziri alisema nchi 30 duniani zimeanzisha mapambano dhidi ya maambukizi ya TB kati ya hizo tano zinatoka SADC, na kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizowaibua wagonjwa wa TB.

Kuhusu malaria, Waziri Mwalimu alisema bado ni tatizo katika nchi za SADC, ingawa Tanzania imefanikiwa kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo kutoka asilimia 14 mwaka 2015 hadi asilimia tano mwaka 2017. "Hivyo Makatibu Wakuu pia watajadiliana namna ya kupunguza viwango vya utapiamlo na viriba tumbo kwa watoto, kuongeza lishe, kwa nchi za SADC... Shelisheli peke yao wamefanikiwa kupunguza na wamefikia asilimia nane, Tanzania kiwango cha udumavu kimefikia asilimia 31.8," alisema Mwalimu.

Alisema Makatibu Wakuu pia watajadiliana kuhusu namna ya kuimarisha mifumo ya afya na usambazaji wa vifaa tiba na dawa, pamoja na ugonjwa wa ebola kwa kuja na mkakati wa kuimarisha ulinzi mipakani. "Baada ya makatibu wakuu kukutana na kujadiliana watatuletea taarifa mawaziri wa afya kwa ajili ya utekelezaji, pia tutawapeleka mawaziri wa SADC kwenye kiwanda chetu cha kutengeneza dawa ya kuulia malaria kilichopo mkoani Kibaha," alisema.

Alisema kuwa lengo kuu la serikali ni kuzishawishi nchi za SADC kununua dawa kutoka katika kiwanda hicho, ambacho kina uwezo wa kuzalisha lita milioni sita kwa mwaka. Alisema dawa hiyo ina uwezo wa kuua viruirui kwa asilimia 95 hadi 100.



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, mkoani Simiyu, Robert Rweyo (katikati), Mkurugenzi wa halmashuari hiyo, Merkzedeck Humbe (kushoto) na Mathias Nguzu (kulia) mwakilishi wa Kampuni mbili za ujenzi, Mumangi Trans and Construction Ltd na Pek Brothers (T) Ltd, wakisaini mkataba wa ukamilishaji ujenzi wa stendi ya kisasa ya halmashuari hiyo, juzi. **PICHA: HAPPY SEVERINE**

## Bil. 4.2/- kuzipa maji kata tatu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATA tatu za Halmashauri ya Shinyanga Vijijini mkoani Shinyanga, zinatarajia kunufaika na miradi ya majisafi na salama yenye thamani ya Sh. bilioni 4.2.

Wananchi hao watapata majisafi na salama kutoka kwa mradi wa maji unaotekelezwa na Shirika lisilo la kiserikali la Lifewater International la Marekani.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo, Mkurugenzi wa Shirika hilo nchini, Devocatus Kamara, alisema mradi huo unakwenda kutatua changamoto ya kudumu ya upatikanaji wa maji kwa wananchi hao ambao wanatumia maji yasiyo salama.

Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka miwili kuanzia 2020 hadi 2024, kwa kujenga visima virefu, na kata zitakazonufaika ni Mwamala, Mwantini na Mwalukwa.

"Tulifanya utafiti awali na kubaini kata hizi tatu zinakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa majisafi na salama, ndipo tukaamua kuuleta mradi huu ili kuwaondolea adha ya kutumia maji yasiyofaa," alisema Kamara.

Kwa mujibu wa Kamara, shughuli zitakazofanyika ni kuchimba visima virefu vya maji kwenye makazi ya watu, shuleni na zahanati, na kuwafikia watu zaidi 100,000.

Meneja wa Shirika hilo, mkoani Shinyanga, Benety Malima, alisema pia kwenye vijiji ambavyo vimeshapitiwa na bomba la mradi wa maji Ziwa Victoria, watafanya utaratibu wa kuyavuta maji hayo na kusambaza kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alishukuru shirika hilo kwa utatuzi wa kero ya muda

# Bil. 2.5/- za Ireland kusaidia wanawake, watoto kiafya

**Na Sabato Kasika**

IRELAND imetoa Euro milioni moja (sawa na Sh. bilioni 2.5) ili kusaidia mradi wa kuboresha afya ya wanawake na watoto uitwao 'Ujana wangu nguvu yangu', utakaotekelezwa katika wilaya nne za mkoa wa Kigoma. Mradi huo wa mwaka mmoja, unasimamiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu na Maendeleo (UNFPA), na utatekelezwa katika Wilaya za Kasulu Mjini, Kasulu Vijijini, Kakonko na Kibondo.

Hafla ya kusaini makubaliano ya kutoa kiasi hicho cha Euro ilifanyika juzi jijini Dar es Salaam katika ofisi za ubalozi wa Ireland nchini, huku Balozi Paul Sherlock akisema afya ya uzazi ni muhimu kwa ajili ya maendeleo endelevu.

"Tunaipongeza serikali ya Tanzania kwa hatua yake ya kuboresha afya ya wanawake na watoto. Afya ya mama, mtoto, na vijana balehe imepewa kipaumbele katika sera za afya Tanzania," alisema Sherlock.

Alisema, Ireland imekuwa na uhusiano wa muda mrefu na Tanzania kwa miaka 40 iliyopita na kwamba wanafanya kazi kuisaidia Tanzania kuboresha upatikanaji na ubora wa huduma ya afya.

"Kupitia mradi huu wa UNFPA, unaofadhiliwa na ubalozi, tumeweza kujenga, kuboresha na kununua vifaa tiba katika vituo vya afya kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za afya ya uzazi," alisema. Alisema usawa wa kijinsia na uwezeshwaji wanawake ni muhimu ili mwanamke apate huduma za afya na pia upanuzi wa huduma za afya ya uzazi lazima uendane na kumwezesha mwanamke, ikiwamo kuzuia ukatili wa kijinsia.

"Ushirikiano kati ya UNFPA na Ireland ni sehemu tu ya mchango wa Ireland mkoani Kigoma na kupitia mchango wa Ireland, UNICEF wanatekeleza mpango wa huduma ya afya ngazi ya jamii na kutoa huduma kwa kaya maskini," alisema.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA nchini, Jacqueline Mahon, alisema mradi huo unalenga kuhakikisha vijana hasa wasichana kupata huduma ya afya ya uzazi, na kwamba shirika hilo linashirikiana na serikali kuufanikisha.

"Tunashirikiana na Wizara ya Afya, Tamisemi na halmashauri za maeneo husika, na tumechagua mkoa wa Kigoma kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo hali halisi ya mimba za utotoni," alisema Mahon.

Alisema, Kigoma ni mkoa wenye idadi kubwa ya vifo vya kinamama wakati wa kujifungua, mimba za utotoni ni nyingi na pia kihistoria ni mkoa ambao unapokea wakimbizi wengi na sasa wapo zaidi ya 300,000.

# DC akifunga Chuo cha Afya

Na Neema Sawaka, KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Anamlingi Macha, amekifunga Chuo cha Afya cha ST. Marcus kilichopo Kata ya Isagehe katika Halmashauri ya Mji wa Kahama kwa kuendeshwa bila kufuata taratibu za elimu ikiwamo kusajiliwa.

Akizungumza wakati akifunga chuo hicho, alisema ameamua kufanya hivyo kwa kuwa hakipo kwa mujibu wa sheria, na hakitoi mafunzo kulingana na matakwa ya elimu.

Chuo kina mwalimu mmoja tu ambaye na ye hana sifa za kufundisha wanafunzi sambamba na kukosekana kwa usalama kwenye eneo hilo.

Macha alisema alipokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusiana na uwapo wa chuo bubu katika eneo hilo chenye matatizo, hivyo alikwenda chuoni hapo na kufanya uchunguzi ambao alibaini hata wanafunzi waliopo hawajafanya mtihani kwa mwaka mmoja.

"Chuo hiki hakipo tena kulingana na kukosekana usalama na hakuna mlinzi, huku kukiwa hakuna masomo na shule haijasajiliwa inaendeshwa, hali itakayosababisha uwapo wa wahitimu wasio na sifa," alisema Macha.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka (kulia) pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Ngenya Athuman (kushoto), wakikagua shehena ya mifuko mbadala iliyozalishwa chini ya kiwango walipotembelea kiwanda cha Al-Haseeb Jewellery Limited jijini Dar es Salaam. MPIGAPICHA WETU

# Sababu kiwanda cha mifuko mbadala kutozwa faini Dar

Na Mwandishi Wetu

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limekipiga faini ya Sh. milioni 35 kiwanda cha kuzalisha mifuko mbadala cha Al-Haseeb Jewellery Limited kwa makosa mbalimbali likiwamo la kuzalisha mifuko mbadala iliyo chini ya kiwango cha 70gsm.

Akizungumza wakati wa ziara ya siku moja katika kiwanda hicho kilichopo jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Dk. Ngenya Athuman, alisema uzalishaji wa mifuko mbadala iliyo chini ya kiwango imekua changamoto kubwa kwa Baraza pamoja na wafanyabiashara wa mifuko hiyo wanaofuata sheria na taratibu zilizopo.

Distributed via ipmedia

Alisema viwanda kama cha Al-Haseeb Jewellery ni moja ya vikwazo vinavyorudisha nyuma juhudi za Rais John Pombe Magufuli katika kutekeleza azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda na uchumi wa kati ifikapo 2025.

"Tumepata malalamiko mengi kutoka kwa wafanyabiashara wanaofuata sheria kuwa sokoni mifuko yenye kiwango cha 70gsm haiuziki, na tulipofanya uchunguzi tukagundua uwepo wa wazalishaji kama hawa ambao wamejaza sokoni mifuko isiyokidhi vigezo, huu ni uhujumu wa uchumi kwa taifa," alisema Dk. Gwamaka.

Aliyataja makosa ambayo kiwanda hicho inakabiliana nayo kuwa ni pamoja na kuzalisha mifuko mbadala zaidi ya milioni mbili iliyochini ya kiwango na kupigwa faini ya milioni 20, kufanya uzalishaji bila kufanya tathmini ya athari kwa mazingira (EIA) ambapo faini yake ni milioni 10 pamoja na milioni 5 kwa kusambaza mifuko hiyo katika masoko mbalimbali.

"Fuateni sheria zilizopo kinyume na hapo madhara yake ni makubwa. Ninawaonya wamiliki wengine wa viwanda visivyofuata sheria kufuata sheria kwani mpango wa NEMC ni kuwabaini wote wanaoendesha viwanda kinyume na utaratibu. Nia yetu ni kulinda viwanda vya ndani vinavyofuata sheria ili kuweza kutimizia azma ya serikali ya awamu ya tano ya kuwa nchi ya uchumi wa Kati na viwanda ifikapo mwaka 2025," Dk. Gwamaka alisisitiza.

Hata hivyo Dk. Gwamaka aliongeza kuwa tayari kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaouza mifuko hiyo chini ya kiwango wameshakamatwa na watafunguliwa mashtaka. Aliomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuripoti mambo yote yanayohusiana na uvunjifu wa Sheria ya Mazingira na wao watafanyia kazi taarifa hizo.

Kwa upande wake Dk. Athuman alisema shirika lake halitakuwa na huruma dhidi ya wenye viwanda ambao wamekuwa wakizalisha bidhaa zao chini ya kiwango na wataendelea kuchukua hatua za kisheria.

"Hatuwezi kuchekea vitendo kama hivi vinavyorudisha juhudi za Rais wa nchi yetu, tumejipanga vizuri na tutapambana na kila mtu anayekiuka taratibu zilizopo atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria," alisema Dk. Athuman.

# Mkandarasi mpya ujenzi stendi apewa miezi miwili

Na Happy Severine, SIMIYU

HALMASHAURI ya Mji wa Bariadi mkoani Simiyu, imeingia mkataba na kampuni mbili za ujenzi, Mumangi Trans and Construction Ltd na Pek Brothers (T) Ltd za mkoani Mara kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa mradi wa stendi mpya ya kisasa ya halmashauri.

Mkataba huo wa miezi miwili utahusisha ukamilishaji wa jengo la abiria na utawala pamoja na barabara ya kilometa 1.5 inayozunguka stendi hiyo hadi eneo la Ikulu ndogo kwa gharama ya Sh. bilioni 2.1.

Hatua hiyo imekuja zikiwa zimepita siku 18 tangu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashuari hiyo, Merkzedeck Humbe, achukue hatua ya kuvunja mkataba na Kampuni ya Kings Builders ambaye alikuwa akishirikiana na kampuni ya Helen Construction Co.Ltd za Dar es Salaam ambazo zilikuwa zikijenga stendi hiyo.

Uamuzi huo wa mkurugenzi ulifikiwa baada ya kubaini makandarasi hao hawana uwezo wa kukamilisha ujenzi huo ndani ya muda licha ya kuongezewa muda zaidi ya mara tatu, lakini hawakuweza kuendana na makubaliano ya mkataba.

Alisema mradi huo ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia kwa kushirikiana na serikali unatekelezwa kwa Sh. bilioni 7.2, ambapo mpaka wanavunja mkataba huo, mkandarasi huyo alikuwa amelipwa Sh. bilioni 5.1.

"Kazi hii ilianza rasmi Novemba 3, 2017 na ilitakiwa kumalizika Novemba 3, 2018, lakini ameshindwa kumaliza bila sababu za msingi, ameomba kuongezewa muda mara mbili," alisema na kuongeza:

"Tumekubaliana, lakini bado ameshindwa, kama mwajiri nilipitia vifungu vyote vya sheria na taratibu zinazotakiwa na kuamua kuvunja mkataba."

Humbe alisema kutokana na masharti ya mkataba yaliyopo kati ya serikali na Benki ya Dunia, mradi huo unatakiwa kukamilishwa Desemba 31, 2019, ambapo wamemtaka mkandarasi mpya kukamilisha kazi hizo kabla ya muda huo.

"Tumebakiwa na muda wa miezi miwili kabla ya mkataba huo kuisha, na sisi hatutaki pesa zirudi, tumemwambia huyu mkandarasi mpya afanye kazi usiku na mchana ili tuweze kukamilisha ujenzi huu haraka iwezekanavyo," alisema Humbe.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Jumanne Sagini, ambaye alihudhuria hafla fupi ya utiaji saini wa mkataba huo, alisema kilichosababisha ujenzi huo usikamilike mapema ni viongozi wa halmashauri kushindwa kuchukua hatua mapema.

Alisema mkandarasi wa awali alikuwa akionekana hana uwezo wa kukamilisha kazi hiyo, ambapo alimtaka mkandarasi mpya kuhakikisha anakamilisha ujenzi huo ndani ya muda aliopewa.

"Ndani ya siku tatu tunataka kuona kazi iwe imeanza kwa kasi kubwa, ikiwezekana fanyeni kazi usiku na mchana, tunataka hata kabla ya miezi hiyo miwili kazi ikamilike na ofisi yangu itakuwa ikifuatilia kila wiki ujenzi huu," alisema Sagini.

Mwakilishi wa kampuni hizo, Mathias Nguzu, aliahidi kufanya kazi usiku na mchana, huku akiomba ushirikiano kutoka Ofisi ya Mkurugenzi pale ambapo itahitajika ili kukamilisha kazi hiyo kwa muda waliopewa.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) wa halmashauri hiyo, Mathias Mgolozi, ambao ndiyo wasimamizi wa mradi huo, alisema ujenzi huo unafadhiliwa na Benki ya Dunia na mkataba wa ufadhili unaisha Desemba 31, 2019, na wana uhakika makandarasi hao watakamilisha ndani ya muda huo.



Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, mkoani Arusha, Jerry Muro, akikata utepe kama ishara ya kupokea pikipiki zilizotolewa na Benki ya CRDB, kusaidia doria, wilayani humo jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

Distributed via ippmedia

# Kada wa CCM atimkia Chadema

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

ALIYEKUWA Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Bagara, Stephano Salaho, ametimkia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Katika kutangaza uamuzi huo juzi, alisema alipokuwa CCM hakuwa na haki ya kuzungumza badala yake aliambulia adhabu ya miezi 30 kwa kuwatetea mabalozi wa Kijiji cha Nakwa waliowadhulumu fedha zao.

Alisema amekuwa kiongozi wa Kata ya Bagara kwa miaka 10, lakini alichokiona CCM ni kulewa madaraka na kuwa na ubinafsi, tofauti na Chadema ambao alidai wanatetea wananchi na kusimamia maendeleo.

"Mimi nilitetea mabalozi wa Nakwa ili walipwe fedha zao za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 kwa kwenda Dar es Salaam na Dodoma, lakini niliambulia adhabu ya miezi 30 eti sina nidhamu ambayo nilipewa na uongozi wa wilaya," alisema Salaho.

Aidha, alisema alipokuwa kwenye chama hicho ni kama alikuwa amefungiwa kwenye chupa kwa madai kuwa hakuwa na uhuru wa kuzungumza kuwatetea wananchi badala yake wanachokifanya ni kusifia watu kwa maslahi yao binafsi.

Salaho alisema ameamua kuhamia Chadema ili aungane na watu wachache ambao alidai wanatetea haki kuliko kuendelea kukaa na watu wengi, ambao hawatetei haki za wanyonge bali ni kuangalia maslahi binafsi na kusifiana.

"Mimi sijaja Chadema kwa ajili ya kutaka madaraka bali nataka kutetea wanyonge, tena naona kama nilichelewa kuja huku ambako watu wanatetea wanyonge bila woga," alifafanua.

Alisema amejiunga Chadema kwa kuwa ni wawazi na wakweli na akadai daima wawazi hupondwa na watu wengi, kama ilivyo kwa CCM inavyopinga upinzani kwa ukweli wanaosema.

Aliahidi mbele ya viongozi wa Chadema Wilaya kuwa atakuwa mwaminifu na hatabadilika kama wanasiasa wengine wanaohama na kurejea tena kwenye vyama vyao na atashirikiana na wanachama wa Chadema na viongozi wake kutetea haki za wanyonge zinazopokonywa na CCM kwa sababu ya ubinafsi.

Naye Mwenyekiti wa Chadema Wilaya ya Babati Mjini, Edger Mwageni, akimpokea kada huyo wa CCM, alisema wao wanafanya kitendo cha kumbatiza na kuwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kugombea uongozi wa serikali za mitaa na kupinga kura siku ya uchaguzi.

Tukio hilo la kumpokea kada huyo, lilishuhudiwa na Mbunge wa Viti Maalum, Anna Gidaria, na viongozi wengine ngazi ya wilaya.

# DC akabidhi pikipiki polisi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, jana alikabidhi pikipiki tano kutoka Benki ya CRDB Kituo cha Polisi cha Usa River wilayani humo, kwa ajili ya kuimarisha usalama kwa kufanya doria maeneo mbalimbali.

Akizungumza jana wakati wa hafla ya kupokea pikipiki hizo, Muro alimwagiza Mkuu wa Kituo hicho, David Mapunda, kusimamia zana hizo ili zitumike kwa malengo yaliokusudiwa ili kuzuia uhalifu na si vinginevyo.

Alisema isitokee mtu akazitumia kwa manufaa yake na katika hilo, serikali haitakubaliana nalo kwa sababu hawajatoa mtaji kwa mtu binafsi.

"Pikipiki hizi tumieni kufanya doria kila mahali kwenye wilaya yetu kukomesha uhalifu na hatutaki kuona uhalifu ukifanyika. Lakini naonya msitumie kama mitaji binafsi. Hizi ni za kufanyia kazi iliyokusudiwa," alisisitiza Muro.

Alishukuru CRDB kuwapatia pikipiki hizo ambazo alisema zitasaidia kuimarisha ulinzi wilayani humo na kuwalinda wananchi wake.

Aidha, Muro alisema mikakati ya ofisi ya wilaya na benki hiyo ni kuhakikisha wanaleta maendeleo kwa wananchi, hivyo serikali itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi.

Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na wa Kati kutoka CRDB, Boma Rabara, alisema benki hiyo imetoa pikipiki hizo kutokana na changamoto za usafiri katika kituo hicho hasa kwenye doria.

"Sisi tumekuwa tukichangia kuboresha utendaji wa Jeshi la Polisi na kutoa usafiri ili kuongeza ufanisi wa askari katika kupambana na uhalifu," alisema.

# Mangariba wazidi kubwaga manyanga

**Na Cynthia Mwilolezi,**
HANANG

MANGARIBA wanaokeketa watoto wa kike wilayani Hanang' mkoani Manyara, wanazidi kuachana na kazi hiyo kutokana na elimu inayoendelea kutolewa na serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali na jamii juu madhara ya ukeketaji.

Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Joseph Mkirikiti, akizindua mdahalo wa vijana wa kupiga vita ukeketaji jana kwenye Kata ya Gehandu, ulioandaliwa na Shirika la Civil Social Protection (CSP) Foundation, alisema matukio ya ukeketaji yanazidi kupungua.

Alisema kadri elimu inavyoendelea kutolewa, jamii ya eneo hilo, wafugaji wa Kibarbaig, wanazidi kuachana na vitendo hivyo vya kikatili.

Mkirikiti aliipongeza CSP kwa elimu inayoendelea kutolewa kwa jamii ya eneo hilo, hasa vijijini ili kuhakikisha wananchi wanazidi kutambua madhara ya ukeketaji.

"Nitoe wito kwa watafiti wanaofanya utafiti kwenye vijiji vyetu, watambue kuwa idadi ya matukio ya ukeketaji inazidi kupungua mno tofauti na miaka iliyopita," alisema Mkirikiti.

Mkurugenzi Mtendaji wa CSP, Nemence Iriya, alisema wanaendelea kutoa elimu kwenye wilaya hiyo katika kata 10 na vijiji 20. Iriya alisema wanaendesha midahalo kwa vijana wakiwamo wanafunzi wa shule za sekondari ili kutambua madhara ya ukeketaji na kupinga vitendo hivyo.

Alisema jamii inatakiwa kuwajibika kuchochea mila na desturi rafiki kwa msichana kwa kuwa ukeketaji umeshapitwa na wakati.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, jamii inapaswa kuwalinda wasichana ambao hawajafanyiwa ukeketaji kwa kuhakikisha wanatoa taarifa dhidi ya watu wanaofanya au wanaojihusisha na ukeketaji.


Mkazi wa Katesh, Paulina Longu, alisema jamii inazidi kupata uelewa juu ya ukeketaji na unazidi kutokomea maeneo mbalimbali wilayani Hanang'.

Longu alisema kutokana na mwamko huo na elimu inayoendelea kutolewa, ukeketaji unazidi kutoweka japo elimu inapaswa kuendelea kutolewa na kuwafikia watu wengi zaidi.

Mmoja wa mangariba walioachana na shughuli hiyo, Hawa Hussein, alisema elimu inayotolewa na CSP inasababisha waachane na ukeketaji.

Hussein alirithi kazi hiyo kutoka kwa bibi yake, lakini hivi sasa ameachana nayo baada ya serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kupiga vita ukeketaji.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 2006, matukio ya ukeketaji kwenye Mkoa wa Manyara yapo kwa asilimia 58, huku vitendo hivyo vikifanyika kwa wingi wilayani Hanang'.





# Mchungaji ataka yatima wasaidiwe

**Na Paul William,** MOSHI

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kisamo wa Dayosisi ya Kaskazini, Joram Mamuya, amewataka waumini kuanzisha utamaduni wa kwenda kutoa misaada ya kibinadamu kwa yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu ili kutimiza matakwa ya kiimani.

Aliyasema hayo wakati akikabidhi baadhi ya misaada ya kibinadamu ikiwamo sare za shule kwa yatima na wanaoishi katika mazingira magumu waliopo katika Shule ya Msingi Matemboni, Wilaya ya Moshi.

"Msaada huo umetolewa kupitia ofisi kuu ya Dayosisisi ya Kaskazini Idara ya Udayakonia ambapo kupitia idara hiyo, wamekuwa wakitoa misaada mbalimbali kwa makundi maalum lengo likiwa ni kuwafanya kujiona wapo sawa na watu wengine," alieleza Mamuya.

Alisema watoto hao wana ndoto za baadaye, hivyo jamii ina jukumu kubwa la kuhakikisha inasaidia ili kutimiza ndoto zao kwa maslahi mapana ya Taifa.

"Kupitia idara yetu ya Udiakonia tulifika hapa shuleni na kupewa majina ya watoto 15 ambao wengine ni yatima, lakini wapo wanaoishi katika mazingira magumu, hivyo kupitia wafadhili mbalimbali tumeweza kuwaletea sare za shule leo," alisema Mchungaji Mamuya.

Alisema wataendelea kutoa misaada kwa wenye uhitaji kuhakikisha nao wanajiona sawa na watu wengine.

Mwenyekiti wa Udayakonia Usharika wa Kisambo, Dora Lyatuu, alisema baadhi ya wanafunzi wamekuwa wakikatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kukosa ada na michango mbalimbali ya shule, hivyo wamekuwa wakiwasaidia kuendelea na masomo.

Alisema pia wamekuwa wakiwasaidia wajane, na kuwa wameshajenga nyumba mbili na kuwakabidhi pamoja na kugharamia matibabu kwa kuwakatia bima watu mbalimbali wasiojiweza katika usharika huo.

Naye Mwalimu wa shule hiyo, Haika Temba, alisema shule hiyo ina watoto wanaohitaji msaada wa jamii kutokana na kusomea katika mazingira magumu.

Alisema watoto hao wamekuwa wakivaa sare za shule ambazo zimechakaa, hali ambayo imekuwa ikisababisha kuishi kinyonge na kupelekea kutofanya vizuri katika masomo.

# Vitendo vya kutisha ubakaji, ulawiti

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NI 'aibu' ndivyo unavyoweza kusema kuhusu kushamiri kwa matukio ya ubakaji na ulawiti, baada ya Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Kilimanjaro (Mawenzi), kueleza kwamba kati ya Januari hadi Septemba mwaka huu, watoto waliothibitika kubakwa na kulawitiwa ni 127.

Akitoa taarifa hiyo katika eneo la kambi ya mapadri wazee wa Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi, Dk. Boniface Masau wa hospitali hiyo, alisema kasi ya ubakaji na ulawiti wa watoto inazidi kushika kasi. Alikuwa akizungumza jana wakati akieleza umuhimu wa huduma za afya kwa waathirika wa ukatili wa kijinsia kwenye warsha ya siku mbili ya vyombo vya habari na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Wadau wanaoshiriki warsha hiyo ni wanahabari kutoka mikoa ya Kilimanjaro na Manyara, maofisa ustawi wa jamii, wanasheria, maofisa maendeleo ya jamii na wanaharakati kutoka mashirika ya kiraia.

"Kati ya Januari hadi Septemba mwaka huu, watoto 127 ambao kesi zao za ukatili zilipitia kwetu Hospitali ya Rufani ya Mawenzi, walikuwa wamefanyiwa ukatili ambapo kesi za ubakaji zilikuwa 90 na za ulawiti zilikuwa 37.

"Angalia takwimu za mwaka jana (2018), pale Mawenzi kesi zilizoripotiwa kuhusu ukatili zilikuwa 151 na kati ya hizo 122 zilikuwa ni za watoto kubakwa na kesi 29 zilikuwa ulawiti."

Wiki iliyopita, serikali ilisema kuna haja ya kufanyika upya tathmini ya kitaifa kuhusu hali ya ukatili wa kijinsia, baada ya takwimu za utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) na serikali ya Tanzania zilitolewa miaka mitano iliyopita kushindwa kuwa na uhalisia kwa sasa. Tamko hilo la serikali lilitolewa na Kamishna wa Ustawi wa Jamii nchini anayefanya kazi Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Naftali Ng'ondi, alisema uhitaji huo ni mkubwa kutokana na kuongezeka kwa matukio ya ukatili hasa wa kingono kwa watoto.

Dk. Ng'ond alikuwa akizungumza katika mkutano mkuu wa mwaka na kongamano la kitaifa la Chama cha Wataalamu wa Ustawi wa Jamii Tanzania (TASWO) unaoendelea mjini Moshi.

Takwimu hizo za Hospitali ya Rufani ya Mawenzi ni tofauti na ripoti iliyotolewa wiki iliyopita na Katibu Mkuu wa TASWO, Furaha Dimitrios.

Ripoti hiyo ilileza hali ni mbaya zaidi katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro ambako kati ya Januari hadi Septemba mwaka huu, watoto 157 wameripotiwa kufanyiwa ukatili wa aina mbalimbali.

Katika ripoti hiyo, watoto 52 kati ya hao 157 wamefanyiwa ukatili wa kingono ambayo ni sawa na asilimia 33.



Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule, akimkabidhi cheti cha heshima ya uanzilishi wa Chama cha Walimu cha Akiba na Mikopo cha Same Teachers Saccoss, Omary Mchome wakati wa sherehe za miaka 20 tangu kuanzishwa kwake, jana.
**PICHA: GODFREY MUSHI**

# Ataka utafiti wa changamoto ajira watunza kumbukumbu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amekitaka Chama cha Kitaaluma cha Watunza Kumbukumbu na Nyaraka Tanzania (Trampa), kuanza kuangalia namna ya kufanya utafiti wa kukabiliana na changamoto ya ajira inayoweza kujitokeza katika kada hiyo.

Mghwira alitoa ushauri huo alipokuwa akifungua mafunzo ya siku moja katika Manispaa ya Moshi, ambayo yatafuatiwa na mkutano mkuu wa nane unaotarajiwa kufunguliwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo.

"Fikirieni pia kuhusu hili la changamoto ya ajira kutokana na mabadiliko ya Tehama (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), lipo kundi kubwa la wataalamu lilakalokosa ajira, hivyo jikiteni katika kuhakikisha mnafanya utafiti wa mambo mbalimbali ikiwamo nini chanzo cha kufilisika kwa baadhi ya taasisi za kiserikali na ushirika nchini," alisema.

Alisema ili chama hicho kiendelee kuwa hai, upo umuhimu wa kujadiliana mambo mbalimbali kwa masilahi mapana ya nchi, na kuwa watafiti wa kuona namna ya kukabiliana na changamoto za Tehama.

"Ni kweli tunaelekea katika kuhifadhi kumbukumbu kwa njia za Tehama, kwa hiyo katika ofisi waliokuwa wanahitajika labda wataalamu watano, kupitia mfumo huu watahitajika wawili, hivyo ni lazima chama kione namna ya hawa wengine wanavyoweza kusaidika, napendekeza wajikite katika tafiti zitakazoleta mabadiliko na tija kwa wataalamu,"alisema Mghwira.

Aliongeza: "Na nyinyi watunza kumbu kumbu na nyaraka, jitahidini kuwa waaminifu kwani mnalalamikiwa na changamoto mbalimbali zikiwamo za kuficha nyaraka bila kufika eneo husika na kusababisha kukwama kwa maendeleo, badilikeni fuateni maadili ya kazi zenu ili kuboresha taasisi hii."

Aidha, Mkuu huyo alisema kuwa mbali na taaluma na maarifa wanayoongezewa katika mafunzo hayo pia ni vyema kuleta taarifa nini hutokea baada ya taasisi kufilisika.

Rais wa Trampa, Josephine Manase, aliahidi kufanyia kazi changamoto zinazoikabili taaluma hiyo.

"Tumepokea ushauri na maelekezo uliyoyatoa mkuu, tutahakikisha katika siku hii ya mafunzo tumekumbushana wajibu wetu, maadili ya kazi na namna ya kukabiliana na changamoto hizi," alisema Manase.

ama
ALHAMISI OKTOBA 31, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Binadamu wa leo wanatoka Botswana

Ukurasa 17



Elimu na sheria zawekwa kapu moja kunyoosha wazazi Msalala

Ukurasa 14



Ukurasa 16

Kompyuta kukusanya mapato imezaa neema kwa wagonjwa vituoni Kahama



SHIDA NAULI YAMKWAMISHA ...

# Majeruhi wa ajali abaki kitandani miaka 3 akiikosa ripoti ya malipo

Ukurasa 19



Wananchi walioathirika na matatizo ya hali ya hewa  wakihama. **PICHA: MTANDAO.**

# Tabianchi yaibeba Al- Shabaab, UN yatoswa

**Mogadishu, Somalia**

UCHUNGUZI mpya uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Amani Duniani (SIPRI), unaonyesha mabadiliko ya tabianchi yanatishia kuleta changamoto kubwa kwa walinda amani wa sasa na baadaye nchini hapa.

Ripoti inasema, mabadiliko ya tabianchi yanaongeza changamoto katika sura ya kuimarika makundi ya itikadi kali, wakati tayari miongo mitatu ya mzozo nchini Somalia imeifanya taifa kukabiliwa na ongezeko la ukame.

Matokeo ya mabadiliko ya tabianchi  katika hali ya hewa, yanaongeza shinikizo kwenye mifumo iliyoelemewa ya kiutawala na mahakama nchini hapa.

Hadi sasa kitisho kikubwa dhidi ya mchakato wa ujenzi wa Somalia, ambayo tangu mwaka 1991 imebaki njia panda na ujumbe wa amani wa Umoja wa Mataifa, Somalia (UNSOM) hivi sasa, ikipata kuzuizi kikubwa kutekeleza majukumu yake.

Ripoti imegundua ongezeko la mafuriko, ukame na njaa, hali inayowapa mwanya wanamgambo wa al-Shabaab kujionyesha wana uwezo wa kuisaidia jamii kuliko wawakilishi wa Umoja wa Mataifa.

Ni mkakati wao mpya tofauti na awali, ambao walizuia watu kuondoka kwenye maeneo yao na kuomba misaada kwenye maeneo yanayodhibitiwa na serikali.

Inaelezwa, Al-Shabaab huchukuliwa kama mtoaji bora wa huduma kwa sababu ni kundi linalostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi na UNSOM huonekana dhaifu, hali inayoipa uhalali mbele ya raia.

Pia inaelezwa hatua iliyofikiwa sasa, wananchi wengi wanakimbilia kuhudumiwa katika mahakama za al-Shaabab, kwa madai hazina urasimu na uamuzi wao unatekelezwa, kwa sababu ina uwezo wa kutumia nguvu.

**DW**

AFYA

OPERESHENI MIMBA 'STOP' ...

# Elimu na sheria zawekwa kapu moja kunyoosha wazazi Msalala

## • Viongozi wachoshwa majanga ya likizo
## • Mtindo; mimba, ndoa, mahari ng'ombe

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MIMBA kwa wasichana, awe mwanafunzi au siyo mwanafunzi, haijengi picha nzuri hata kidogo. Inapomgusa aliye masomoni, inakuwa zaidi kwa kuigonga jamii yote.

Pale inapomgusa aliye masomoni, iwe katika elimu ya sekondari au msingi, inakuwa mbaya. Ni Ujumbe unaoweza kusonga mbali zaidi katika mustakabali wa umma.

Hao wanalindwa na tafsiri kutoka sheria nyingi tu, zikitajwa baadhi kama; Sheria ya Watoto, Sheria ya Ndoa iliyofanyiwa marekebisho na na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana.

Mimba za utotoni kwa wanafunzi wa kike, shule za msingi na sekondari nchini, zimekuwa kikwazo kikuu kwao kukosa masomo baada ya kupata ujauzito na kushindwa kufikia ndoto zao ambazo wamejiwekea.

Pia zimekuwa zikiwaweka mbali na jamii kwa kutengwa nakuonekana kuwa hawana tabia njema huku wazazi wengine wakiwakata watoto wao wasiendelee kuwa karibu yao kwa kisingizio kuwa watajifunza tabia mbaya.

Aidha, sababu ya mwanafunzi kubeba mimba akiwa bado shuleni, inatajwa kwamba inasababishwa na ugumu wa maisha wa wazazi, wazazi kuwasisitiza watoto wasifanye vyema kwenye mitihani yao ya mwisho kwa kisingizio hana uwezo wa kumsomesha.

Hata hivyo, Mkoa wa Shinyanga umetajwa kuongoza kitaifa kwa ndoa za utotoni na mimba kwa wanafunzi, ukifuatiwa na Tabora,, Mara, Dodoma, na kisha Lindi. Sababu kuu inatajwa kote ni ugumu wa maisha na kuchukulia kama moja ya kitega uchumi watoto wa kike.

Mikoa mingine inayofuata kwa nafasi kama ilivyofuatana ni: Mbeya, Morogoro, Singida, Rukwa, Ruvuma, Mwanza, Kagera, Mtwara, Manyara, , Pwani, Tanga, , Arusha, Kilimanjaro, Kigoma, Dar es Salaam na Iringa asilimia 8.

Sababu kuu zinazochangia kukua tatizo hilo kila mwaka ni pamoja  na mila na desturi potofu, zinazojengeka katika imani za baadhi ya makabila kuwa 'mtoto wa kike ni mama wa nyumbani na kuolewa tu' huku mtoto wa kiume akiendelea na masomo.


Distributed via ippmedia

Moja ya majengo waliyopewa na Kanisa la Kikatoliki, jimbo la Segese, kwa ajili ya kufundisha masomo ya ziada, wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi na sekondari. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

> **"Lakini wanaoendelea na masomo unakuta ni wanafunzi 30 tu, huku wengine wakiwa wameshaozeshwa na kubebeshwa ujauzito."**

**KINACHOJIRI MSALALA**

Katika kupambana na tatizo hilo, wananchi wa Kata ya Segese, katika Halmashauri ya Msalala, Wilayani Kahama, mkoa wa Shinyanga, wameanzisha kituo cha kuwakutanisha wanafunzi wa kike wanaomaliza masomo ya shule za msingi na sekondari na kuwaandaa kuendelea na masomo.

Patrick Mahona ni Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chela Msalala anayesema, wameanzisha darasa la kuwakutanisha wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi na sekondari na kuwapatia miongozo, pindi watakapochaguliwa kuendelea na masomo.

Anasema, asilimia kubwa ya wanafunzi wanaopata ujauzito kwenye kata ya Segese, ni wale waliomaliza elimu ya shule wakisubiri matokeo, ndipo katika kutumia uhuru huo katika mpito wa subira, wanakutana na madhila ya kunasa mimba, inayokamilishwa kwa ndoa ya mabadilishano ya mifugo kwa wazazi.

"Unakuta kata nzima ina zaidi ya wanafunzi wa kike 800 waliomaliza elimu ya msingi pamoja na sekondari na kufaulu wote," anasema Mahona na kuongeza:

"Lakini wanaoendelea na masomo unakuta ni wanafunzi 30 tu, huku wengine wakiwa wameshaozeshwa na kubebeshwa ujauzito."

Mahona anaendelea: "Huku kwetu mtoto wa kike akimaliza darasa la saba anaozeshwa na kama wazazi wake hawana uelewa juu ya elimu humtafutia mchumba wa kumuoa. Kwa kuliona hilo, tumeamua kuanzisha senta ya kufundisha watoto wote wanaomaliza elimu ya msingi kama njia ya kupambana na mimba."

Anandelea kwamba Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 iliyolalamikiwa sana kuwa na mwanya unaomruhusu binti kuolewa akiwa na umri kuanzia miaka 14 kwa ridhaa ya wazazi na miaka 15 kwa ridhaa ya mahakama, wiki iliyopi-

**Inaendelea Uk. 15**

AFYA

Inatoka Uk. 14

ta kipengele hicho kilibatilishwa na mahakama, kutokana shauri lililofikishwa na wanaharakati.

**KINACHOWAFIKA WAZAZI**

Mahona anasema, kuwa wazazi na baadhi ya viongozi wasio waadilifu wanaonekana kuwa chanzo cha ongezeko la mimba na ndoa za utotoni, kutokana na hawatoi ushirikiano, pindi kesi inapofikishwa mahakamani.

Ofisa Mtendaji huyo anasema wamekuwa wakiwachukulia hatua za kisheria wazazi wanaobainika kutoshiriki katika mashauri.

Sheria ndogo iliyoko katika eneo lao ni kwamba akibainika mtoto wa kike hajafika shuleni kwa zaidi ya siku tatu bila ya taarifa, hutozwa faini ya mifuko mitatu ya saruji.

Pia anasema, wamekuwa wakifutilia ufaulu wa mwanafunzi wa kike kuanzia darasa la kwanza hadi atakapomaliza masomo yake na akibainika kufanya vibaya, wanachukua jukumu la kumhoji mzazi wake na pindi ikibainika kumshawishi mtoto wake kufanya vibaya, anawajibishwa kisheria.

Katika hoja hiyo, mkazi wa eneo hilo

Robert Kisiminza, anajitetea kwamba hana sababu ya kumuozesha mwanafunzi kwa tamaa za mali, badala yake anajikita kumtengenezea mazingira bora ya kutimiza ndoto yake kielimu.

Anasema wamekuwa wakiungana na uingozi kuwachukulia hatua viongozi waliobainika kushiriki kuwaozesha mabinti katika umri mdogo, kutokana na taarifa zinazoripotiwa na wanafunzi wenyewe.

**WAFUGAJI SEGESE**

Warioba Marwa, ni mkazi wa Kata ya Segese, anayesema wameanzisha mpango wa elimu kwa jamii za kifugaji, ili kuwapa mwamko wa kupeleka mabinti zao shuleni na kuwaondolea dhana mbaya kichwani, kwamba mtoto wa kike hana haki ya elimu.

Anasema kuwa wafugaji wengi wamekuwa wakiwapeleka watoto wa kiume pekee shuleni na kuwaachia wasichana majukumu ya nyumbani, kwa madai mtoto wa kike akiolewa wakati ana elimu, familia inayoenda kufaidika ni upande alioolewa.

Pia, Marwa anaongeza kwamba wamekuwa wakipokea mahali wakati binti akiwa mdogo na inapobahatika akapelekwa shuleni, basi akimaliza mwisho wake ni elimu ya msingi tu, kisha anaozeshwa kwa kubadilishana na ng'ombe.

Mwingine ni Imani Elisha, anayeeleza kuwapo wazazi wanaopeleka watoto wa kike shuleni na inapotokea wanafanya vizuri, wanakosa fedha za kuwapeleka shuleni, nao wanaangukia mikono ya kuolewa.

OPERESHENI MIMBA 'STOP' ...

# Elimu na sheria zawekwa kapu moja kunyoosha wazazi Msalala


Distributed via ippmedia

Wanafunzi wa kike na kiume waliohitimu elimu ya msingi katika Kata ya Segese, wakisimama mbele ya madarasa waliyopewa na kanisa.

> **"Tumekuwa tukiwapatia wazazi mifano ya mafanikio yetu ambayo tumeyapata wakati tunapatiwa elimu na wazazi ikiwa kama moja ya kuwahamasisha kutowaozesha watoto na kuwanyima haki za kielimu pindi anapohitimu darasa la saba," anasema.**

Elisha anasema, wazazi katika jamii ya wafugaji wamekuwa wakithamini ng'ombe wanazomiliki, kuliko kuwapeleka watoto shuleni, jambo linalofungua ukurasa wa kuhitajika elimu ya ziada kuwakomboa kifikra jamii hiyo katika vitongoji walivyopo, ili kuwapatia mwanga wazazi, wakitumia mifano ya viongozi wa kike kitaifa na kimataifa waliopo.

**MAKTABA SEGESE**

Mahona anasema, wanatarajia kuanzisha maktaba kwa ajili ya wanafunzi wa shule za misingi na sekondari na watu wazima kuanza kujisomea, hali anayoamini itamsaidia mtoto wa kike na kiume anapotoka shuleni, apatumie kujisomea.

Anasema, moja ya sababu ya wanafunzi kupata ujauzito ni kuwa na muda huru wa kuzurula mitaani, badala ya kujisomea kwa ajili ya mandalizi ya kuendelea na masomo, hali inayomkwepesha na vishawishi vya mimba.

Mahona anasema, watoto wengi wanakosa masomo na kupata ujauzito kutokana na ugumu wa maisha yaliyopo majumbani, baadhi wakitumikishwa katika miradi ya kijasirimali za kifamilia, wanakokutana na umma.

**MWALIMU ALONGA**

Rehema Komba, ni mwalimu wa Shule ya Msingi Busungu, katika Kata ya Chela, anawashauri wazazi kujitahidi kuwapeleka watoto wa kike shule na kuacha tabia ya kuwaozesha kwa kubadilishana na mifugo.

Anasema, idadi kubwa ya walimu wanaofundisha katika shule ya msingi Busungu wanatoka mikoa mbalimbali, ambako anajivuna kwamba waliwapatia elimu wazazi na kuacha tamaa za kuwaozesha.

"Tumekuwa tukiwapatia wazazi mifano ya mafanikio yetu ambayo tumeyapata wakati tunapatiwa elimu na wazazi ikiwa kama moja ya kuwahamasisha kutowaozesha watoto na kuwanyima haki za kielimu pindi anapohitimu darasa la saba," anasema.

"Ukimsomesha mtoto wa kike, unakuwa umeokoa taifa zima. Kwa hiyo tunashauri wazazi wasikimbilie mahari...mahari ipo hata kama akisoma. Mimi nisingesomeshwa wazazi wangu wasingepata mahari na kuwasaidia kimaisha." anasema.

Maximilian Matongo, anachangia kwamba: "Tunajihadi sana kuwajengea uwezo wazazi namna ya kutambua umuhimu wa elimu na mpaka sasa wana wanafunzi 90 waliomaliza darasa la saba, huku wa kike wakiwa 60 kutoka jamii za wafugaji jambo ambalo jamii hiyo imeanza kutambua umuhimu wa elimu."



Mwalimu Maximilian Matongo, aliyeteuliwa na wazazi kuwafundisha wanafunzi waliomaliza elimu ya msingi katika shule za msingi zilizopo katika Kata ya Segese.

AFYA

# Kompyuta kukusanya mapato imezaa neema kwa wagonjwa vituoni Kahama

## DC: Ole wenu igeuzwe ya miziki na sinema



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, akizungumza na wasimamizi wa vituo vya afya na zahanati, wakati wa ufungaji mafunzo ya mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za utoaji wa huduma za afya. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

KATIKA kupambana na upotevu wa mapato ya papo kwa papo katika vituo vya afya na zahanati zilizopo katika Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, halmashauri hiyo imefunga mifumo ya ukusanyaji taarifa za utoaji huduma za afya katika vituo hivyo.

Halmashauri ya Ushetu, ina jumla ya vituo vipya vya huduma za afya 25. Katika mgawanyo huo, kuna vituo vya afya vitatu, zahanati 22 na hospitali moja ya wilaya, inayotarajia kuanza kutoa huduma za kiafya hivi karibuni.

Mfumo huo wa kukusanya taarifa za utoaji huduma kwa wagonjwa sio kwamba umefungwa katika vituo vya afya na zahanati katika Halmashauri ya Ushetu pekee, bali uko nchi nzima na azma ya serikali kufunga mifumo hiyo ni kupunguza gharaza za uendeshaji.

Vituo vya afya na zahanati zisizofungwa mifumo hiyo, hutumia gharama kubwa za uendeshaji kununua karatasi na kuna kasi ndogo ya kuwahudumia wagonjwa, ikiwa ni pamoja na upotevu wa fedha za papo kwa papo na kushuka kwa mapato.

Wingi wa zahanati na vituo vya afya vimepunguza usumbufu kwa wananchi wa halmashauri hiyo kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 100 kufika katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama kupatiwa huduma za matibabu.

> **"Nakuagiza ofisa Tehama, kuhakikisha unazikagua mara kwa mara kompyuta zote zitazofungwa kwenye vituo vya afya na zahanati na ukibaini zitakazokuwa na sinema na muziki, toa taarifa kwangu haraka iwezekanavyo, ili tuweze kuwachukulia hatua za kisheria mara moja," anasema.**

Pia, vimepunguza wimbi la vifo vya kinamama wajawazito na watoto, ambao awali walijifungulia njiani wakati wakielekea katika Hosptali ya Mji wa Kahama, kufuata matibabu, sambamba na vifo vya watoto.

**MGANGA MKUU**

Nicodemus Senguo, ni Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, anayesema mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za utoaji wa huduma za afya utasaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti upotevu wa fedha za papo kwa papo, ambazo hutolewa na wagonjwa wanaofika katika vituo kupatiwa huduma.

Anasema, pia utasaidia kuongeza uwajibikaji kwa watumishi na kuongeza kasi ya utoaji huduma sambamba na kutunza kumbukumbu za wagonjwa ambao katika kipindi cha nyuma mgonjwa akitibiwa leo, aliporudi baada ya siku tatu, nyaraka yake inakuwa vigumu kupatikana kwa urahisi.

Senguo anasema kuwa, Halmashauri ya Ushetu ilitenga kiasi cha Sh. milioni 96 za kununua vifaa vya mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za utoaji wa huduma za afya ambavyo vitatumika kwenye vituo vya kutolewa huduma 25, huku vituo vya afya zikiwa vitatu na zahanati 22.

Anasema, lengo wa ufungaji mifumo hiyo kwenye vituo vya afya na zahanati ni kuongeza huduma ya mapato, upotevu wa fedha za papo kwa papo, uwajibikaji na kupunguza gharama za uendeshaji wa vituo na upotevu wa taarifa za wagonjwa.

**NISHATI UMEME**

Hata hivyo, Senguo anasema kuwa, kukosekana nishati ya uhakika ya umeme katika vituo vya afya na zahanati, inatishia kukwamisha matumizi ya mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) wa ukusanyaji wa taarifa za utoaji huduma za afya.

Aidha anasema umeme umefika hatua ya baadhi ya kata na kukitarajiwa kufika katika vituo vyetu vya kutoa huduma za kiafya, na kusisitiza vituo vyote vya matibabu vimeshafanya mfumo wa upokeaji nishati ya umeme, japo vinaendelea kutumia nishati ya jua.

Anasema kuwapo umeme wa nishati ya jua katika vituo vya afya na zahanati, kunaweza kukasababisha kuwa na changamoto ya uendeshaji wa mfumo huo, huku kati ya vituo vya afya vitatu na zahanati 22 kituo kimoja cha afya ndicho chenye nishati ya umeme wa uhakika na zahanati tatu.

Pia anasema Halmashauri ya Ushetu imetenga fedha Sh.milioni 20 kupitia mapato yake ya ndani kwa mwaka wa fedha uliopo; 2019/2020 kwa ajili ya kuongeza nishati ya jua kwenye vituo vya afya na zahanati vyenye nishati ya jua ya kusuasua, ili inapotokea tatizo waweze kukabiliana nalo.

**MKUU WILAYA**

Anamringi Macha, ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, anayesema kupitia Mradi wa Umeme Vijijini (Rea) Awamu ya Tatu, wanatarajia kupeleka umeme katika vijiji vyote 53, zahanati na vituo vya afya vitakayokuwa na zahanati zitapewa kipaumbele.

Anasema, kwa sasa waendelee kutumia nishati ya umeme wa jua ambayo ipo na wasitumie vifaa vya umeme visivyoruhusiwa hospitalini kama vile pasi majiko ya kupikia chai, ili kufanikisha kutumia mfumo huo vyema.

"Kuna baadhi ya maeneo watumishi wa umma wanatumia umeme vibaya. Wanakwenda na mabegi ya nguo wananyooshea nguo kazini, kwa lengo la kupunguza nishati ya umeme majumbani mwao na wengi wanakwenda kupikia maharage ofisni badala ya nyumbani," anasema Macha.



Wasimamizi wa vituo vya afya na zahanati kutoka katika Halmashauri ya ushetu wilayani hapa mkoani Shinyanga wakimsikiliza Mkuu wa Wilaya ya kahama, Anamringi Macha hayupo pichani

**HATUA KISHERIA**

Mkuu wa Wilaya anatahadharisha kwamba hatosita kuwachukulia hatua za kisheria wauguzi na wasimamizi wa vituo vya afya na zahanati watakaobainika kuweka muziki na sinema kwenye kompyuta zenye mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za utoaji wa huduma za afya.

Anasema komputa zilizofungwa mfumo huo, zinatakiwa kutumika kwa malengo yaliyopangwa na si vingnevyo, huku akimuagiza Ofisa Tehama kufanya ukaguzi wa kila mara kubaini mwenendo na kuwachukulia hatua dhidi ya watakaobainika kukiuka agizo hilo.

"Nakuagiza ofisa Tehama, kuhakikisha unazikagua mara kwa mara kompyuta zote zitazofungwa kwenye vituo vya afya na zahanati na ukibaini zitakazokuwa na sinema na muziki, toa taarifa kwangu haraka iwezekanavyo, ili tuweze kuwachukulia hatua za kisheria mara moja," anasema.

Macha: "Endapo mfumo utasumbua, hakikisheni mnatoa taarifa kwa Ofisa Tehama wa Halmashauri, ili aje ashughulikie tatizo litalokuwepo na sio kujifanya fundi au kuwatumia mafundi wa mitaani, ambao wataichezea mifumo hiyo na kuiharibu na 'kudukua taarifa za serikali.

Pia, anawataka wasimamizi wa vituo vya afya, kuacha kuichezea mifumo hiyo kwa kutaka kuingiza taarifa za udanganyifu na kuhakikisha kila huduma watakayoitoa kwa wagonjwa wanaofika vituoni, wahakikishe inawekwa kwenye mfumo huo.

**WASIMAMIZI AFYA MSIMAMIZI KITUO**

Baraka Clement, ni msimamizi wa Kituo cha Afya cha Ushetu-anase anasema, ufungaji mfumo huo utaongeza kasi ya utendaji kazi na kutunzaji taarifa za wgonjwa, wakati ule ukihumdumia mgonjwa akirejea baada ya siku tatu ilikuwa ni vigumu kupata taarifa zake.

Anasema kuwa, mfumo huu utasaidia pia kuwabaini wale watumishi ambao sio waadilifu na waliokuwa wakitumia fedha za papo kwa papo ambazo hutolewa na wagonja wanaofika katika vituo vyetu kupatiwa huduma za kiafya.

Pia anawaasa wasimamizi wa vituo vya afya na zahanati kuacha kutumia vitu ambavyo vinatumia umeme mwingi kama vile pasi na kuacha kuweka sinema na muziki kwenye mifumo hiyo, ili kuweza kufanikisha ukusanyaji wa mapato na taarifa.

Stanely Azaki ni Ofisa Tehama kutoka Halmashauri ya Msalala, anayetoa ufafanuzi kwamba ili kufanikisha mifumo hiyo iendelee kufanya kazi, ni vyema kufanyika ukaguzi wa kila mara kuweka umeme wa unaohakikisha unaendelea kutumia nishati ya jua.



Kusini mwa Mto Zambezi, Botswana ambako maji yamekauka na kumejaa chumvi, kunatajwa ndiko binadamu wanakotokea. **PICHA: BBC.**

# Binadamu wa leo wanatoka Botswana

WANASAYANSI wanalitaja eneo la Kusini mwa mto Zambezi, nchini Botswana ndiko binadamu wote walio hai leo kuna asili yao.

Ni eneo ambalo kwa sasa limejaa chumvi nyingi, ingawaje historia inataja kuna wakati lilikuwa ziwa kubwa, ambalo huenda likawa ndio chimbuko la wanadamu tangu miaka 200,000 iliyopita.

Watafiti wanasema, wazee waliotangulia waliishi huko kwa miaka 70,000, hadi hali ya hewa ilipobadilika na wakaanza kusogea wakati ardhi yenye rutuba ilipozidi kugunduliwa na kuchangia uhamiaji wa vizazi viilivyofuata kutoka Afrika.

"Limekuwa wazi kwa muda fulani sasa kwamba kimaumbile, binadamu wa leo waliokuwapo Afrika kwa kukadiria miaka 200,000 iliyopita," anasema Profesa Vanessa Hayes, mtaalamu wa masuala ya jenetiki kutoka chuo cha utafiti nchini Australia, kiitwacho Garvan Institute of Medical Research.

"Kile ambacho kimejadiliwa kwa muda mrefu ni eneo maalum la wapi walikozuka na kufuatia na kutawanyika kwa mababu waliotangulia," anaeleza mtafiti huyo.

Analitaja eneo Kusini mwa Mto Zambezi, Kaskazini mwa nchini Botswana na watafiti wanahisi binadamu wa kale walitua karibu na mfumo mkubwa Afrika kwenye Ziwa , Makgadikgadi ambalo hivi sasa kumejaa chumvi.

"Ni eneo kubwa mno, huenda lingekuwa na maji maji sana, na ardhi yenye kuvutia," anasema Profesa Hayes na kuongeza: "Na huenda lingekuwa eneo zuri la kuishi kwa binadamu wa leo, pia wanyama."

Baada ya kuishi kwa miaka 70,000, watu walianza kuondoka na mabadiliko katika namna ya mvua inavyonyesha, yalichangia mawimbi yaliyowahamisha kati ya miaka 130,000 na 110,000 iliyopita, yakichangiwa na kufunguka ardhi yenye rutuba.

Wahamiaji wa kwanza walielekea Kaskazini Mashariki, na kufuatwa kwa wimbi la pili la wahamiaji waliosafiri kuelekea Kusini Magharibi, na idadi ya tatu ya watu walisalia katika eneo hilo mpaka leo hii.

Taswira hiyo imetokana na kuangalia nyuma muundo wa familia za binadamu kwa kutumia mamia ya sampuli za vunasaba za DNA zinazotoka kwa kizazi cha mama wa Kiafrika walioko sasa.

Kwa kuchanganya elimu hiyo na Jiolojia, ikiongezwa na ufuatiliaji kutumia kompyuta na hali ya hewa, watafiti walifanikiwa kutoa taswira ya namna Bara la Afrika, lilivyokuwa katika miaka 200,000 iliyopita.

Ripoti ya utafiti huo uliochapishwa katika Jarida la Nature, ambalo ni la kitaaluma, ulifanyiwa mapitio ya kina na ikaweka pingamizi kwamba ni vigumu kuunda upya hadithi ya chimbuko la binadamu, kutokana na vinasaba vya DNA pekee.

Uchambuzi au tathmini nyingine, inatoa majibu tofuati kwa kutumia ugunduzi wa mabaki ya kiumbehai, kuashiria chimbuko lao limetokea Afrika Mashariki.

Profesa Chris Stringer, aliyeko katika Jumba la Kitaifa la Ukumbusho wa Historia, jijini London, Uingereza ambaye hakushiriki katika utafiti huo, anasema "mageuzi ya binadamu wa kale 'Homo sapiens' ulikuwa ni mfumo mgumu."

"Huwezi kutumia usambazaji wa 'DNA mitochondrial' peke yake kutambua eneo moja la chimbuko la binadamu wa leo," anafafanua kwa kuhimiza kwamba:"Nadhani inapita kiwango cha 'data' kwa sababu unatazama sehemu moja tu ya muundo huo kwahivyo hauwezi kukupa taarifa kamili ya chimbuko letu."

Hivyo basi, huenda kukawapo chimbuko nyngi au maeneo walikotoka binadamu wa leo, kuliko hilo moja.

**Hatua zilizopigwa**

Hadi sasa hatua zilizopitiwa katika historia ya mageuzi ya binadamu yanahusu: Miaka 400,000 iliyopita; Neanderthal binamu zetu waanza kuonekana na kusogea bara la Ulaya na Asia; miaka 300,000 hadi 200,000 iliyopita, Homo sapiens binadamu wa leo waonekana Afrika; na miaka 50,000 hadi 40,000 iliyopita: Binadamu wa leo wafika Ulaya.

- ***Kwa mujibu wa mtandao.***

AFYA

# Watafiti, washirika wanapopima zigo la malaria kwa maendeleo

Na Michael Eneza

MALARIA ni ugonjwa wenye nafasi ya kipekee katika mpangilio mzima wa jitihada za kulinda afya nchini.

Katika nyakati zilizopita, ulikuwa ugonjwa unaosumbua maeneo mengi duniani na hasa ukanda wa joto. Hadi sasa kuna maeneo yanayokabiliwa na msukumo huo wa malaria.

Baadhi ya maeneo yaliyopata 'salamu' za malaria ni kwenye mataifa ya watu wengi zaidi duniani, kama India na China, ambako kuna joto na ukanda wa tropiki, Indonesia na Brazil katika ukanda wa Ikweta.

Tofauti iliyopo ni kwamba, nchi hizo hivi sasa zimeanza au zimeshafikia hatua karibu na udhibiti kamili wa malaria, ikiiacha Afrika kwa sasa inabeba sehemu kubwa ya mzigo wa malaria duniani.

Moja ya changamoto zinazotajwa zaidi katika suala la udhibiti wa malaria, ni kuzoeleka tiba za kawaida kwa baadhi ya aina kuu za visababishi vya ugonjwa huo.

Mojawapo ya vyanzo vinatajwa ni kuzoeleka dawa na matumizi holela ya dawa zilizopo. Pia, kuna maeneo mengine ambako mamlaka za dawa za nchi tofauti na mashirika ya Umoja wa Mataifa, hasa yenye wajibu mkuu, Shirika la Afya Duniani (WHO), inaamua kubadili aina za dawa zinazotumika.

Ni hatua inayochukuliwa hata kama bado kuna watu wengi wanaomudu kudhibiti malaria kwa dawa zilizozoeleka. Matokeo yake, ni dawa za majaribio zilizowapata tabu baadhi ya watumiaji.

Hiyo inaleta ujumbe kwamba, siyo jambo la ajabu kuona uwapo wa utafiti wa malaria, namna ya kusambaa kwake nchini na ufanisi wa dawa zinazotumika, kwa aina tofauti za malaria na makundi tofauti ya watu.

**MWAMKO WA UTAFITI**

Inaelezwa umuhimu katika kazi za Chuo Kikuu cha Tiba Muhimbili (MUHAS) na nyinginezo nchini, zikashirikiana na wadau wa taaluma kutoka maeneo mengi duniani wenye mwelekeo wa kuelewa matatizo ya tiba katika eneo la joto na udhibiti wa malaria barani Afrika.

Hiyo inaweza kufanyika kwa kuangalia kinachotokea nchini. Utafiti wa miaka ya karibuni, umegusa maeneo mengi kuelewa ugonjwa huo na ufanisi wa tiba katika nyanja takriban zote.

Tafiti zimeshafanyika katika maeneo mengi ambazo ni endelevu, zikiwafungulia milango wataalamu kupata picha pana ya kuzuka magonjwa (yaani malaria) kwa maeneo tofauti na aina za hali ya hewa, lishe na viwango vya maisha kwa jumla.

Pia, inasaidia kupanua wigo wa kupatikana vielelezo mahali dawa zinashindwa kufanya kazi, inapotokea jamii inakuwa dhaifu kiafya na wanaugua kirahisi.



Kampeni ya ugawaji dawa za mbu. Picha ya chini, mbu anayesumbua. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> **Nchini Uganda, ilifika hatua serikali wakati fulani iliamua kurudisha matumizi ya dawa aina ya DDT, iliyopigwa marufuku duniani na Umoja wa Mataifa, miaka iliyopita, ikielezwa kwamba inaacha sumu isiyodhibitika katika mazingira, hasa imapoingia katika mkondo wa maji na chakula cha nyumbani.**

Hivyo, inaelezwa kwamba ni vyanzo vya kawaida vinavyopatikana kwa pamoja na kuna njia za kubainisha chanzo kinachofanya kazi zaidi katika eneo fulani, kwa kutangulizia utafiti, kisha ndiyo vinaagaliwa vyanzo vingine.

Ni namna inayojenga njia sahihi inayosaidia kupima ufaulu kwa namna tofauti za kupambana na malaria.

**CHANGAMOTO**

Moja ya changamoto iliyopo katika kupambana na malaria ni tofauti kubwa za uwezo wa udhibiti kutoka eneo moja hadi jingine, kulingana na miradi iliyowekwa katika maeneo hayo ambayo kwa kiasi kikubwa yanategemea wafadhili wa kimataifa.

Katika upande mmoja wa Muungano, Zanzibar, kunatajwa kufanikiwa kudhibiti malaria kwa kiwango kikubwa sana.

MUHAS inasema, kujaza mapengo hayo kunabidi wadau washirikiane zaidi, huku Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID), linatajwa kuwa na mchango mkubwa kudhibiti malaria, Zanzibar.

Huo ni mpango uliounganishwa na jitihada za Marekani kusaidia Tanzania na nchi nyingine za Afrika, kupambana na maambukizi ya virusi vya ukimwi na kifua kikuu.

Nchini Uganda, ilifika hatua serikali wakati fulani iliamua kurudisha matumizi ya dawa aina ya DDT, iliyopigwa marufuku duniani na Umoja wa Mataifa, miaka iliyopita, ikielezwa kwamba inaacha sumu isiyodhibitika katika mazingira, hasa imapoingia katika mkondo wa maji na chakula cha nyumbani.

Zilishafanyika kampeni za kuzuia matumizi ya dawa hizo nje ya nyumba kuzuia athari zake kwa binadamu, lakini ikagundulika haitazuia dawa hiyo kuingia katika mikondo ya maji na chakula (mboga).

Kinachojengeka katika mtazamo wa jumla ni kwamba, udhibiti wa malaria ndani ya umasikini, katika hali ya kawaida siyo kazi rahisi.

Hiyo inatajwa ni athari katika mazingira ya umaskini na makazi yaliyokosa ubora katika kudhibiti usambaaji maji, uoto wa majani na madimbwi, wakati lishe za kaya tofauti hazileti tija ya kutosha kuwezesha mwili kutumia kinga asili dhidi ya malaria.

Kupungua vipato kwa jumla, kunaleleta changamoto ya ununuzi wa dawa, licha ya upatikanaji wake umeboreshwa katika vituo vya afya.

Ongezeko la watu katika baadhi ya maeneo, ina uelekeo wa watu kuambukizwa malaria. Pia, kuna watoto wanaoathirika na maskani duni na utumiaji holela wa dawa, kwani si rahisi kila mtoto akapata homa apimwe na kupewa dawa stahili kwa dozi sahihi.

Fundisho la muhtasari wa tafiti kuhusu malaria kwa mwaka huu, ni tofauti na udhibiti wa malaria kutokana na uwepo wa misaada kutoka nje ya nchi na mikoa tofauti.

Jitihada zilizopo sasa zinawasukuma wafadhili kutoa ushirikiano zaidi.



AFYA

SHIDA NAULI YAMKWAMISHA ...

# Majeruhi wa ajali abaki kitandani miaka 3 akiikosa ripoti ya malipo

- Agalagala bila msaada, mke ayeyuka
- Mama abeba jukumu lake na watoto
- Simulizi ya mlo wao 'Mungu anajua'

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KUNA wakati aliyekuwa Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Said Mwema, wastani wa mwaka mmoja baada ya kupewa nafasi hiyo, alitaja changamot0 kuu kwake ilikuwa katika ajali za barabarani, baada ya kupiga hatua katika kuwakabili majambazi.

Hadi sasa ni mtazamo unaumiza vichwa na hakuna anayeweza kujiweka kando nalo. Polisi na Mamlaka ya Kudhibiti wa Usafiri Ardhini (Latra) na raia kwa ujumla ni waathirika wakubwa wa ajali za barabarani.

Inatajwa, changamoto yao ni kutojua haki zao za msingi pindi wanapopatwa na majanga kama hayo.

Sheria ya Bima ya Mwaka 2009, ina ufafanuzi bayana kuhusu malipo ya fidia halali za wananchi walio na kinga za bima, baada ya kupatwa na majanga, huku Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1974, inamtaka mtu kulipwa fidia anapopata ajali ya gari.

Pia sheria hiyo ya usalama inafafanua kwamba mtu anapokufa kutokana na ajali ya gari, basi kikao cha familia kinatakiwa kikae na kumteua atakayetambulika kisheria kufuatilia malipo na fidia zote.

Licha ya kuwapo haki hizo za kisheria, lakini inaonekana wengi katika jamii hawana uelewa wa kutosha uhusu suala la fidia, pindi wanaopata ajali. Huangukia katika kukosa haki zao za msingi.



Picha tofauti za maisha ya Anthony Juma akiwa na wanawe katika maisha yake ya sasa, nyumbani kwao wilayani Bahi, Dodoma anakoishi kwa msaada wa mama yake mzazi. **PICHA ZOTE: AUGUSTA NJOJI.**

**MKASA ULIOJIRI**

Wakati katika jamii kuna kundi la waathirika waliokosa haki zao za msingi kwa kushindwa kufuatilia fidia, hali ni tofauti kwa kijana Anthony Juma (30), aliyepata ajali ya kugongwa na gari mnamo Oktoba 4, mwaka 2015 katika mji wa Bagamoyo mkoani Pwani.

Ni tukio lililobadilisha ghafla maisha yake. Leo hii inatimu miaka mitatu na wiki nne kasoro siku moja, kijana huyo anaishi kwenye mateso, akiwa amedhurika mgongoni na hivyo kumfanya maisha yake yaishie kitandani.

Pamoja na mateso hayo, Juma ambaye kwa sasa anaishi katika kijiji cha Mwitikila wilaya ya Bahi, umbali wa kilomita 71 kutoka Dodoma mjini, anasema ameshindwa kupata haki zake.

Sababu kuu anaitaja ni kwamba amekosa nauli ya kufuata ripoti ya daktari, ili aiwasilishe kwenye kampuni ya bima, afike uwezo wa kulipwa fidia.

Juma anasema, alipata ajali ya kugongwa na gari Toyota Saloon yenye (namba tunazo), majira ya mchana wa Oktoba 4, 2015 katika mji wa Bagamoyo mkoani Pwani akiwa na baiskeli yake kwenye harakati za kutafuta riziki.

**"Nikiwa wodi ya Sewa Haji – Muhimbili, alikuja Rais John Magufuli kwa mara ya kwanza. Alikuta wagonjwa tumejazana ndipo akatoa pesa za kutengeneza mashine zilizoharibika na tukahamishiwa jengo la ghorofa na chakula nikawa napata na matibabu kiasi," anasema.**

Anasema ni mkasa uliomfanya amzimie na alizinduka siku mbili baadaye, Oktoba 6, akijikuta yuko wodini katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

"Waligundua sijafa, walinisaidia huduma ya kwanza na kunikimbiza Muhimbili, ambako nilizinduka siku ya tatu. Watu wa Bagamoyo na Polisi ndiyo walifanya niendelee kuhema hadi leo," anaeleza.

Majeruhi huyo anasimulia kwamba, madaktari walimsaidia hata wakafanikiwa kuokoa maisha yake, ingawa kuna sura ya pili kwamba gharama za matibabu kwake ilikuwa mtihani mkubwa, kwani hakuwa na bima ya afya.

Anasema wakati huo mmiliki wa gari lililomgonga (anamtaja) ndiye alishughulikia hadi alipopata nafuu kisha akamwambia gari yake ilikuwa na bima, hivyo afuatilie.

"Nikiwa wodi ya Sewa Haji - Muhimbili, alikuja Rais John Magufuli kwa mara ya kwanza. Alikuta wagonjwa tumejazana na ndipo akatoa pesa za kutengeneza mashine zilizoharibika na tukahamishiwa jengo la ghorofa na chakula nikawa napata na matibabu kiasi," anasema.

Hata hivyo, anasema alikaa hospitalini hapo hadi Aprili 2017, huku akidai kuwa umasikini wa kipato umechangia kukaa muda wote baada ya kumkosa wa kufuatilia matibabu yake, baada ya mke kumkimbia.

Anabainisha kuwa, mdogo wake Martin Juma (27), alilazimika kuuza kila kitu kijijini, ikiwamo mashamba, ili kuwezesha kurudisha Anthony.

Ni safari anayosimulia kwamba, alichukua siti ya nyuma ya basi ambayo ni kwa ajili ya abiria watano kumfikisha ndugu yake aliyepata ulemavu, akiwa na maisha ya kulala tu.

"Aprili mwaka 2017 nilirudishwa kijijini hapa Mwitikila nikiwa na majukumu ya kuwahudumia watoto wangu wawili ambao mke wangu alikimbia na kuwaacha baada ya mimi kupata ajali na kukaa muda mrefu hospitali,"anasema.

Anasema maisha yake kwa sasa ni ya tabu, shida si suala la chakula pekee, bali hata msongo wa mawazo kuhusu hatima ya watoto wake wadogo, vidonda vikubwa vilivyopo mgongoni na sehemu za makalio, kwa sababu ya kulala.

"Ukiacha hii shida niliyo nayo, lakini nawaza nitapataje nauli ya kufika Hospitali ya Muhimbili kupata ripoti ya daktari, ili nilipwe na bima," anaeleza Anthony

Anasema kampuni ya bima ilishakubali kumlipa fidia yake, lakini tatizo lililopo ni kukosekana ripoti ya daktari, ambayo ndio kugezo muhimu kuidhinisha malipo hayo.

"Kikubwa naomba wasamaria wema na serikali mnifikishe Muhimbili ili nipate 'medical report' (ripoti ya matibabu), ili niweze kulipwa fedha zitakazosaidia matibabu ya afya yangu,"anasema.

Anaendeklea:"Kama ningelipwa huenda ningeweza kupunguza maumivu ya mwili na vidonda vingetibiwa, lakini ningetafuta jinsi ya kuwekeza kwa ajili ya maisha

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Daktari matatani; mtoto azaliwa bila pua, macho, fuvu lake haliko sawa

•Umma waja juu, aupisha uchunguzi
•Aibuliwa mikasa kibao inayofanana


Mjamzito akihudumiwa nchini Ureno. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Mwandishi Wetu**

DAKTARI wa nchini Ureno, ameingia matatani baada kumhudumia mwanamama tangu ujauzito mchanga, lakini akaishia kujifungua mtoto asiye na pua, macho na baadhi ya sehemu ya fuvu la kichwa chake.

Mzazi wa mtoto huyo, aliyetambulishwa kwa jina la Rodrigo, anasema hakufahamu kama atakabiliwa na hali isiyo ya kawaida kwa mwanawe aliyezaliwa mapema mwezi huu kwani mara zote aliambiwa 'mambo safi.'

Maofisa wa Baraza la Tiba, walifikia uamuzi wa kumsimamisha kazi Daktari Artur Carvalho, kuhusiana na tuhuma hizo, ili uchunguzi uchukue nafasi yake.

Inadaiwa kwamba mkasa huo si wa kwanza kwa daktari huyo kukabiliwa nayo, kwani ndani ya wastani wa muongo mmoja uliopita, kuna mikasa kama hiyo inayomuangukia daktari huyo, kwa watoto wengine waliozaliwa chini yake. Hata hivyo, amekuwa akiikwepa

Ripoti ya matukio hayo inaelezwa kwenda mbali katika vyombo vya habari vya Uturuki na Dk. Carvalho amekuwa kimya kusema lolote kuhusiana na mkasa huo unaomuangikia sasa .

Kilichotokea

Mkasa wa safari hii ni kwamba mtoto mchanga alitwaye Rodrigo, alizaliwa wiki tatu zilizopita, mnamo tarehe 7 ya mwezi huu katika Hospitali ya São Bernardo, iliyoko Setúbal, nje kidogo ya mji mkuu wa Lisbon.

Mama wa mtoto huyo katika kipindi cha ujauzito anasema alikuwa mikononi mwa Daktari Carvalho, alikofantiwa vipimo vya 'ultra-sound' mara tatu katika ujauzito wake na mara zote, daktari hakueleza kuwapo dalili za shaka yoyote, inayohusiana na afya ya mama na mtoto.

Katika maendo hayo, mama huyo anasema alifanya vipimo vingine vya aina ya 'ultrasound' katika kliniki nyingine tofauti alikoelezwa dalili ya kutokuwapo hali isiyo ya kawaida kwa mtoto tumboni.

"Alinieleza kuna uwezekano baadhi ya viungo vya mtoto (kupitia ultrasounds) havitakuwapo," anatamka shangazi wa mtoto huyo wa kiume, ambaye madaktari walisema ataishi kwa saa kadha, lakini hadi sasa ana wiki mbili za uhai, chini ya uangalizi wa hospitali .

Maofisa afya wanasema, hadi sasa kuna mlolongo wa malalamiko yasiyopungua sita dhidi yake kutoka kwa wazazi, ikianzia mwaka 2013.

Huko nyuma mwaka 2011, kuna mkasa uliomhusu kuzaliwa mtoto ambaye miguu na mwili haijakaa sawa, pia akili yake. Mama wa mtoto huyo, aitwaye Laura Afonso, alifikisha malalamiko hayo katika mamlaka ya kisheria, lakimi daktari hakuchukuliwa hatua.

Mama huyo anaeleza hadi sasa mtoto ana umri wa miaka minane, ameshafanyiwa upasuaji mara nyingi, lakini suala la uwezo wake kutembea bado ni mtihani, hakuna mabadiliko.


Dk. Artur Carvalho, aliyeko matatani.

Huko nyuma mwaka 2007, mtoto mwenye umri miezi kadhaa alifariki, katika mkasa unaolalamikiwa kwamba ni uzembe wa daktari huyo.

Nao ulichukua sura pana ya hasira ya umma, kwamba mikasa imetawala nchini Ureno kuhusiana na utata dhidi ya mifumo ya afya katika nchi hiyo, ambayo sasa imezua maswali katika jumuia katika nchi hizo.

Sasa kunatajwa kuwapo maswali yanayozuka, namna mfumo wa afya katika nchi unavyofanya kazi, huku Rais wa Chama cha Madaktari wa Ureno, Miguel Guimarães, wiki iliyopita alisema kwamba alishazungumza na Dk. Carvalho, kumueleza hali inayojiri dhidi yake kutoka upnade wa kilio cha umma

Anasema daktari huyo mlalamikiwa, hadi sasa ameshasimama kazi kupisha uchunguzi wa malalamiko dhidi yake na chombo cha nidhamu cha Bodi ya Madaktari, kiliamua kumsimamisha kazi kwa miezi sita, uchunguzi dhidi uchukue nafasi.

Mkuu wa Baraza la Madaktari, Alexandre Valentim Lourenco, anafafanua msimamo wa awali kwamba, kuna ushahidi wa kutosha kwa tuhuma zinazomkabili daktari mlalamikiwa.

Lourenco anaeleza kwamba, hivi sasa chombo hicho kinafanyika kutuliza hali ya hewa dhidi ya misuguano kuhusu matatizo ya kinamama wajawazito kutokuwa na madaktari

# Majeruhi wa ajali abaki kitandani miaka 3 akiikosa ripoti ya malipo

**INATOKA UK.19**

ya baadaye kwa wanangu."

**MAMA YAKE**

Mama mzazi wa Anthony, Juliana Mshegamo, anasema maisha ya familia yake yalibadilika tangu mwanawe alipopata ajali, kwani sasa anaishi maisha magumu hata mlo kwake ni wa shida.

"Kwa umri huo, amerudi kuwa mtoto ninayemhudumia kwa kila kitu. Lakini angelipwa, labda angejenga hata kibanda kwa ajili ya kuishi na watoto wake, kwa hapa maisha ni magumu sana," anasema

Anafafanua kwamba, hata majirani wamemsaidia sana, ila wamefika hatua wamechoka, kwani mahitaji ni mengi, yakiwamo matibabu ya vidonda mwilini yatokanayo na kulala muda mrefu.

"Tunasaidiana na ndugu. Tunamtoa nje ili aone mwanga wa jua, lakini nafanya hivi kila baada ya kupata mtu wa kusaidiana naye kumtoa. Kama hapa tumemtoa baada ya kukaa mfululizo siku nane hatujamtoa," anasema.

**MWENYEKITI KIJIJI**

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwitikila, Albert Mlulu, anasema kijana huyo anaishi maisha ya tabu na watoto wake, anaungana na matazamo wa kuhitajika msaada wa haraka utakaomnusuru maisha yake.

Mlulu anasema, kijana huyo anahitaji kusafiri na watu angalau wawili kwa ajili ya kusaidiana kumbeba kwenda Dar es Salaam, hivyo ni gharama wanayoshindwa kuimudu.

"Kama ulivyomuona lazima kuwapo watu wengine wawili angalau, kwa hiyo gharama zake zinatakiwa si chini ya Sh. 500,000 hivi ndiyo anaweza kufika (Hospitali) Muhimbili kufuata taarifa ya daktari," anasema Mlulu na kuongeza:


Anthony Juma

"Naamini Bima wakimlipa fedha zile, zinaweza kumsaidia hata kwa mlo wa siku kadhaa na kumpa ahueni mama yake kupumzika, lakini anaweza kuanzisha hata kitu cha ujasiriliamali."


**AJALI ZILIVYO**

Takwimu zinaonyesha bado ajali za barabarani ni tatizo nchini. Ripoti iliyotolewa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini mwaka jana, inaonyesha kati ya mwezi Januari na Februari kuna jumla ya ajali 769 zimeshatokea na kusababisha vifo 344, huku kukiwapo majeruhi 698.

Shirika la Afya Duniani (WHO), katika ripoti yake inasema hali ya usalama barabarani inaonyesha watu milioni 1.35 wanapoteza maisha kila mwaka kutokana na ajali hizo na kati yao watu kati ya milioni 20 hadi 50 wanaachwa na majeraha.

Vivyo hivyo, katika gharama zake, kila mwaka inachangia kuwapo hasara ya Dola za Marekani trilioni 1.8(Sh. Trilioni 4,140) kila mwaka na kusababisha kushuka kwa uchumi nchini.

Distributed via ippmedia





# Songwe kulisha magereza Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Gereza la Kilimo la Songwe lililoko mkoani Songwe, Peter Anatoly, ametangaza kuwa katika msimu wa kilimo wa 2019/2020 gereza hilo linakusudia kulima zaidi ya hekta 400 ambazo pamoja na kulisha wafungwa wake, huenda zikatosheleza kulisha magereza mengine kadhaa nchini.

Alisema hayo wakati wa kufunga mafunzo ya matumizi sahihi ya zana za kisasa za kilimo, yaliyokuwa yanatolewa kwa askari wa jeshi hilo hivi karibuni.

Anatoly, alisema hekta hizo 400 zilizoandaliwa ana hakika zikilimwa zitatosheleza mahitaji ya magereza yote ya mikoa ya Mbeya na Songwe na kwamba ikiwezekana hata magereza ya mikoa mingine nchini kulingana na maelekezo watakayopewa na viongozi wa kitaifa.

Aidha, katika hatua nyingine, serikali imeanza kulipa Jeshi la Magereza vifaa vya kilimo yakiwamo matrekta ili lianze kuzalisha chakula cha kulisha wafungwa na kuuza ziada ndani na nje ya nchi.

Hayo ni kwa mujibu wa Kamishna Msaidizi wa Magereza, Rock Mbena, aliyoyasema wakati alipokuwa anafunga mafunzo ya matumizi sahihi ya zana za kisasa za kilimo, yaliyokuwa yanatolewa kwa askari wa jeshi hilo.

Alisema uwezeshaji huo ni sehemu ya kulisaidia jeshi kutekeleza kwa vitendo agizo la Rais John Magufuli la kulitaka jeshi hilo, kujitosheleza kwa chakula cha kulisha wafungwa badala ya kutegemea serikali, wakati taasisi hizo zinaweza kuwatumia wafungwa kuzalisha.

Mbena ambaye ndiye msimamizi wa uzalishaji alisema kutokana na kupatiwa mitambo hiyo, jeshi hilo litakuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha na hivyo kujitosheleza kwa chakula na ziada kuuzwa kwa ajili ya kuendelea kuboresha kilimo na uwekezaji.

Alisema wanakusudia kuhakikisha magereza yanakuwa na mahindi, unga wa kutosha, maharage, mboga za majani na nyama na kwamba mitambo waliyopewa ni mipya hivyo itafanyakazi kwa muda mrefu.

"Katika mwaka huu wa fedha, serikali imetuwezesha kununua matrekta mapya 16 ambayo ni miongoni mwa zana askari wetu walizokuwa wanafundishwa kuzitumia na tunaamini tutaongeza uzalishaji," alisema Mbena.

Mhandizi wa Mitambo ya Kilimo wa Jeshi la Magereza, Johanes Baitange, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwaelimisha askari matumizi sahihi ya mashine hizo ambazo baadhi hawajawahi kuzitumia ili wasiiharibu.

Alisema vilevile mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha askari kuitumia huku wakizingatia usalama na kulinda maisha yao.

"Miongoni mwa mambo tunayowasisitiza ni pamoja na kuhakikisha mtu ambaye si mhusika hapandi trekta hilo, lakini pia trekta ni sawa na vyombo vingine vya moto hivyo lazima dereva azingatie sheria zote za udereva," alisema Baitange.



Mratibu wa Kilimo na Mifugo kutoka Jeshi la Magereza nchini, Rock Mbena (kushoto), akiwa na Mhandisi wa Kilimo wa Jeshi hilo, Mkoa wa Mbeya, Jonas Baitange (wa pili kushoto), na maofisa wengine, wakikagua mashamba ya mahindi katika Gereza la Kilimo Songwe juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wadau wasaidia watoto wahitaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO wahitaji na wanaoishi katika mazingira magumu wanaosoma katika Shule ya Msingi Iduda ya jijini Mbeya, wametakiwa kusoma bila hofu kwa kuwa jamii iko pamoja nao.

Aidha, pamoja na ahadi hiyo, watoto hao wamekabidhiwa msaada wa daftari na kalamu na asasi ya kiraia ya Elimisha kwenye hafla iliyofanyika katika Ofisi ya Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Juu, na kwa wale ambao hawakuwapo ikakabidhiwa kwa mmoja wa walimu wa shule hiyo ili awapatie watakapofika shuleni hapo.

Mkurugenzi wa Elimisha, Festo Sikagonamo, alisema lengo la kutoa misaada hiyo ni kuwawezesha watoto hao kusoma bila kuwa na vikwazo vya kukosa vifaa hivyo muhimu.

Alisema vifaa ambavyo walioona ni muhimu wanafunzi wawe navyo ni pamoja daftari na kalamu na kila mtoto anapewa daftari nane na kalamu nane.

Alisema shirika lake linafanya shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kusaidia jamii kupanga bajeti kuanzia ngazi ya familia, kutoa elimu kwa wanawake na vijana pamoja na kuelimisha jamii kuhusu masuala ya mazingira.

"Sisi huku ni wageni, hivyo ni vigumu kujua mtoto gani anaishi katika mazingira magumu na nani ni yatima, kwahiyo tuliwatumia viongozi wa mtaa watusaidie kuwabaini maana wao ndiyo wanaoishi nao, tunaamini vifaa vitu hivi vitawasaidia walezi wao kupunguza bajeti angalau kwa mwaka mmoja," alisema Sikagonamo.

Alisema katika Ofisi ya Mtendaji wa Mtaa ilichangia Sh. 200,000 ambazo zinahitajika kwa ajili ya ukarabati wa ofisi hasa kuweka madirisha.

Mwenyekiti mstaafu wa Mtaa wa Juu, Mwalizi Sawasawa ambaye alishiriki kuwatambua watoto hao, alisema walikuwa wanaangalia wale ambao hawana wazazi ama wanaishi na mzazi mmoja ambaye hajiwezi.

"Sio kila anayetoa ni tajiri bali wengine ni moyo tu wa huruma, kuna watu ambao ni matajiri kuliko hata nyie mliotuletea msaada kwa watoto wetu, lakini hawajawahi kulete misaada kama hii, tunaomba mwendelee na moyo huo," alisema Sawasawa.

Kwa upande wake mmoja wa walimu wa Shule ya Msingi Iduda, Frank Mkeya, ambaye alikuwapo kwenye tukio hilo alisema watoto yatima wanakabiliwa na matatizo mengi ambayo wakati mwingine yanawafanya wasihudhurie shuleni.

Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Juu, Grace Msemwa, aliwaomba watu wengine wenye uwezo kuwakumbuka watoto yatima kwa kuwasaidia kutimiza ndoto zao za elimu.

# Wajasiriamali watakiwa kuakisi walichofunzwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA wanaopata mafunzo ya ujasiriamali kutoka kwenye taasisi mbalimbali mkoani Mbeya wametakiwa kuzingatia wanachofundishwa na kutumia elimu wanayopata kujiajiri badala ya kusubiri ajira rasmi.

Ofisa Biashara wa Mkoa wa Mbeya, Stanley Kibakaya, alisema hayo wakati wa kikao cha kutathmini mafunzo kwa vijana kilichoitishwa na asasi ya kiraia ya 'Saidia Wahitaji SHOP' inayotoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana kwa kushirikiana na The Foundation for Civil Society. Alisema lengo la mafunzo ni kuhakikisha vijana hao wananufaika na rasilimali mbalimbali ndani ya maeneo yao na nchini kwa ujumla na kuwaepushia tabia ya kukaa vijiweni wakisubili kuajiriwa.

Kibakaya alisema vijana hao wakizingatia elimu hiyo wanaweza kujiongezea kipato kwa kuanzisha biashara mbalimbali ambazo zitakuwa na tija kwao na kwa serikali kwa madai kuwa zitasaidia kupunguza tatizo la ajira na kuiongezea serikali kiwango cha ukusanyaji wa mapato.

"Kuna vijana wengi ambao wanakaa vijiweni wakisema hakuna ajira, ni kweli hawataziona na wataendelea kulalamika kila siku, hivyo kila kijana aliyepata fursa ya elimu hii ni lazima aitumie kubadilisha maisha yake na ya wengine," alisema Kibakaya.

Ofisa Vijana wa Jiji la Mbeya, Baraka Mlonga, alisema vijana waliopata elimu hiyo kutoka SHOP wanatakiwa kuwa mabalozi kwa jamii kwa kutoa elimu ya kujitambua na kuibua fursa zilizopo ndani ya maeneo yao.

Alisema baadhi ya vijana kutoka katika jiji hilo ambao tayari wameshapata mafunzo, wameanzisha biashara na wengine wameanza kuunda vikundi ili wakope mikopo ya halmashauri na kufanya shughuli zao. "Vijana sasa hivi ni miongoni mwa makundi ambayo serikali inayaangalia kwa makini, kuna mikopo pale halmashauri, lakini vikundi havipo, hebu undeni vikundi mvisajili tutawasaidia kupata mikopo hiyo," alisema Mlonga.

Mratibu wa Shirika la Shop, Maria Dominick, alisema katika utekelezaji wa mradi huo walikumbana na changamoto ikiwamo uelewa mdogo kuhusu masuala ya ujasiriamali na wengine kuishi kwenye mazingira ambayo sio rafiki.

Vilevile alisema kuna tatizo la vijana kushindwa kurasimisha biashara kutokana na baadhi ya sheria zilizopo kuwa ngumu pamoja na vijana kukosa maeneo ya kufanyia shughuli zao.

Maria alisema ili kuepukana na changamoto hizo Halmashauri ya Jiji la Mbeya inatakiwa kuwatafutia maeneo kwa ajili ya kufanyia shughuli na kuwawezesha kupata nembo ya ubora kutoka TBS.





# Sababu kuajiri wataalamu wa nje zatajwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) imetaja sababu ya waajiri kuajiri wataalamu kutoka nje ya nchi kuwa ni kutokana na kukosekana kwa nguvu kazi yenye ujuzi wa kutosha nchini.

Maeneo sita yenye uhitaji wa nguvu kazi hiyo ni pamoja na sekta za ujenzi, teknolojia ya habari na mawasiliano (Tehama), kilimo, mifugo, utalii na nishati.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, alisema hayo juzi katika kikao kilichowakutanisha kati yao na Baraza la Ujenzi na Tehama na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Ujuzi kupitia mradi wa kukuza stadi za kazi na ujuzi (ESPJ).

TPSF kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza kipengele kimoja cha mradi huo wa ESPJ.

Simbeye alisema kwa miaka mingi waajiri nchini wamekuwa wakipata changamoto kubwa ya rasilimali watu wenye ujuzi unaohitajika katika kutekeleza majukumu yao.

"Changamoto hii imekuwa ikisababisha kuongezeka kwa gharama za uendeshaji wa biashara, waajiri kulazimika kutafuta wataalamu wenye ujuzi stahiki kutoka nje ya nchi au kutumia fedha nyingi katika kugharamia mafunzo kwa watumishi katika sehemu za kazi," alisema.

Kutokana na hali hiyo, Simbeye alisema mradi huo ni muhimu kwa sekta binafsi na watatekeleza kwa ufanisi mkubwa kwa maslahi mapana ya waajiri na taifa.

"Katika kutatua changamoto hii, TPSF tumeanzisha mabaraza sita ambayo ni ya ujenzi, Tehama, kilimo, mifugo, utalii na nishati ili kuwakutanisha wadau muhimu wanaohusika katika mnyororo mzima wa kukuza ujuzi nchini," alisema.

Aidha, alisema kuna changamoto ya kutokuwa na takwimu sahihi (database) ya ujuzi wanaojua vijana wanaohitimu vyuo, kutokuwa na usimamizi mzuri wa ubora wa vyuo vinavyotoa mafunzo, ufuatiliaji wa vijana wanaomaliza vyuo ili kutambua wameajiriwa wapi na urasimishwaji wa vyeti.

"Hizi changamoto zikitatuliwa wajuzi watapatikana hapa nchini bila kutegemea nje ya nchi kama ilivyo sasa, licha ya mradi wa mabaraza haya kumalizika mwaka 2021 tutahakikisha unakuwa endelevu, sisi tunamini kuwa bila ujuzi hatuwezi kuendelea."

"Hata kama hizo barabara tunazojenga na miradi mingine tunayotekeleza tunahitaji ujuzi, unaweza kuwajengea watu kumbe hawajui hata kutumia vifaa ndiyo maana hata juzi Rais John Magufuli alipokuwa anapokea ndege alisema hivi vitu tuvitumie vizuri, hivyo lazima tuwe na watu wenye ujuzi," alisisitiza.

Mkurugenzi huyo alisema suala la ujuzi utekelezaji wake unafanyika kwa mazoea kutokana na kutokuwa na sera itakayosaidia kutekeleza mradi huo kwa ufanisi na kuiomba serikali kuweka sera hiyo.

Naye Mshauri Mwelekezi kutoka TPSF, Nicholas Mbwanji, alisema nchi zinazoendelea, ikiwamo Tanzania, kama zinataka kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 lazima kuongeza idadi ya nguvu kazi yenye ujuzi.

"Kwa takwimu za Wizara ya Elimu mwaka 2012 inaonyesha kwamba katika mwaka 2011/12 uwiano ulikuwa mtaalamu mmoja, fundi 0.9 na ufundi stadi 0.7," alisema.


Distributed via ippmedia

Kinamama wachuuzi wa mananasi wakisaka wateja, katika Mtaa wa Uhindini, jijini Dodoma jana. **PICHA PETER MKWAVILA**

## AfDB yashauri ulinzi barabara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), imeishauri serikali kuweka mipango ya kuanzisha wakala utakaojihusisha na usalama barabarani ili kulinda mazingira ya barabara yanayotengenezwa.

Hayo yalibainishwa na Mwakilishi wa Benki hiyo, Dk. Alex Mubiru, katika uzinduzi wa ujenzi wa barabara ya mzunguko ya njia nne yenye urefu wa kilomita 112.3 jijini Dodoma.

Dk. Mubiru alisema hatua hiyo itasaidia kulinda mazingira ambayo yako pembezoni mwa barabarani hususani miti na taa za barabarani.

"Nawashauri mwanzishe wakala wa usalama barabarani lengo ni kuhakikisha mazingira yaliyoko pembezoni mwa barabara yanaimarika badala ya kuharibiwa na jamii inayozunguka," alisema.

Mwakilishi huyo alisema benki hiyo imetenga Dola za Marekani bilioni 7.5 kwa ajili ya kuboresha mazingira ya barabara ikiwamo upandaji miti na uwekaji wa taa za barabarani.

Alisema miti hiyo itakayopandwa na taa zitakazofungwa kwenye barabara hizo zinazotarajia kujengwa zinahitaji kutunzwa.

Naye Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema serikali ya awamu ya tano kwa mradi huo ambao pia umesaidia kujengwa kwa vituo vya afya katika baadhi ya vijiji na kuchimba visima vya maji.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Isack Kamwelwe, alipongeza benki hiyo imetoa fedha hadi hivi sasa kwa miradi 1,655 yenye thamani ya Sh. trilioni 2.548.

Alisema serikali imejipanga kuhakikisha mradi huo wa barabara unajengwa kwa kiwango cha juu.

# Ukaguzi wa dawa sasa kufanyika kila robo mwaka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI inatarajia kuanza ukaguzi wa dawa kwa kila robo ya mwaka kwenye mikoa ili kukomesha ubadhirifu wa dawa zinazotolewa na serikali kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya.

Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) anayeshughulikia Afya, Dk. Doroth Gwajima, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wafamasia katika kikao kazi cha wataalamu hao jijini hapa. Alisema wafamasia wanatakiwa kutumia mfumo wa ugavi wa dawa (elmis) ambao taarifa zote zinaingizwa na kutumika kama muhtadha wa kuombea dawa kwa kila robo. Dk. Gwajima alisema mfamasia wa mkoa atakuwa na wajibu wa kuhalalisha maombi ya dawa kwenda Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kila mara na mikoa itakayoanza kazi hiyo ni Singida, Dodoma, Manyara, Kagera na Geita.

"Tunataka kufanyika kwa 'medicine audit' (ukaguzi wa dawa) kila robo mwaka na taarifa yake kwa kila mkoa iwasilishwe Tamisemi. Lengo ni kuchakata taarifa za mifumo ya dawa ili kubaini kama kuna hazina ya dawa za kutosha au lah ili kusaidia maeneo ambayo yana upungufu wa dawa na kudhibiti ubadhirifu wa dawa," alisema.

Alibainisha kuwa Rais John Magufuli ametekeleza vyema ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuijali na kuipa kipaumbele sekta ya afya. Katika kufanya hivyo, alisema kwa mwaka wa fedha wa 2019/20, serikali imepitisha bajeti ya Sh. bilioni 57.4 na katika mgawanyo, eneo la dawa ni miongoni mwa vipaumbele vitatu vilivyopewa umuhimu.

Aidha, alisema serikali iko katika mpango wa kuboresha mfumo wa uendeshaji wa shughuli za Afya (GoTHOMIS) ambao baada ya kukamilika kwake, utatoa taarifa nyingi za makusanyo ya fedha za dawa mpaka ngazi ya mtumiaji wa mwisho. Awali, Mkurugenzi wa Idara ya Afya na Ustawi wa Jamii wa ofisi hiyo, Dk. Ntuli Kapologwe, alisema afya imekuwa miongoni mwa sekta zilizopewa kipaumbele na Rais, hivyo wataalamu lazima waonyeshe kwa vitendo kuwa Rais hajakosea kwenye hilo.

Alisema kikao hicho kinalenga kuweka mipango ya kuhakikisha mianya ya ubadhirifu wa dawa inakomeshwa na kuweka mikakati endelevu ya upatikanaji wa dawa.





Wafanyausafi wakijipanga kuanza kazi katika eneo la Namanga Msasani, jijiji Dar es Salaama jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali kunufaika vitambulisho vipya

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema matumizi ya vitambulisho vipya vya Mzanzibari Mkazi 'smart card' yatawezesha kuhifadhi kumbukumbu za matukio ya watu na taarifa zao kwenye Daftari la Usajili na Utambuzi.

Rais Shein alisema hayo wakati wa uzinduzi wa kadi mpya za kielektroniki ya kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi.

Uzinduzi huo ulifanyika katika ukumbi wa Sheikh Idrisa Abdul Wakil Kikwajuni Mjini Zanzibar.

Alisema matumizi ya vitambulisho hivyo yataiwezesha serikali, taasisi za umma na za watu binafsi kupanga vipaumbele vya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazohusiana na huduma na maendeleo ya kijamii.

Alisema kuwapo kwa mfumo huo wa matumizi ya vitambulisho vipya kutaiwezesha serikali kuwatambua watu wanaostahili kupata haki za msingi, kama ilivyobainishwa katika Katiba ya Zanzibar ya 1984.

Dokta Shein alisema ujio wa vitambulisho hivyo utairahisishia serikali kazi ya ukusanyaji wa mapato hivyo kuimarisha huduma muhimu za kijamii, ikiwamo afya, elimu, barabara pamoja na ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Vile vile alieleza kuwa vitambulisho hivyo vimetengenezwa kwa teknolojia ambayo siyo rahisi kughushiwa, vikiwa na uwezo mkubwa wa kiusalama wa taarifa za mtumiaji na hutumika katika nchi kadhaa duniani.

Aidha, aliwataka wakuu wa mikoa kusimamia vizuri taarifa za uhakiki wa watu walioko katika maeneo yao, kuanzia ngazi za shehia, wadi na wilaya ili kuwatambua wananchi wao na taarifa zao zilizo sahihi.

Mapema, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Haji Omar Kheir, aliwataka wananchi wenye sifa za kisheria kufika katika vituo vya usajili vilivyopo kila wilaya nchini.

Alisema vitambulisho vipya vya Mzanzibari Mkaazi ndicho kitakachotumika katika upatikanaji wa huduma mbalimbali muhimu kama vile kupati leseni, miamala ya fedha, mahitaji katika taasisi za umma pamoja na zile zenye kutaka kuwasilisha vitambulisho.

Aidha, alisema wizara itaendelea kusimamia utoaji wa elimu kwa wananchi ili kutii sheria ya ukaazi na kupata fursa mbalimbali ziliopo nchini.

Akizungumza kwenye uzinduzi, Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Usajili na Matukio ya Kijamii Zanzibar, Dk. Hussein Khamis Shaaban, alisema ofisi hiyo itaendelea na mikakati ya kusajili na kuwapatia vitambulisho wananchi wenye sifa za kupata huduma hiyo kisheria.

Alisema mfumo wa vitambulisho vya kielektroniki ni ufunguo katika kufikia maendeleo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa pamoja na kudumisha ulinzi na usalama wa taifa.

Aidha, alisema Zanzibar inakabiliwa na changamoto kubwa ya uingiaji wa wageni kutoka nje, hivyo kuwapo kwa vitambulisho hivyo ni muhimu kwani kutawezesha kuwatambuwa wageni hao.

Katika hafla Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Haji Omar Kheri, alimkabidhi Dk. Shein kitambulisho kipya cha Mzanzibari Mkaazi.

Aidha, aliwakabidhi viongozi mbalimbali wa serikali, akiwamo Mama Mwanamwema Shein mke wa Rais, pamoja na watu wengine kadhaa.

# Halmashauri yatamba kufanya makubwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kaskazini A imeeleza kuwa na mafanikio makubwa kwenye kuimarisha sekta afya, elimu, kilimo na uvuvi na kutimiza lengo la serikali la kutoa huduma bora kwa wananchi.

Akizungumza katika kikao cha kujadili na kutathmini sekta hizo huko Mkokotoni mhasibu msaidizi wa halmashauri hiyo Haji Haji, alisema.

Alieleza kuwa katika utekelezaji wa mpango wa kuimarisha sekta hizo halmashauri imetumia zaidi ya Sh. milioni 100 kwa ajili ya kuanzisha kambi ya wanafunzi wa darasa la sita ili kujiandaa na mitihani yao.

Alisema uendeshaji wa shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi, kuhamasisha wananchi kujikinga na magonjwa kama surua pamoja na kuboresha afya za wananchi kwa kufuatilia na kuwaepusha na maradhi ya mlipuko katika maeneo hatarishi ni baadhi ya juhudi zilizofanywa ili kuwa na afya na jamii bora.

Akiwasilisha taarifa ya miradi inayoendelea kutekelezwa katika sekta hizo Mhandisi wa Halmashauri hiyo, Khamis Nassor Khamis, alisema kazi zinaendelea na utekelezaji baadhi ya mambo ni pamoja na ujenzi wa vyoo katika Shule ya Msingi Moga, ukarabati kituo cha afya Donge na Mchangani.

Nyingine ni ujenzi wa mnara na usambazaji maji kwenye shule ya msingi na sekondari ya Gomani na kupeleka umeme Shule ya Mlilile.

Akichangia ripoti ya sekta hizo Diwani wa Wadi ya Gamba, Machano Fadhil Babla, aliomba kuwapo kwa mshauri elekezi wa miradi ya maendeleo ya halmashauri hiyo na siyo kuchukua mshauri kutoka nje ili kupunguza gharama na matumizi ya fedha kiholela.

Kikao hicho cha siku mbili kimepitisha matumizi ya sekta zilizofanyiwa ugatuzi kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba mwaka huu.

# SMZ yawahakikishia wawekezaji ushirikiano

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ina nia ya kuendelea kuwakaribisha wawekezaji wa taasisi na kampuni za ndani na za nje ili kuimarisha uchumi, kuleta maendeleo na kuongeza pato la taifa.

Hayo yalielezwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, wakati akibadilisha mawazo na ujumbe wa viongozi wa kampuni za simu za Tigo na Zantel, uliomtembelea ofisini kwake hivi karibuni.

Ujumbe huo ulioongozwa na Makamu wa Rais wa Uhusiano wa Kampuni ya Kimataifa ya Millicom Group kutoka Miami Marekani Rachel Samren.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kushirikiana na mashirika ya uwekezaji ya ndani na nje ili kuimarisha uchumi.

Aidha, Balozi Iddi, aliuhakikishia ujumbe huo wa Kampuni ya Millcom Group kwamba Serikali ya Zanzibar itaendelea kutoa kila aina ya msaada ili azma ya uwekezaji ifanikiwe.

Makamu wa Rais wa Mahusiano wa Kampuni ya Kimataifa ya Millicom Group, Rachel Samren, alisema taasisi hiyo itaendelea kushirikiana na Zanzibar kutoa huduma za mawasiliano na kuzifikisha kwa wananchi wengi.

Alisema taasisi hiyo inayosimamia huduma za mawasiliano ya kampuni za mitandao ya simu za mkononi za Zantel na Tigo imejipanga kitaalamu kuhakikisha kwamba kila mwanajamii anayetumia mawasiliano ya kampuni hizo anaridhika na huduma zinazotolewa.

Alisema Millicom Group kwa sasa imefikia hatua kubwa kwa kuungwa mkono kwake na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwamba ushirikiano umefikia asilimia 99.5.

# Taasisi zilizolipa malipo hewa korosho kikaangoni

**Na Futuna Seleman,**
MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ameagiza vyombo vya dola kuhakikisha vinazihoji taasisi za fedha zilizojihusisha na ulipaji wa malipo hewa ya fedha za wakulima wa korosho ili zirejeshwe mikononi mwa serikali.

Ametaka ushirikiano upatikane ili ijulikane fedha hizo zimelipwa kwa kina nani kwa vile taasisi zilizotajwa ndizo zinazojua wakulima ambao walilipwa wakati hawakustahili kulipwa, huku wengine wakilipwa zaidi na waliostahili kulipwa hawajalipwa.

Aliyasema hayo katika mkutano wa wadau wa korosho uliowajumuisha pia wakulima wa korosho mkoani Pwani.

Mkutano huo pia ulihudhuriwa na Wenyeviti wa Halmashauri zote mkoani Pwani, wakuu wa wilaya, Bodi ya Korosho, wasafirishaji wa zao hilo na wadau wanaojishughulisha na kusimamia zao hilo.

"Taasisi za fedha zilizohusika wakae tayari kutoa ushirikiano kwa vyombo vya dola ili ukweli upatikane...haisaidii kukataa kutoa ushirikiano, haiwezekani jina liandikwe Ndikilo wakati akaunti benki imemlipa mkulima Njwayo," alisema na kuhoji:

"Umakini uko wapi, mimi najua jina likitofautiana na akaunti haiwezi kulipwa... iweje taasisi ya fedha ijiridhishe akaunti si ya mhusika jina si lake hafu walipe fedha?" "Kumetokea udanganyifu mkubwa katika ulipwaji wa fedha hizo ikiwamo baadhi ya wakulima kulipwa mara mbili na wasiostahili kulipwa wamelipwa. Kuna wengine hawana shamba la korosho kwenye AMCOS (vyama vya msingi), hawapo majina yao yanaonekana, wakulima wengine hawana mashamba si wanachama kwenye chama cha msingi, lakini amelipwa fedha hivyo, lazima warudishe fedha," alisema na kuongeza:

"Vyombo vya dola Jeshi la Polisi, Takukuru, watafanya kazi hizo wote watakaothibitika kufanya wizi na ubadhirifu wa fedha za serikali zitarudishwa na wasiolipwa utaratibu utafanyika ili walipe." Alisema hadi sasa Sh. bilioni 18.1 ndizo ambazo serikali inadaiwa na wakulima wa korosho mkoani Pwani.

Alisisitiza Tume ya Uhakiki ikamilisha kazi yake ya uhakiki, wakulima watalipwa, na kuwa AMCOS zitakazohusika na ubadhirifu, lazima watawajibika kisheria ikiwamo kulipa fedha wanazodaiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, GullamHussein Kiffu, alisema changamoto iliyojitokeza wilayani kwake ni wakulima kulipwa mara mbili, na kuwa wakulima 42 walilipwa mara mbili na kusababisha hasara ya zaidi ya Sh. milioni 100, hivyo majina kufutwa na wino mweupe.

Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Juma Njwayo, alisema changamoto za wakulima wa wilayani kwake nyingi zinafanana na za Kibiti na Mkuranga.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa hakukuwapo na ushirikiano katika malipo, na kwani walipojaribu kuhoji Bodi ya Korosho iliwazungusha, huku wakijibiwa malipo ni haki ya wakulima.



Mfanyabiashara wa magamba ya samaki akiyatandaza ili kuyakausha na jua, katika eneo la Kamanga, jijini Mwanza jana. Gunia moja la magamba hayo, linauzwa kwa bei ya 15,000/-. **PICHA ELIZABETH FAUSTINE**

# Waandishi wa habari Afrika wapewa neno

**Na Mwandishi Wetu,**
JOHANNESBURG

WAANDISHI wa habari Afrika wamehimizwa kuandika kwa wingi na ubora habari zinazohusu bara hilo, ili kuweka kumbukumbu na marejeo bora kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Akitoa tamko hilo jana mbele ya mkutano wa siku tatu wa waandishi wa habari wa Afrika, wabobezi wa habari za uchunguzi jijini Johannesburg, Afrika Kusini, Rais wa Taasisi ya Waandishi wa Habari Tanzania (Tajoa), Simon Mkina, alisema baadhi ya waandishi katika bara hilo mara nyingi wamekuwa hawapendelei kuandika mambo mazuri yanayofanywa na nchi hizo. Alisema ni vema waandishi wa habari wakabadilika na kupendelea kuandika mambo mazuri ya kwao yanayohusu maendeleo, watu, mazingira na masuala mengine ya bara hilo kwa bidii zaidi.

Katika mkutano huo unaofanyika katika Chuo Kikuu cha Witwatersrand nchini humo, Mkina alisema wakati umefika sasa kwa waandishi hao kuunganisha nguvu ili kuwa na sauti ya pamoja kujenga taswira sahihi ya Afrika.

"Nguvu ninayohimiza hapa ni kuandika mazuri kuitetea Afrika, ili kuwaonyesha mazuri wale waliopo nje ya Afrika ambao wamezoea kuandika kwa kupotosha kwa kuandika mabaya ya Waafrika na tunaamini nao watabadilika tu, Afrika ni bora na inafanya mambo makubwa mazuri," alisema Mkina.

Mkina alisema hata kama yapo mabaya yanayofanywa na nchi hizo, lakini siyo mengi ya kuzidi yale yaliyo mazuri.

Alisema habari nyingi ambazo zimekuwa zikiandikwa na baadhi ya vyombo vya habari nje ya Afrika husussani zenye mlengo mbaya zimekuwa zikijumuisha bara lote la Afrika hata kama zinaihusu nchi moja.

"Hatuwezi kusema hakuna nchi katika Bara hilo la Afrika ambazo zinateleza, lakini kwa nini nchi moja ikifanya kosa linaunganishwa bara zima? Hili jambo siyo sahihi.

Mkina alitumia mkutano huo kukumbusha umuhimu wa vyombo vya habari katika kuchangia maendeleo ya Afrika na watu wake.

Alisema ifike wakati vyombo vya habari nje ya Afrika vimulike na mambo mazuri yanayofanyika katika nchi hizo.

"Tunaomba na yale mambo mazuri yamulikwe, tunaamini kwamba vyombo vya habari vina nguvu kubwa katika kuelimisha jamii, kwa hiyo ni vema kuhakikisha kwamba taarifa zinazoenda kwao ni sahihi," alisema Mkina.

# NEMC yajivunia taarifa za wananchi

**Na Enok Charles**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linajivunia ushirikiano linaoupata kutoka kwa wananchi, ikiwamo kupewa taarifa za uchafuzi wa mazingira na madhara ya kelele.

Hayo yalielezwa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alipokuwa akizungumza jijini Dar es Salaam.

Dk. Gwamaka alieleza kuwa juhudi ya baraza katika kuwaelimisha wananchi juu ya kulinda na kuhifadhi mazingira imekuwa ikizaa matunda na kutoa mfano wa elimu ambayo imetolewa na baraza kuhusu madhara ya kelele kutoka kwenye kumbi za starehe, magari ya matangazo na nyumba za ibada.

"Itakumbukwa kwamba mara kwa mara tumekuwa tukitoa elimu juu ya kulinda na kuhifadhi mazingira na nini kinasemwa na Sheria ya Mazingira na kanuni zake juu ya masuala mbali mbali," alisema na kuongeza:

"Hivi majuzi nikiwa Mbeya nilitoa taarifa kwa taifa juu ya suala la kelele kama chanzo cha uchafuzi wa mazingira. Nilieleza kwamba tayari tumepokea malalamiko rasmi 600 kutoka kwa wananchi. Jambo hili limetutia moyo sana sana. Tunajivunia ushirikiano tunaoupata."

Alieleza kwamba ushirikiano ambao baraza lao linaupata kutoka kwa wananchi ni dalili ya mambo makubwa mawili. Kwanza, ni dalili ya kwamba Watanzania ni taifa la watu wenye uelewa na pili ni dilili ya kwamba wananchi wanaunga mkono kazi zinazofanywa na baraza.

Alisema akiwa Mbeya alitoa mfano mmoja juu ya lalamiko la mtoto mchanga sana ambaye kapoteza uwezo wa kusikia kwa sababu ya kelele za kupindukia. Mtoto alipochunguzwa hospitalini, iligundulika kwamba kiungo cha sikio (cochlear) kimeharibiwa kutokana na kelele kubwa kupindukia.

Aliwataka wananchi waendelee kutoa taarifa rasmi kwa baraza juu ya kosa hilo na kuliahidi taifa kwamba baraza litachukua hatua za haraka kwa walalamikiwa baada ya uchunguzi.

Walalamikiwa wa kosa lililothibitika la kelele zinazochafua mazingira wanakabiliwa na faini ya kuanzia Sh. 200,000 hadi milioni moja. Walalamikiwa wakorofiwatapelekwa mahakamani.

Kwa mujibu wa Dk. Gwamaka, hakuna hoja ya aina yoyote itakayokubalika kama utetezi baada ya kuvunjwa kwa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake.

Amesema kuwa kelele za kupindukia ni siyo tu kwamba ni kero kwa wananchi, bali zina madhara ya kiafya kwa watu.

## Ghasia zapamba moto chuoni Makerere

**KAMPALA, Uganda**

JESHI la Polisi nchini Uganda limefyatua mabomu ya kutoa machozi kuwatawanya wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Makerere na waliokuwa wamekusanyika katika eneo la Freedom Square.

Wahadhiri wa Chuo hicho pia wametawanywa na wanafunzi wakalazimishwa kuondoka katika vyumba vya madarasa.

Ghasia hizi zimetokea siku moja tu baada ya Rais wa nchi hiyo, Yoweri Museveni, kuwaagiza wanajeshi kuondoka katika chuo hicho, baada ya ripoti kuwa waliwapiga wanafunzi katika chuo hicho

Picha za Televisheni ya NTV Uganda zilizotumwa kwenye mtandao wa kijamii wa twitter zilionesha Jeshi la Polisi la kutuliza ghasia wakiwasili katika chuo hicho.

Wanafunzi wa Chuo Kikuu hicho maarufu wamekuwa wakiandamana kupinga ongezeko la asilimia 15 ya karo iliyoidhinishwa na baraza la vyuo vikuu nchini Uganda tangu wiki iliyopita.

Rais Museveni aliwataka wadau wote katika Chuo Kikuu cha Makerere kufanya mazungumzo ili kutatua mzozo wowote uliopo kuhusu karo.

Utawala wa Chuo Kikuu na viongozi wa wanafunzi walikutana mwanzoni mwa wiki siku ya Jumatatu kujadili suala hilo, lakini wakashindwa kufikia makubaliano, jambo lililofanya mkutano wao kuahirishwa.

Uongozi wa vyuo vikuu nchini Uganda unadai kuwa nyongeza ya sasa ni ndogo ikilinganishwa na inayotozwa na vyuo vingine vikuu nchini humo.

Ghasia hizi zinatokea saa kadhaa tu baada ya bodi ya utawala ya chuo hicho, Baraza la vyuo vikuu kuahidi kuwa vimesitisha sera ya asilimia 15 ya karo kufuatia maandamano ya wanafunzi yaliyoanza wiki iliyopita.

Vyombo vya habari nchini humo vinasema kuwa tangu Jumanne, kumekuwa na ripoti za wanajeshi na Askari wa kutuliza ghasia kuingia ndani ya vyumba au makazi ya wanafunzi usiku na kuwapiga.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi limedai hueda maandamano hayo yana uchochezi wa kisiasa.

Wakati huo huo, Jeshi la polisi nchini Uganda inachunguza ripoti kuwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Makerere wanalipwa na wanasiasa na wanaharakati kufanya maandamano.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini Uganda, Fred Enanga alisema kuwa taarifa walizonazo ni kwamba malipo kwa wanafunzi hao yanatolewa kwa njia ya simu za mkononi, kwamba taarifa hiyo ni moja ya taarifa zinazochunguzwa kuwa chanzo kilichochochea maandamano katika chuo cha Makerere.

**BBC**

# Papa aruhusu wanaume walioa kuwa mapadri

**ROMA, Italia**

MAASKOFU wa Kanisa Katoliki wamepiga kura kuruhusu wanaume walioa kuwa mapadri ili kuweza kupata mwanya wa kuhubiri katika eneo la Amazon.

Hatua hiyo imekuja baada ya Papa Francis kutoa ombi kuwa ni vyema kutoa ruhusa kwa wanaume walioa kuwa mapadri kwenye sehemu maalumu katika eneo hilo la Amazon.

Amazon ni eneo ambalo waumini wengi wanaotaka kushiriki misa na kupokea mkate wa komunio hawajawahi kuwaona mapadri kwa zaidi ya miezi kadhaa na muda mwingine hata miaka.

Alisema yeye na washiriki wengine wanaojulikana kama 'synod' wapo wazi kwa mawazo ya kutafuta njia mpya itakayosaidia kusambaza imani hiyo.

Hivyo, watahitajika kupata wanaume wanaoheshimika na kulingana na stakabadhi hizo watafanya kazi katika jamii wanazotoka.

Maaskofu kutoka Marekani Kusini wamepigania juhudi hizo ili kukabiliana na upungufu wa mapadri katika eneo hilo.

Lakini wakosoaji wamedai kuwa Papa Francis anapaswa kuhamasisha mapadri wasioe, ingawaje katika karne ya kwanza ya kanisa, mapadri waliruhusiwa kuoa, na karibia mapapa wote wa mwanzo walikuwa wameoa.

Vilevile kuruhusu wanaume walioa katika sehemu za Amazon ambazo zinakabiliana na ukosefu wa mapadri, kutaenda kinyume na sheria za kikatoliki ambazo zimekuwapo kwa miaka kadhaa sasa.

Kwa sasa Papa Francis ameruhusu wanaume walioa kuwa mapadri katika makanisa ya mashariki ya kati pekee.

Upigaji kura ukiwa unafikia ukingoni huko mjini Vatican kutokana na uhaba wa mapadri ili mapendekezo hayo yaanze kufanya kazi rasmi. Wengi wakiwa wanahofia mabadiliko hayo katika kanisa kwa kuanzisha utaratibu mpya katika kanisa.

Kura zimechukuliwa kwa kipindi cha wiki tatu, kwa maaskofu 180 kutoka mjini Roma. Wakiwa wanaangalia majukumu ya wanawake katika kanisa na namna mazingira yatakavyoweza ruhusu.

Kanisa Katoliki ni taasisi kongwe ya kidini ambayo imekuwa na historia kwa zaidi ya miaka 2,000 iliyopita huku ikiwa na mabilioni ya waumini.

Huku inakadiriwa kuwa karibu asilimia 85 ya vijiji huko Amazon haviwezi kusherehekea Misa kila wiki kwa sababu ya uhaba wa mapadri na wengine huoana na makuhani mara moja tu kwa mwaka.

***BBC***


Distributed via ippmedia

Waziri wa Mambo ya Nje wa Ujerumani, Heiko Maas (kushoto) akiwa na Waziri wa Mambo ya Nje wa serikali ya Libya, Mohamed Siala. **PICHA: AFP**

# Mtoto wa miaka 12 adahiliwa chuo kikuu

**ACCRA, Ghana**

MTOTO wa miaka 12, Viemens Bamfo ameshinda nafasi ya kusoma Chuo Kikuu cha Ghana masomo ya utawala wa Umma.

Bamfo, ni mtoto mdogo zaidi kati ya wanafunzi 3,000 waliodahiliwa katika chuo kikuu cha Ghana.

Imeelezwa kuwa Bamfo alishinda mtihani wa majaribio kwa alama za juu baada ya kufundishwa na baba yake, Robert Bamfo nyumbani.

Alilieza Shirika la utangazaji la BBC kuwa anatamani kuwa na kazi ya juu kabisa nchini Ghana.

"Ninataka kuwa Rais wa Ghana, ninataka kupeperusha bendera ya Ghana na kuifanya Ghana kuwa nchi huru ya kweli kama ilivyo Marekani, Uingereza, China na nchi nyingine," alisema Bamfo.

Alieleza kuwa anamatumaini ya kusoma masomo ya Sheria ya Katiba, mifumo ya kisiasa, masuala ya uongozi, uchumi na utunza fedha.

Bamfo, ambaye ana shahada ya kwanza ya uhandisi wa kemikali, alisema mafanikio ya mtoto wake si jambo la kushtukiza.

"Nimewekeza muda na nguvu nyingi kumuwezesha kuweza kukabiliana na changamoto na fursa zinazoambatana nazo. Hivyo sikushtushwa,"alisema baba mzazi.

Alieleza siri ya mafanikio katika malezi ya mwanae: "Awali nilimfundisha mwanangu asikubali kutafsiriwa kuwa mtu wa wastani, na kuwa anapaswa kuwa wa tofauti kwa kuweka bidii na amejiandaa kupambana kufikia lengo hilo."

***BBC***

# Wanawake Dar wakumbwa na ugonjwa kiribatumbo

**Na Gwamaka Alipipi**

UTAFITI umeonyesha kuwa wanawake wengi walio kwenye umri wa kuzaa wanasumbuliwa na ugonjwa wa kiribatumbo (unene kupita kiasi), huku idadi kubwa wakiwa katika Jiji la Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Dar es Salaam kuhusu maandalizi ya mkutano wa mawaziri wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) wanaoshughulikia afya na ukimwi, Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Lishe wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Grace Moshi, alisema tatizo hilo limezidi kuongezeka na kufikia asilimia 31.9.

"Utafiti huu tuliufanya mwaka jana na ulihusu hali ya lishe nchini hususani uzito uliozidi au kiribatumbo na tukabaini kuwa tatizo limeendelea kuongezeka. Mpaka sasa kwa wanawake walio katika umri wa kuzaa tatizo hilo limezidi kuongezeka," alisema Dk. Moshi.

Alisema kwenye utafiti huo, walibaini kuwa mikoa inayoongoza na ambayo imezidi asilimia 20 Dar es Salaam na Kilimanjaro wakati kwa upande wa Zanzibar ni maeneo ya Stone Town na Unguja.

"Hali ya kiribatumbo hailidhishi nchini. Kadri miaka inavyozidi kwenda, ndivyo tatizo linazidi kuwa kubwa. Wanawake wengi sasa ambao wako katika umri wa kuzaa wana kiribatumbo au uzito uliozidi," alisema Moshi.

Alisema mwaka 2014 tatizo hilo kwa wanawake ilikuwa asilimia 29.7 wakati mwaka 1991 ilikuwa asilimia 11.3.

**CHANZO CHAELEZWA**

Dk. Moshi alisema chanzo kikubwa kinachosababisha kiribatumbo ni mtu kula chakula kingi kuliko uwezo wake hususani vyakula vilivyo katika kundi la wanga pamoja na mafuta kwa wingi.

Alisema chanzo kingine ni utandawazi kwa sababu wetu wengi hivi sasa wamebadilisha hali zao za maisha, namna ya kuishi, shughuli zao.

Kwa mujibu wa Dk. Moshi, sababu nyingine ni watu kupendelea kula vyakula vilivyokaangwa hasa wakazi wa maeneo ya mjini kupendelea kula chipsi mayai.

Moshi alisema kwenye mkutano wa mawaziri wa afya na ukimwi wa SADC unaotarajiwa kuanza Novemba 4 hadi 8, mwaka huu, wataangalia tatizo la kiribatumbo kwa watoto.

"Utafiti unaonyesha kuwa mtoto akiwa na kiribatumbo wakati wa utoto anaweza kupata uzito uliozidi wakati wa utu uzima. Hivyo kwenye nchi za SADC tunaangalia hilo ili watoto wawe na uzito unaohitajika, wasiwe na uzito uliopitiliza," alisema Dk. Moshi.

Alisema kuna nchi za SADC zimeonekana kuwa na watoto wenye uzito uliopitiliza au kiribatumbo kama vile Afrika kusini.


Distributed via ippmedia

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Adelardus Kilangi, akizungumza wakati wa kufungua kikao kazi cha wakurugenzi wa sheria, wakuu wa vitengo vya huduma za kisheria kutoka Wizara, Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wakala na Taasisi mbalimbali za Serikali, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ahukumiwa kulipa fidia ya bil. 1/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemwamuru mwanasiasa, Salma Mntambo, kulipa fidia ya Sh. bilioni 1.004 baada ya kumaliza kifungo cha miaka 99 dhidi ya makosa 17 yaliyokuwa yakimkabili, ikiwamo kuwasilisha nyaraka za uongo na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Septemba 18, mwaka huu mahakama hiyo ilimtia hatiani Mtambo na kumhukumu kwenda jela kutumikia kifungo hicho na mahakama imetoa amri ya kumlipa mlalamikaji fidia.

Amri hiyo ilitolewa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Mfawidhi, Kelvin Mhina.

Alisema mahakama yake ilimtia hatiani mshtakiwa kwa makosa matatu ya kutoa hati za uongo na 14 ya kujipatia Sh.1,027,000,000 kati ya mashtaka 24 yaliyokuwa yakimkabili.

"Hasara aliyoisababisha mshtakiwa haiwezi kupita hivi hivi kwa mlalamikaji, kwa sababu alikuwa anafanya biashara ya kununua viwanja, kujenga na kuuza nyumba kwa hiyo imevuruga biashara ya mlalamikaji huyo, mshtakiwa atalipa fidia ya Sh. bilioni 1.004," alisema Hakimu Mhina.

Akimsomea hukumu Septemba 18, mwaka huu, Hakimu alisema mahakama yake baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi watano wa upande wa Jamhuri bila kuacha shaka wamethibitisha makosa 17 kati ya mashtaka 24 yaliyokuwa yanamkabili.

"Pia mahakama hii inakutia hatiani kwa makosa 14 ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, hivyo mshtakiwa utakwenda jela kutumikia kifungo cha miaka sita kwa kila kosa," alisema Hakimu Mhina wakati akimsomea hukumu hiyo.

# Mhasibu OUT ahukumiwa kulipa faini ya mil. 700/-

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemuhukumu aliyekuwa mhasibu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Engels Mrikaria kutumikia kifungo cha miaka mitano jela au kulipa faini ya Sh. milioni 700, baada ya kupatikana na hatia katika makosa ya kughushi na utakatishaji fedha.

Kadhalika, mahakama imemhukumu mshtakiwa huyo kulipa fidia ya Sh. milioni 700 alizosababisha hasara kwa chuo hicho pamoja na kutaifisha ardhi anayoimiliki iliyopo Mkoa wa Morogoro.

Hukumu hiyo ilisomwa na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Agustine Rwizile, pia, imewaachia huru Lucy Mrikaria, Boniface Msofe, Stanley Msofe na Rose Maungu baada ya upande wa mashtaka kushindwa kuthibitisha mashtaka dhidi yao.

Hakimu alisema upande wa Jamhuri ulileta mashahidi 35 pamoja na vielelezo 48, na kwamba bila kuacha shaka wamethibitisha mashtaka dhidi ya Mrikaria ambaye alikuwa analipa mshahara kwa wafanyakazi wa chuo hicho.

Alisema mshtakiwa amekutwa na hatia katika mashtaka 53 ya kughushi, saba ya utakatishaji fedha na moja la kuisababishia chuo hicho hasara ya Sh. 566,446,500.

Hakimu Rwizile alisema katika mashtaka ya kwanza hadi ya 53, mahakama inamwachia huru mshtakiwa huyo kwa sababu amekaa rumande kwa miaka saba na kwa mujibu wa sheria, mashtaka ya kughushi kifungo cha juu ni miaka saba.

Pia alisema katika mashtaka ya utakatishaji fedha kila moja atatakiwa kulipa faini ya Sh. milioni 100 au kutumikia kifungo cha miaka mitano jela.

Alisema adhabu za vifungo vitakwenda sambamba, pia mahakama inataifisha ardhi iliyopo mkoani Morogoro na kuhusu kiwanja kilichopo Arumeru mkoani Arusha kwa sababu bado haijajulikana kama kiliingia mikononi mwa mshtakiwa au la.

Alisema endapo Jamhuri itataka mali hiyo kutaifishwa, ipeleke maombi ikiwamo kuorodhesha mali zote inazotaka zitaifishwe.

Mrikaria anadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Julai 2009 na Aprili 2011 ambapo alighushi nyaraka ya malipo ya mshahara na kuwatumia fedha watu mbalimbali kupitia akaunti za CRDB na NBC ambao hawakuwa wafanyakazi wa OUT.

Inadaiwa kati ya Julai 15 na 31, 2009 Makao Makuu ya OUT, jijini Dar es Salaam, alighushi nyaraka ya malipo ya mshahara lengo kuonyesha S. M January alilipwa mshahara wa Sh. milioni mbili, B. J Msoffe (1,983,000) na A. Mrakari (1,603,000) wakati akijua sio wafanyakazi wa chuo hicho.

Katika mashtaka ya utakatishaji fedha, inadaiwa Julai 2009 na Aprili, Mrikaria na Lucy Mrikaria, walijipatia Sh. 28,776,750 zilizoingia kwenye akaunti ya familia kama mshahara.

Pia inadaiwa mshtakiwa aliingiza fedha kwenye akaunti ya Kampuni ya Kyungu Hill kama mshahara.

Inadaiwa Aprili, 2011, maeneo ya Dar es Salaam na Dodoma, alijipatia shamba la ekari 130 katika Kijiji cha Muungano kilichopo Kongwa, fedha ambazo zililipwa na chuo hicho kama mshahara kupitia akaunti zake.

Mshtakiwa pia ilidaiwa alinunua kiwanja Kijiji cha Kiharaka Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani na vilevile alinunua kiwanja kilichopo Kijiji cha Meru wilayani Arumeru mkoani Arusha.

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

Amana Bank
*Pamoja, katika njia sahihi*

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2019**

| | SHS '000 Robo Mwaka 30 - 09 - 2019 | SHS '000 Robo Mwaka 30 - 06 - 2019 |
|---|---|---|
| **A. MALI** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 10,361,063 | 12,523,126 |
| 2. Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 20,095,694 | 16,954,196 |
| 3. Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 0 | 0 |
| 4. Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 6,469,307 | 9,011,201 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 250,603 | 65,720 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 22,647,774 | 18,433,268 |
| 10. Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 158,723,070 | 155,176,095 |
| 12. Mali Nyingine | 7,064,427 | 8,438,590 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14. Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 14,148,024 | 12,834,233 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **239,759,962** | **233,436,429** |
| | 0 | |
| **B. DHIMA** | 0 | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 7,707,792 | 2,072,250 |
| 18. Amana za Wateja | 177,914,576 | 183,032,145 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20. Amana Maalumu | 14,424,817 | 10,838,837 |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 110,372 | 124,687 |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 198,125 | 121,045 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 52,691 | 167,087 |
| 27. Dhima Nyingine | 12,155,138 | 10,906,868 |
| 28. Madeni | 0 | 0 |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | 212,563,511 | 207,262,919 |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **27,196,451** | **26,173,510** |
| | | |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 39,697,089 | 39,697,089 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 8,036,457 | 7,520,195 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (21,340,885) | (21,696,407) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 803,790 | 652,633 |
| 35. Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 0 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **27,196,451** | **26,173,510** |
| | | |
| 38.Dhima Zisizo Dhahiri | 15,901,868 | 20,521,840 |
| 39. Mikopo Chechefu | 14,785,368 | 10,728,165 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,277,609 | 2,277,609 |
| 41. Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| | | |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 11% | 11% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 9.2% | 6.8% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 80% | 80% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 67% | 67% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 76% | 74% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 2% | 2% |
| (vii) Ongezeko la Mali | 3% | 1% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2019**

| | SHS'000 Robo ya Mwaka sasa | SHS'000 Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | SHS'000 Limbikizo la Mwaka wa sasa | SHS'000 Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | **30 - 09 - 2019** | **30 - 09 - 2018** | **30 - 09 - 2019** | **30 - 09 - 2018** |
| 1. Mapato yatokanayo na Mikopo | 4,615,437 | 4,902,112 | 14,294,841 | 14,316,197 |
| 2. Gawio la Faida kwa waweka Amana | (1,390,509) | (1,665,119) | (4,423,951) | (5,061,402) |
| 3. Mapato Halisi ya Mikopo (1kutoa 2) | **3,224,928** | **3,236,993** | **9,870,890** | **9,254,795** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | - | 99,359 | (286,519) | (108,550) |
| | | | | |
| **6. Fiada isiyotokana na Mikopo:** | **1,523,668** | **1,538,548** | **5,416,546** | **5,155,403** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 332,199 | 181,364 | 1,429,442 | 685,657 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,191,469 | 1,357,184 | 3,987,104 | 4,469,746 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **7. Gharama za Uendeshaji:** | **(4,646,502)** | **(4,294,475)** | **(13,801,230)** | **(13,226,680)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,489,481) | (2,092,251) | (6,944,673) | (5,972,128) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,157,021) | (2,202,224) | (6,856,557) | (7,254,552) |
| 8. Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | 102,094 | 580,425 | 1,199,687 | 1,074,968 |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | 49,062 | - | (395,897) | (20,000) |
| **10. Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **151,157** | **580,425** | **803,790** | **1,054,968** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **151,157** | **580,425** | **803,790** | **1,054,968** |
| | | | | |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 243 | 210 | 243 | 210 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 15. Idadi ya Matawi | 9 | 8 | 9 | 8 |
| | | | | |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.06% | 0.27% | 0.34% | 0.5% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 0.4% | 1.6% | 3.0% | 3% |
| (iii) Uwiano wa Gharama za Uendeshaji na Mapato Ghafi | 76% | 67% | 70% | 68% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya yatokanayo na Mikopo na Wastani wa Mali | 2% | 2% | 5% | 7% |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2019**

| | SHS'000 Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30 - 09 - 2019 | SHS'000 Robo Mwaka Uliopita 30 - 06 - 2019 |
|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 102,094 | 560,484 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | 0 | |
| - Hasara Katika Mali | 1,097,360 | 771,320 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (3,546,975) | (2,319,012) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 4,103,953 | 4,514,496 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| - Mabadiliko ya kiwango kinachohitajika na banki kuu kisheria | (1,728,503) | (274,025) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,196,639 | 1,767,964 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (60,372) | (892,133) |
| - Kodi Iliyolipwa | (32,986) | (32,986) |
| - Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **1,131,210** | **8,734,132** |
| | | |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (71,366) | (1,280,995) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (21,122) | 0 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(92,488)** | **(1,280,995)** |
| | | |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | 0 | 0 |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | 0 | 0 |
| | | |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 1,038,722 | 7,453,137 |
| | | |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 44,707,439 | 37,254,302 |
| | | |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **45,746,161** | **44,707,439** |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2019**

Distributed via ippmedia

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2019 | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **39,697,089** | 0 | **(17,465,000)** | **2,843,597** | **1,316,975** | 0 | **26,392,661** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 803,790 | 0 | 0 | 0 | 803,790 |
| Share zilizouzwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (5,192,860) | 5,192,860 | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 1,316,975 | 0 | (1,316,975) | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **39,697,089** | 0 | **(20,537,095)** | **8,036,457** | **0** | **0** | **27,196,451** |
| | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mwaka Uliopita 2018 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwanzo wa Mwaka** | **35,697,280** | 0 | **(16,686,216)** | **3,451,838** | **1,263,376** | 0 | **23,726,278** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 616,493 | 0 | 0 | 0 | 616,493 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 3,999,809 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3,999,809 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 608,241 | (608,241) | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | (53,599) | 0 | 53,599 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **39,697,089** | 0 | **(17,465,000)** | **2,843,597** | **1,316,975** | **0** | **26,392,661** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.

Jina na cheo

**Dr. Muhsin Salim Masoud**
Mkurugenzi mtendaji — Imesainiwa Oktoba 29, 2019

**CPA Said Mshana**
Kaimu Mkuu wa Fedha — Imesainiwa Oktoba 29, 2019


**CPA Mwinyi sekro**
Mkuu wa Ukaguzi — Imesainiwa Oktoba 29, 2019

Benki ilitozwa faini ya SH 618,000 kwa kutofuata utaratibu wa utayarishaji, ufungaji na uandaaji wa fedha kama ilivyoanishwa kwenye sheria husika ya Benki kuu ya mwaka 2015"

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Abdallah Nahdi**
Mwenyekiti — Imesainiwa Oktoba 29, 2019

**Abdullatif Essajee**
Mkurugenzi — Imesainiwa Oktoba 29, 2019



# TANGAZO

Amana Bank
*Together, on the right path*

## Tariff Guide

| | PRODUCT/SERVICES | LOCAL CURRENCY (TZS) | FOREIGN CURRENCY |
|---|---|---|---|
| 1 | **SAVINGS ACCOUNT (Personal/Joint/Annisaa Account)** | | |
| | Minimum Opening balance | 20,000 | USD 100 |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | USD 100 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD 1,000 |
| | Limit on Withdrawal | No limit | No limit |
| | Monthly Maintenance Fee | 1,500 | USD 4 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | Below USD 1,000 - 0% Over USD 1,000 - 0.25% |
| | Over the counter withdrawal limit (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 4 Per Statement |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | USD 10 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 2 | **STUDENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 10,000 | N/A |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | N/A |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | N/A |
| | Limit on Withdrawal | No limit | N/A |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal limit ( above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | Free | N/A |
| | Bank Statements (monthly, quarterly, annually) | Free | N/A |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | N/A |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | N/A |
| | Electronic Statement | Free | N/A |
| 3 | **KILIMANJARO DIASPORA ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 200,000 | USD 100 |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | USD 100 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD 1,000 |
| | Limit on Withdrawal | No limit | No limit |
| | Monthly Maintenance Fee | 1,500 | USD 4.0 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | 1.2% minimum USD 6 |
| | Over the counter withdrawal limit ( above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly, quarterly, annually) | Free | USD 4.0 Per Statement |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 10 Per Statement |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | Free |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 4 | **ASHRAF ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | Free | Free |
| | Account Maintenance balance | 2,000,000 | USD/GBP/EURO 1,000 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD 1,000 |
| | Monthly Maintenance Fee | 10,000 | USD/GBP/EURO 10 |
| | Over the counter withdrawal fee | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly, quarterly, annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 4.0 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| | Hajj Time SMS Alert | Free | Free |
| 5 | **BODABODA ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | Free | N/A |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | N/A |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | N/A |
| | Limit on Withdrawal | No limit | N/A |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | N/A |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | N/A |
| | Over the counter withdrawal limit ( above TZS 10,000,000 ) | Above 10,000,000 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Over the counter balance enquiry fee | Free | N/A |
| | Bank Statements (monthly, quarterly, annually) | Free | N/A |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | N/A |
| | Bank Statements above twelve months | 20,000 per statement | N/A |
| | Electronic Statement | Free | N/A |
| 6 | **HAJJ SAVINGS ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 10,000 | USD 50 |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | USD 50 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD 1,000 |
| | Limit on Withdrawal | Once Annually | Once Annually |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | Free |
| | Over the counter withdrawal fee | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| | Hajj Time SMS Alert | Free | Free |
| 7 | **NURU SAVINGS ACCOUNT (Children Account)** | | |
| | Minimum Opening balance | 10,000 | USD 50 |
| | Account Maintenance balance | 10,000 | USD 50 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD 1,000 |
| | Limit on Withdrawal | Four times in a year | Four times in a year |
| | Charge on withdrawal exceeding 4 times a year | 12,000 | USD 6 |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | Free |
| | Over the counter withdrawal limit (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | N/A |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 8 | **SALARY SAVINGS ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 0 | 0 |
| | Account Maintenance balance | 2,000 | USD 5 |
| | Profit Participation Balance (Min. Daily balance) | 100,000 | USD 1,000 |
| | Monthly Maintenance Fee | 1,500 | USD 1.5 |
| | Over the counter withdrawal limit (above TZS 10,000,000) | 0.18% of the whole amount, Minimum TZS 18,000 Maximum 180,000 Fee may be waved if a prior notice of atleast 5 days is given | NA |
| | Over the Counter limit withdrawal Fee | 1,500 | Below USD 1,000 - 0% Over USD 1,000 - 0.25% |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | NA |
| 9 | **PERSONAL CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 100,000 | USD 100 |
| | Account Maintenance balance | 50,000 | USD 50 |
| | Monthly Maintenance Fee | 11,000 | USD 11 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | Below USD 1,000 - 0% Over USD 1,000 - 0.25% |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 10 | **CORPORATE CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 100,000 | USD 500 |
| | Account Maintenance balance | 50,000 | USD 200 |
| | Monthly Maintenance Fee | 15,000 | USD 15 |
| | Over the counter withdrawal fee | 2500 | Below USD 1,000 - 0.5% Over USD 1,000 - 0.5% |
| | Activation of Dormant Account | Free | Free |
| | Certificate of Balance to Auditors/Reference letters | 50,000 | USD 25 |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 11 | **BIASHARA CURRENT ACCOUNT (SMEs)** | | |
| | Minimum Opening balance | 100,000 | USD 100 |
| | Account Maintenance balance | 50,000 | USD 50 |
| | Monthly Maintenance Fee | 13,000 | USD 13 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | Below USD 1,000 - 0.5% Over USD 1,000 - 0.5% |
| | Certificate of Balance to Auditors/Reference Letters | 50,000 | USD 25 |
| | Activation of Dormant Account | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 6,000 Per Statement | USD 4 Per Statement |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 12 | **NGO CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 100,000 | USD 100 |
| | Account Maintenance balance | 0 | 0 |
| | Monthly Maintenance Fee | 0 | 0 |
| | Over the counter withdrawal fee | 1,500 | 1.2% Minimum USD 6 |
| | Certificate of Balance to Auditors/Reference Letters | 50,000 | USD 25 |
| | Activation of Dormant Account | Free | Free |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 2,000 Per Page | USD 1 Per Page |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 13 | **IHSAAN CURRENT ACCOUNT** | | |
| | Minimum Opening balance | 0 | 0 |
| | Account Maintenance balance | 0 | 0 |
| | Over the counter withdrawal fee | 0 | 0 |
| | Bank Statements (monthly, quarterly annually) | Free | Free |
| | Second and Subsequent bank statement copy(ies) | 2,000 Per Page | USD 1 Per Page |
| | Monthly Maintenance Fee | Free | Free |
| | Electronic Statement | Free | Free |
| 14 | **FIXED/TERM DEPOSITS** | | |
| | Minimum Opening balance | 1,000,000 | USD 1,000 |
| | Profit Participation Balance | Amount placed | Amount placed |
| | Limit on Withdrawal | Until maturity | Until maturity |
| | Certificate of Investment | Free | Free |
| | Certificate of Balance to Auditors | 50,000 | USD 25 |
| 15 | **OTHER DEPOSIT SERVICES** | | |
| | Over the counter balance enquiry fee (for all a/cs) | Free | Free |
| | Account Closure Fee (for all account types) | 10,000 | USD 10 |
| | Activation of Dormant Accounts | Free | Free |
| | Cash deposits for all account types | Free | Free |
| | Cash deposits for small denominations (less than USD 50) | N/A | 5% of total |
| | Withdraw by using counter cheque :Forgotten/ loss/stale | 15,000 | USD 7 |
| 16 | **CHEQUE BOOKS** | | |
| | Issuance: 100 leaves cheque book | 60,000 | USD 35 |
| | Issuance: 50 leaves cheque book | 30,000 | USD 20 |
| | Issuance: 25 leaves cheque book | 15,000 | USD 10 |
| | Stop Payment of Cheque | 40,000 | USD 35 |
| | Unpaid Cheque - Insufficient fund and uncleared effect | 100,000 | USD 50 |
| | Unpaid Cheque - technical reason | Free | Free |
| | Uncollected Cheque book after advice period of 3 months | 20,000 | USD 12 |
| 17 | **BANKERS CHEQUE/ PAYMENT ORDER/ BANK / DEMAND DRAFTS** | | |
| | Issuance: For Account holder | 30,000 | USD/GBP/EURO 25 |
| | Cancellation: For Account holder | 30,000 | USD/GBP/EURO 25 |
| | Stop Payment | 40,000 | USD/GBP/EURO 35 |
| 18 | **ATM/DEBIT CARD** | | |
| | Issuance of ATM card fee | 10,000 | N/A |
| | Renewal of expired ATM card | Free | N/A |
| | Replacement of lost/stolen or damaged card | 10,000 | N/A |
| | Replacement of PIN | 10,000 | N/A |
| | Annual fee | Free | N/A |
| | ATM card activation | Free | N/A |
| | Blocking/Hotting ATM card | Free | Free |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction at AMANA BANK and CRDB | 1,300 | N/A |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction Mastercard local | 4,000 | N/A |
| | ATM Cash Withdrawal fee per transaction Mastercard international | 7,300 | N/A |
| 19 | **FUND TRANSFERS/REMITTANCES** | | |
| | Internal Transfers within Amana Bank | Free | Free |
| | Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward USD | N/A | USD 50 |
| | Inward Transfers (TT, SWIFT) | Free | USD 12 |
| | Amendment of TT, SWIFT Message | 12,000 | USD 12 |
| | Confirmation | Free | Free |
| | TISS | 12,000 | USD 12 |
| | EFT (Bulk Payments): Out&Inward/salary processing fee | 3,000 per transaction | USD 2 per transaction |
| | Stop Payments (TISS/EFT/SWIFT) | 20,000 | USD 20 |
| 20 | **STANDING ORDERS** | | |
| | Standing Order Instructions within Amana Bank | Free | Free |
| | Standing Order Instructions - Outward | 12,000 per instruction | USD 12 per instruction |
| | Standing orders - Cancellation/Stopping | Free | Free |
| | Standing Orders - Amendments | Free | Free |
| | Unpaid Standing Orders | 12,000 per instruction | USD 12 per instruction |
| 21 | **INTERNET BANKING** | | |
| | Registration | Free | Free |
| | Equipment (one off) per user | 100,000 | USD 60 |
| | Monthly Service Fee (Corporate) | 15,000 | USD 8 |
| | Monthly Service Fee (Personal) | 6,000 | USD 3.6 |
| 22 | **SMS BANKING** | | |
| | Account Balance Enquiry | 300 | N/A |
| | Ministatement | 300 | N/A |
| | Cheque Status Enquiry | 300 | N/A |
| | Cheque book request | 300 | N/A |
| | Internal fund transfer | 1,500 | N/A |
| | Account activity Alert | 100 | N/A |
| | Airtime recharge | 300 | N/A |
| | Utility bill payment | 300 | N/A |
| | All Mobile Network Operators | Up to 100,000 - TZS 1500<br>100,001 - 500,000 - 2500<br>500,001 - 1,000,000 - 3,500<br>1,000,001 - 3,000,000 - 4,500<br>3,000,001 - 5,000,000 - 5,500<br>5,000,001 - Above - 7,500 | N/A |
| 23 | **OTHER SERVICES** | | |
| | SMS Alert fee per transaction | 100 | N/A |
| | Search Old Documents/Document Retrieval charges - between one months and six months | 10,000 | USD 5 |
| | Search Old Documents/Document Retrieval charges - above six months | 30,000 | USD 15 |
| | Retrieval charges on stale Cheques | 20,000 | USD 10 |
| | Quarterly dormant charges | 5,000 | USD 2 |
| | Electronic Schedule of Charges Fee | Free | Free |
| | Change of Address/Telephone numbers | 50,000 | USD 25 |
| | Status opinion (Reference letter,certificate of balance of Auditors,Embassy letter) | 50,000 | USD 25 |
| | Salary processing | 3,000 Per Transaction | USD 2 Per Transaction |
| | Bulk payment Service | 1,300 per transaction | USD 7 per transaction |

**Dr. Muhsin Salim Masoud**
Managing Director.............................................................................................

**Said Mshana**
Ag. General Manager Finance...........................................................................

Distributed via ippmedia



Islamic Bank

*Get foreign currency exchange service conveniently through a special teller in all our branches*

Customer service 0657 980 000 0657 980 000 /amanabanktz /amanabank

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI KANIMALIZA MANENO - VALVERDE

Nini tena kinaweza kusemwa kuhusu yeye? Kipaji chake hakilinganishwi...

**Barcelona, hispania**

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Ernesto Valverde amesema "amemaliza maneno" ya kumwelezea Lionel Messi baada ya nahodha huyo kuonyesha kiwango cha juu wakati akiiwezesha timu hiyo kushinda mabao 5-1 dhidi ya Real Valladolid juzi.

Messi alionyesha kiwango cha juu akifunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho ['assists'] mbili wakati mabingwa watetezi, Barca wakipaa kileleni mwa msimamo wa La Liga juzi, Jumanne.

Nahodha wa Barca, Messi alimtengenezea bao Arturo Vidal kwa pasi murua kabla ya yeye kutupia kwa mpira wa adhabu ndogo hilo likiwa bao lake la 50 la faulo katika wasifu wake kisoka kwa klabu na timu ya Taifa ya Argentina, akilifunga kabla ya kipindi cha kwanza kwenye mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Camp Nou.

Messi alifunga bao lake la pili kwenye mechi hiyo baada ya mapumziko na mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or alimtengenezea tena mchezaji mwenza, Luis Suarez wakati ikipanda juu ya Granada na Atletico Madrid na kukaa kileleni mwa LaLiga.

"Nini tena kinaweza kusemwa kuhusu yeye? Nimemaliza maneno," Valverde aliwaambia wanahabari. "Mara zote tunajua atatokea, kwa vyovyote mechi itakavyokuwa.

"Kipaji chake hakilinganishwi na kitu chochote; ukweli ni kwamba kila wakati anapogusa mpira, kitu cha kipekee hufanyika. Sijui cha kusema."

Valverde aliongeza: "Anakaribia kiwango chake bora [baada ya kuwa majeruhi], wakati Leo anapata [mpira] kitu kibaya kinatokea kwa wapinzani.

"Ana kipaji hicho ambacho hamna yeyote aliye nacho, anamkwepa kila mmoja na siyo hilo tu kwamba anaweza kucheza binafsi bali anafanya vitu ambavyo hakuna mtu anaviona.

"Inatokea kwangu mara nyingine, anafanya vitu ambavyo havionekani na wengi, kila siku ni bora."

Ingawa bao la kwanza la Barca la dakika ya pili ya mchezo kupitia kwa Clement Lenglet lilisawazishwa na Valladolid dakika ya 13 kupitia kwa Kiko Olivas, Messi aliweza kuwang'arisha Barca dhidi ya wageni wao hao.

Barca ina pointi mbili mbele ya Granada na Atletico Madrid, ambayo imecheza mechi moja zaidi kufuatia mchezo wa El Clasico kuahirishwa mwishoni mwa wiki iliyopita.

"Tunathamini sana kile tunachokifanya," Valverde aliongeza. "Tunayo kwenye kumbukumbu kile tulichokifanya lakini tunataka kutazama mbele na kushinda ligi hii.

"Si rahisi kupeleka michezo mbele, Valladolid imetoka sare dhidi ya Atletico na Real Madrid na si rahisi kuwafunga. "

## KWA UFUPI

**MANDZUKIC KIMEELEWEKA UNITED**

Manchester United ni kama imekamilisha mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Juventus na Croatia, Mario Mandzukic, 33, kuelekea dirisha la Januari. ***(Tuttomercatoweb, via Express)***

**ARSENAL, LIVER KWA ZAKARIA**

Arsenal, Liverpool na Manchester United zimekuwa zikiwasiliana na kiungo wa Borussia Monchengladbach, Mswisi Denis Zakaria, 22. ***(Sky Deutschland, via Inside Futbol)***

**JESUS AIKANA BAYERN**

MSHAMBULIAJI wa Manchester City na Brazil, Gabriel Jesus, 22, amepuuzia tetesi zinazomhusisha na kujiunga na Bayern Munich, akiandika kupitia mtandao wake wa Instagram uvumi huo ulikuwa "uwongo". ***(Manchester Evening News)***

**SALAH, SON WAMULIKWA JUVE**

Juventus imetuma mashushushu wake wa kusaka vipaji kwenda kutazama mechi ya Liverpool dhidi ya Tottenham lengo likiwa ni kumtazama mshambuliaji Mmisri Mohamed Salah, 27, straika wa Tottenham na Korea Kusini, Son Heung-min, 27, na kiungo wa Spurs, Mdenmark Christian Eriksen, 27. ***(Tuttosport, via Mirror)***

**HAZARD AFICHUA DILI LAKE**

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Ubelgiji, Eden Hazard, 28, amefunguka kwamba alizungumza na Rais wa Real Madrid, Florentino Perez kwa mwaka mzima kabla ya kukamilisha usajili wake wa kutua klabuni hapo akitokea Chelsea. ***(Talksport)***

**XHAKA BADO NAHODHA ARSENAL**

KIUNGO wa Arsenal, Mswisi Granit Xhaka, 27, ataendelea kuwa nahodha wa klabu hiyo licha ya kuonekana akikwaruzana na mashabiki wa Gunners wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 nyumbani dhidi ya Crystal Palace Jumapili. ***(Times)***

**IBRAHIMOVIC KUTIMKIA LALIGA**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Manchester United na Sweden, Zlatan Ibrahimovic, 38, amefunguka kuwa atajiunga na kalabu ya La Liga baada ya miezi 18 ya kuitumikia LA Galaxy. ***(Metro)***

**DER VAART AVUTIA ZIYECH SPURS**

KIUNGO wa zamani wa Tottenham, Rafael van der Vaart amekiri kwamba amemwambia Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy kumsajili kiungo mshambuliaji wa Ajax na Morocco, Hakim Ziyech, 26. ***(Star)***

**NEWCASTLE YAJITOSA KWA SISSOKO**

Newcastle ipo tayari kumsajili kiungo mwenye urefu wa futi sita na inchi nne (6ft 4in) Mfaransa Ibrahima Sissoko, 21, kwa dau la pauni milioni 13 kutoka klabu ya Ligue 1, Strasbourg. ***(Sun)***

**UNITED YAONGOZA KWA HAALAND**

Manchester United imeibuka na kuongoza mbio za kumsajili mshambuliaji wa Red Bull Salzburg na Norway, Erling Braut Haaland, 19. ***(Corriere dello Sport, via Manchester Evening News)***

**LYON YAMUULIZIA GIROUD**

Lyon imefanya mawasiliano na wakala wa Oliver Giroud, 33, kuhusu uwezekano wa kuipata saini ya mshambuliaji huyo wa Chelsea na Ufaransa katika dirisha la usajili la Januari. ***(Soccer Link, via Football.London)***

**EVERTON YAMTAKA KRAL**

Everton inamfuatilia kiungo wa Jamhuri ya Czech na klabu ya Spartak Moscow, Alex Kral, 21. ***(Clubcall)***

## HABARI MICHEZO

# PONDAMALI ALIA YANGA KUMZUNGUSHA KUMLIPA

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA wa zamani wa makipa wa klabu ya Yanga, Juma Pondamali amepaza sauti yake kuilalamikia klabu hiyo kwa kumzungusha kumlipa mshahara wake wa miezi saba kwa muda sasa.

Akizungumza na mwandishi wetu, Pondamali alisema aliachana na klabu hiyo akiwa anaidai na hadi sasa hajalipwa malimbikizo ya mshahara wake wa miezi saba huku akiambulia majibu ya kibabe wakati akidai kulipwa haki yake hiyo.

"Ninaidai hela nyingi na mara nyingine ukidai unalipwa kidogo kidogo kama laki ama laki mbili, sasa zitaisha lini? Pili inaniuma maana majibu ninayopewa yanauzi sana," alisema.

"Unajua mimi ni mtu mzima unapopewa majibu ya kibabe mara tupo 'bize' tunaiandaa timu ama tunataka kuwalipa wachezaji kwanza, haifurahishi."

Pondamali alisema ana nyaraka zote muhimu zinazoonyesha kuidai Yanga na kwamba sasa anapanga kwenda mamlaka nyingine ili kupata msaada wa kulipwa haki yake.

Alipoulizwa Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli kuhusu madai hayo ya Pondamali alisema, kwa sasa hana muda wa kulizungumzia hilo kwa kuwa wapo bize na maandalizi ya kuisafirisha timu kuelekea Misri kwenye mechi ya marudiano dhidi ya Pyramids kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# MANULA ATISHA REKODI AKIPIGA YA 100 SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

Kipa wa Simba, Aishi Manula ametisha kwa rekodi ya kutorushu bao ['Clean Sheets'] wakati jana akitimiza mechi ya 100 akiwa na klabu ya Simba alipokaa golini dhidi ya Mwadui FC.

Manula ametimiza idadi hiyo ya mechi akiwa na timu hiyo baada ya kujiunga nayo rasmi Agosti Mosi 2017 akitokea Azam FC.

Kwa mujibu wa rekodi zetu ni kwamba idadi hiyo ni ya mechi zote za Ligi Kuu na michuano mbalimbali kama Kombe la Kagame, Mapinduzi Cup, Ligi ya Mabingwa, Kombe la Shirikisho na mingine.

Katika mechi hizo, ambazo ameondoka uwajani bila kuruhusu bao ni 59, na mechi ambazo timu yake imeondoka na ushindi alipokaa golini ni 67.

Mechi ambazo Manula alizokaa golini Simba ikiambulia vipigo ni 12 na mechi 20 alikaa timu yake ikitoka sare. Hii ni kabla ya mechi ya jana dhidi ya Mwadui FC iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga.

Manula alizaliwa Septemba 13 mwaka 1995 mkoani Morogoro na kuanza kusakata kabumbu kwenye nafasi ya mlindamlango akiwa na klabu ya Mkamba Rangers iliyopo Kirombero mkoani humo.

Alijiunga na Azam FC mwaka 2012 akiwa na umri wa miaka 17 tu na hii ni baada ya kuonekana kwenye michuano ya vijana akiwa na timu ya Mkoa wa Morogoro, viongozi wa Azam FC walipomuona na kumchukua kwenye kikosi cha pili, lakini muda mfupi tu baadaye alipandishwa kikosi cha kwanza.

# Waandishi michezo wanawake wafundwa

**Na Shufaa Lyimo**

WAANDISHI wa habari za michezo wanawake wametakiwa kuwa mstari wa mbele katika kulitangaza soka la wanawake kwa lengo la kulifikisha mbali zaidi ili kufuta dhana potofu kuwa wanaume pekee ndio wanaweza soka.

Ushauri huo ulitolewa na mkufunzi wa semina ya waandishi wa habari za michezo wanawake, Asha Omogisha kutoka Uganda iliyoanza jana katika Hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam.

Aidha, Omogisha aliwataka waandishi hao kufanya kazi kwa weledi hususan kwa upande wa michezo kwa kuandika habari zenye ubunifu huku akiwasisitizia kuongeza elimu kwa kujifunza lugha mbalimbali ili kuweza kuelewana vema pindi wanapokutana na wachezaji kutoka mataifa mbalimbali.

**"Mnapaswa kuelimisha Watanzania wajue kuwa soka si la wanaume pekee bali hata wanawake wana uwezo mkubwa wa kucheza mpira," alisema mkufunzi huyo.**

Pia alilipongeza Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kitendo cha kuwaandalia semina hiyo waandishi wa habari za michezo wanawake, kwa kuwa itawasaidia kwa kiasi kikubwa.

"Mnapaswa pia kuvaa mavazi yenye staha pamoja na kuongea lugha za busara ambazo zitakufanya ukubalike kwenye jamii kwa kitu unachokifanya," alisema.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Soka la Wanawake Tanzania, Amina Karuma, aliishukuru TFF kwa kuhakikisha soka la wanawake linasonga mbele.

"Lengo letu ni kuhakikisha soka letu la wanawake linafika mbali na kuweza timu zetu kushiriki mashindano makubwa kwa mfano mikoani wengi hawajui soka la wanawake, kwa hiyo tunaomba mfikishe ujumbe vizuri katika jamii,"alisema Amina.

# Mshindi ndinga ya SportPesa huyu hapa

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya Michezo na Burudani ya SportPesa kwa kushirikiana na mtandao wa Tigo wamemaliza rasmi Promosheni ya Faidika na Jero kwa kuchezesha droo ya wiki ya sita na kisha kuwapata washindi saba wa simu na mshindi mmoja wa gari aina ya Renault Kwid.

Promosheni hiyo ilidumu kwa muda wa wiki sita na kupata washindi 41. Washindi 40 wakiwa wa simu aina ya Samsung A10s na mmoja wa gari aina ya Renault Kwid.

Yusuph Jackson (29), Mkazi wa Mugumu, Serengeti ndiye aliyeibuka mshindi wa gari mpya ambayo haijatembea kilometa hata moja baada ya droo iliyokusanya washindi wa siku 40.

SportPesa kwa kushirikiana na Tigo kupitia huduma ya TigoPesa iliwapa nafasi wateja wake kujishindia zawadi hizo mara baada ya kuweka ubashiri wao na kuingia kwenye droo ya kila wiki na kujishindia zawadi hizo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas alisema: "Kwanza kabisa napenda kuwashukuru sana Watanzania na wateja wetu wote kwa kushiriki kwenye promosheni hii iliyodumu kwa siku 40.

"Kwa kupitia mtandao wa Tigo na huduma ya Tigo Pesa tumeweza kuzawadia wateja wetu na kuwahamisha kwenye huduma za kidigitali ili kuwafungulia njia zaidi"

"Niwaahidi wateja wetu kupitia mitandao mbalimbali kwamba huu ni mwanzo tu maana mambo ndio kwanza yameanza nikimaanisha wakae mkao wa kula kutokana na kwamba SportPesa kila siku tunaleta vitu vipya kwa ajili ya wateja wetu."

Kwa upande wa Tigo, Meneja wa Kitengo cha Huduma za Kidigitali, Ikunda Ngowi, alisema: "Kwa niaba ya Tigo ningependa kuwapongeza washiriki wetu wote wa promosheni hii na kuonyesha ushirikiano mkubwa kuanzia mwanzo wa promosheni hadi mwisho na ningependa kuwaomba waendelee kutumia huduma zetu hasa kwenye kubashiri na SportPesa."

Kwa siku 40 Sportpesa imeweza kuwazawadia washindi kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Mtwara, Lindi, Manyara na Serengeti.



Distributed via ippmedia

Mchezaji wa Yanga B, Mohamed Othuman (kushoto), akiwania kumtoka mchezaji wa Dege FC, wakati wa usaili wa kutafuta vijana wenye vipaji kwenda kucheza nje ya nchi uliofanyika katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Michezo

Alhamisi Oktoba 31, 2019

Nipashe


## Messi kanimaliza maneno - Valverde

HABARI UK 30

KAZI KWELI...




Kiungo wa Simba, Mzambia Clatous Chama (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Mwadui, Augustino Samson katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani Shinyanga na Simba kulala 1-0. **PICHA :SOMOE NG'ITU.**

# SABABU ZA KUMNG'OA ZAHERA YANGA NI HIZI

●●●Zatajwa huku ikielezwa sasa hatanusurika, kikosi chapaa alfajiri kuifuata Pyramids huku Mwakalebela akitangulia kuweka...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Yanga imekwea pipa leo alfajiri kuifuata Pyramids ya Misri kwenye mechi ya marudiano ya mchujo ya kuwania kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika joto la mashabiki wa klabu hiyo kutaka Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mwinyi Zahera atimuliwe limeendelea kupanda.

Mbali na joto hilo kupanda, sasa zimetajwa sababu muhimu ambazo haziwezi kumbakisha Mkongomani huyo katika kikosi hicho cha mtaa wa Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam ambacho kimeifuata Pyramids kwa ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia.

Mashabiki wa Yanga walikerwa na kitendo cha timu yao kuchapwa mabao 2-1 na Pyramids FC ya Misri kwenye mechi ya awali iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba mwishoni mwa wiki, hivyo kuanza kuimba uwanjani hapo "Zahera aondoke, Zahera aondoke" na kisha kumtupia chupa za maji baada ya mechi kumalizika.

Hata hivyo, mjumbe mmoja wa Kamati ya Utendaji wa klabu hiyo ambaye aliomba hifadhi ya jina lake, aliliambia Nipashe kuwa kwa namna upepo ulivyo Zahera atatimuliwa kwa kuwa siku zote alikuwa akibebwa na mashabiki lakini sasa wamemkataa hivyo hana pakuegemea

"Pamoja na kushindwa kuiunganisha timu, lakini uongozi ulimvutia pumzi kwa kuwa alikuwa anakubalika sana na mashabiki, kumbuka wakati tunajiandaa na mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Township Rollers ya Botswana mikoa ya kaskazini alivyoudhalilisha uongozi.

"Alipendekeza timu iweke kambi maeneo yenye baridi ili kuzoea hali ya hewa ya baridi iliyokuwa Botswana wakati huo, lakini badala yake akauponda uongozi kuwa kambi hiyo ilikuwa kimaslahi zaidi na si kwa ajili ya kuiandaa timu, hata hivyo alivumiliwa kwa kuwa mashabiki walikuwa wanamkubali," alisema mjumbe huyo.

"Lakini pia alipendekeza mwenyewe wachezaji wa kusajiliwa, na awali wakati viongozi wakihangaika kufanya mazungumzo kubakisha baadhi ya wachezaji akiwamo Gadiel Michael na Ben Kakolanya alisema hata wakiondoka wote atasajili wazuri zaidi, lakini leo ndiye anasema hakusajili kwa ajili ya michuano ya kimataifa, inamaana tukitwaa bingwa atafukuza wote ili sasa asajili wa michuano ya kimataifa?"

Mjumbe huyo aliendelea kusema sababu nyingine ya Zahera kupaswa kung'oka Yanga ni kuzidi uswahili badala ya kuelekeza akili yake katika kuiandaa timu ambayo ina wachezaji wazuri lakini ikishindwa kucheza soka la kueleweka.

Aliongeza kuwa kocha huyo hutumia muda mwingi kula 'bata' Ufaransa na kuacha majukumu kwa kocha msaidizi, Noel Mwandila wakati akijua timu inakabiliwa na mashindano makubwa. Juzi mchambuzi wa soka nchini na Mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya Yanga aliyewahi kuitumikia klabu hiyo kwa mafanikio makubwa, Ally Mayay licha ya kuionya klabu hiyo ikitaka kuwa makini kwa maamuzi watakayoyafanya kuhusu kumtimua Zahera kuwa yanaweza kuigharimu timu, pia alikiri kocha huyo kushindwa kuiunganisha timu.

Mayay alisema ni kweli kwa sasa Yanga inacheza soka bovu ukilinganisha na msimu uliopita ikiwa na kocha huyo huyo ambaye kabla ya msimu kuanza alipewa nafasi ya kufanya usajili wa wachezaji anaowataka tofauti na aliowakuta msimu uliopita.

Kwa upande wake Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli akizungumzia safari ya timu hiyo kuelekea Misri alisema, timu imeondoka na wachezaji 20 pamoja na viongozi saba wakiongozwa na Mkuu wa Msafara kutoka Shirikisho la Soka nchini (TFF), Vedasto Lufano, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Mwanza, MZFA.

"Tayari Makamu Mwenyekiti wetu, Frederick Mwakalebela ametangulia huko tangu leo asubuhi (jana asubuhi) kwa ajili ya kwenda kuandaa mazingira ya timu itakaposhukia," Bumbuli alisema.

## Simba yatobolewa

**Na Somoe Ng'itu, SHINYANGA**

MWADUI imekuwa timu ya kwanza kuwatoboa mabingwa watetezi, Simba baada ya kushinda bao 1-0 katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Kambarage mkoani hapa.

Kwa matokeo hayo, Simba imebakia na pointi zake 18 baada ya kucheza mechi saba huku Mwadui walioshuka dimbani mara tisa wakifikisha pointi 11 na hiyo ikiwa mechi yao ya pili kushinda msimu huu.

Bao la Mwadui FC lilifungwa dakika ya 32 na Gerald Mathias kwa kichwa baada ya kumtizama kipa wa Simba, Aishi Manula, akiwa ametoka katika eneo lake na kuunganisha nyavuni krosi iliyopigwa na Hassan Kapalata.

Hadi timu hizo zinakwenda mapumziko, wenyeji Mwadui ambao wanafundishwa na Kocha Mkuu Khalid Adam, walikuwa mbele kwa bao hilo moja lililowapa pointi tatu muhimu baada ya kushindwa kutamba katika michezo mitatu iliyopita wakiwa nyumbani.

Mwadui ilianza kwa kasi katika mchezo huo wakifanya shambulizi la kwanza dakika ya tatu kupitia kwa Omar Daga, lakini Manula alipangua shuti hilo na kuwanyima wenyeji hao bao la mapema.

Dakika ya 16 kiungo wa kimataifa kutoka Sudan, Sharaf Eldin Shiboub akipaisha juu akiwa kwenye nafasi nzuri ya kufunga na kupoteza kazi nzuri iliyofanywa na Mzambia Clatous Chama.

Mzambia huyo alipiga pasi nyingine nzuri kwa Muzamiru Yassin lakini kiungo huyo alipiga shuti pembeni na kupoteza nafasi nyingine ya kufunga dakika ya 26 na dakika iliyofuata Yassin alipiga shuti safi lakini kipa wa Mwadui FC, Mahmoud alipangua mpira huo na kuliweka lango lake salama.

Mathias alikaribia kufunga bao lingine baada ya kupiga vema mpira lakini beki wa Simba, Gadiel Michael aliokoa hatari hiyo ikiwa ni dakika ya 42 na dakika mbili baadaye Manula akadaka shuti la mshambuliaji huyo.

Baada ya Simba kuwa nyuma, benchi la ufundi liliwasimamisha Ibrahim Ajibu, Miraji Athumani na Hassan Dilunga na wachezaji hao waliingika dakika ya 46 isipokuwa Ajibu na kuanza kulishambulia lango la Mwadui mara kwa mara.

Baada ya mechi ya jana, Simba inatarajia kurejea jijini Dar es Salaam kuwasubiri Mbeya City katika mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa Novemba 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042


9 770856 541002 >